

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 1 Juni, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:-

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu.

NDG. PAMELA PALANJO - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 351

**Wahitimu wa Vyuo vyaa Ufundu
Kuelekea Uchumi wa Viwanda**

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA aliuliza:-

Wapo wahitimu wengi sana kutoka Vyuo mbalimbali vyaa Ufundu nchini ambapo hadi sasa hawajapata ajira wala hawajaweza kujiajiri, ikiwa pia tuko kwenye wakati wa kuanzisha uchumi wa viwanda ambapo taaluma za wahitimu hao zinahitajika sana:-

Je, ni lini Serikali itafanya juhudzi za dhati za kushughulikia suala hili kwa lengo la kuongeza tija?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha tatizo hili linapungua kwa kiasi kikubwa, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kukabiliana na changamoto hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha kuwa vijana wahitimu wa Vyuo vya Ufundi wanapata fursa za ajira katika miradi mikubwa ya maendeleo kama vile ujenzi wa reli ya *Standard Gauge*, ujenzi wa bomba la mafuta, mradi wa usambazaji wa umeme vijijini, mradi wa kufufua umeme na mingine. Mathalan, katika ujenzi wa bomba la mafuta, uchambuzi umeonyesha kutakuwa na fursa za ajira zaidi ya 11,000 za aina mbalimbali. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Ajira (*TaESA*) inaratibu upatikanaji wa Watanzania wenye sifa za kuajirika katika miradi hiyo.

(ii) Kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini, Serikali imeainisha aina ya ujuzi unaohitajika katika ujenzi wa miradi husika na imetenga fedha za kugaramia kuziba ombwe la ujuzi lililopo kati ya wahitimu na mahitaji ya soko la ajira kuwezesha Watanzania wakiwemo wahitimu wa Vyuo vya Ufundi kupata sifa na kuajirika.

(iii) Kuendelea kuhamasisha na kuwawezesha vijana kujiajiri kwa kuanzisha makampuni na vikundi vya uchumi vilivyosajiliwa kisheria ili kutumia taaluma zao kuzalisha na kujipatia vipato halali. Kwa mfano, Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini (*REA*) umetoa fursa za ajira kwa vijana wengi wenye ufundi. Aidha, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Taasisi nyingine za Serikali, Serikali imeendelea kutoa mikopo yenyenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana ili kuwajengea mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa tunapoolekea katika uchumi wa viwanda taaluma za wahitimu wa vyuo vya ufundi zitaendelea kuhitajika sana kwa ajili ya uendeshaji endelevu wa viwanda vitakavyoanzishwa. Serikali imeona jambo hilo na kwa kushirikiana na vyuo vya ufundi imeanza kutoa mafunzo kwa kuzingatia mahitaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kupata majibu hayo ya kina ambayo yameelezea vizuri sana juu ya miradi muhimu kama hiyo *REA*, *Standard Gauge* na bomba la mafuta lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, ni kwa nini Serikali isije na utaratibu wa kuwachukua vijana hawa moja kwa moja kutoka kwenye vyuo ili kuwapunguzia mihangai ko ya kuzunguka na barua za maombi na kushinda mitandaoni kama ilivyokuwa kwenye sekta nyingine, mfano, afya na elimu ambapo watu hupata ajira kwa wepesi zaidi kutokana na taaluma zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Wizara hii na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ina mikakati gani kutengeneza mazingira wezeshi ikiwemo *Incubation Centres* za uhakika za kutosha, mitaji, vitendea kazi kwa wahitimu hawa ili waweze kupata wepesi wa kujajiri na vilevile kwenda na Sera yetu ya Tanzania ya Viwanda, Inawezekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza la kuwachukua vijana hawa wahitimu wa vyuo vya ufundi moja kwa moja, tunachokifanya kama Serikali kwanza kabisa kwa kushirikiana na sekta binafsi ambazo pindi nafasi zinapopatikana huwa tunawaunganisha moja kwa moja na vyuo vyetu vya ufundi ili vijana hawa waweze kupata nafasi za ajira za moja kwa moja. Pia baadhi ya vyuo, kwa mfano,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Chuo cha *Don Bosco* kimekuwa kina utaratibu wa kila mwaka kuandaa Kongamano la Waajiri ambapo wamekuwa wakiunganisha wahitimu hawa moja kwa moja na waajiri na vijana wengi wameajiriwa kwa kupitia mfumo huo. Kwa hiyo, naamini kabisa wazo la Mheshimiwa Mbunge ni jema, nasi kama Serikali tutaona namna ya kuweza kuviunganisha vyuo vyetu vya ufundi pamoja na waajiri ili vijana hawa wapate nafasi za ajira za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, suala la *incubation* kwa ajili ya kuwandaan vijana hawa, kuwalea na kuwapatia mitaji, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tunavyo Vituo vya Vijana. Kipo Kituo cha Vijana Sasanda-Mbozi, Ilonga pale Kilosa na Kilimanjaro. Vituo hivi viko kwa ajili ya kuwalea vijana na kuwandaan kuwa na sifa za kuajiriwa. Pia vijana hawa wanawezeshwa kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana ambao umekuwa ukitoa mikopo kwa vikundi vya vijana lakini vilevile na asilimia 5 za mapato ya ndani ya Halmashauri yamekuwa yakisaidia katika kuwakomboa vijana kwa kuwapatia mitaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtolea, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tatizo hili la ajira halipo tu kwa wahitimu wa vyuo vya ufundi, lipo pia kwa wahitimu wengine wa vyuo vikuu hapa nchini. Kwa kuwa wahitimu wengi wa vyuo vikuu tayari ni wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu, kwa maana hiyo ni watu ambao wanaaminika. Kwa nini Ofisi ya Waziri Mkuu isishirikiane na Wizara ya Elimu kuandaa mikopo ya wahitimu ya kuanzia maisha pale ambapo wanamaliza masomo yao ili waweze kujitengenezea fedha ambazo zitasaidia kuendesha maisha yao lakini kurejesha mikopo waliyokopa wakiwa vyuoni. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtalea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuendelea kuwakusanya vijana wahitimu wa vyuo vikuu katika makundi tofauti tofauti na mmoja mmoja ambaao wanaweza kufanya shughuli za kiuchumi na lengo letu ni kuweza kusaidia kufikia malengo yao. Chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu tunalo Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ambapo ndani ya Baraza lile tuna mifuko zaidi ya 19 inayotoa mikopo na *grants*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa vijana wote nchi nzima hasa wahitimu wa vyuo vikuu wenye mawazo mbalimbali ya kibashara, watumie fursa ya uwepo wa Mfuko wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na mifuko mingine ili waweze kujikwamua kiuchumi. Naamini kabisa kwa kutumia Baraza hili itasaidia sana wao kuweza kupata sifa ya kupata ajira lakini vilevile na kutengeneza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili huwa napenda kutoa mfano na naomba nirudie mfano wangu, tunao vijana waliomaliza Chuo Kikuu cha Sokoine pale Morogoro ambaao walipohitimu walijiunga pamoja, wakaunda kampuni, sisi kama Serikali tukawapa dhamana ya mkopo na hivi leo wanafanya kazi kubwa sana katika kilimo cha mboga mboga hapa nchini na wameanza kuwaajiri mpaka vijana wenzao. Kwa hiyo, natoa rai kwa vijana wengine wote kufuata mfano huo na inawezekana kabisa kutimiza malengo yao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Lameck Okumbo Airo, Mbunge wa Rorya sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

Na. 352

Hitaji la Hospitali ya Wilaya-Rorya

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO) aliuliza:-

Wilaya ya Rarya iliyoanzishwa mwaka 2007 sasa ina wakazi wapatao 400,000 na ina kata 26 na vijiji takriban 87 na ina vituo vya afya 4 lakini haina Hospitali ya Wilaya na wananchi wake hulazimika kutembea umbali wa takribani kilomita 30 kufuata huduma za afya Tarime na akina mama ambao ni asilimia 52 wanahitaji huduma ya hospitali kamili:-

Je, ni lini Wilaya ya Rarya itajengewa Hospitali ya Wilaya?

NAIBU SPIKA: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rarya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 105 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya 67 hapa nchini ikiwemo Hospitali ya Rarya ambayo tumeitengea shilingi bilioni 1.5.

NAIBU SPIKA: Hongereni sana TAMISEMI kwa majibu mafupi. Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, swali la nyongeza.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri na kueleza mkakati, lakini naomba niulize swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizi hospitali 67 ambazo zitajengwa, je, Wilaya ya Songea Mjini ipo? Kwa sababu kuna wakazi 300,000, Kata 21 na hakuna Hospitali ya Wilaya na kuna kituo hata kimoja tu cha afya. Je, Wilaya ya Songea Mjini ambapo Jimbo la Songea Mjini lipo itapata hizo hospitali 67?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke nilipo-*table budget speech* yangu mwaka huu tarehe 14, niliaishwa hospitali hizo ambapo kwa mara ya kwanza tunakwenda kuweka historia katika nchi yetu. Katika Mkoa wa Ruvuma tunakwenda kujenga hospitali Namtumbo, Songea DC pamoja na Nyasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi kwamba kwa Songea Mjini bado hatujatenga bajeti yake kwa sababu pale tuna Hospitali ya Mkoa. Hata hivyo, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge tumewasiliana mara kadhaa. Tulichokifanya ni nini? Hapa katikati tutafanya *resource mobilization* kusaidia watu wa Songea Mjini waweze kupata japo kituo kingine acha afya *as a backup strategy* kupunguza idadi ya wagonjwa ambao wengi wanakwenda katika hospitali ya mkoa. Kwa hiyo, tutakwenda kulifanya kazé suala hili katika kuimairisha vituo vyá afya.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wote mmepitia ile bajeti mna uhakika wilaya zenu hazimo kwenye ile *list*? Mheshimiwa Desderius Mipata, swali la nyongeza.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Hivi karibuni katika kuboresha shughuli za afya nchini, Serikali ilitoa ahadi kwamba itatoa pesa kwa

ajili ya kuboresha Kituo cha Afya cha Wampembe pamoja na kile kinachojengwa na wananchi cha Kasu. Nataka kuuliza, ni lini pesa hizi zitatolewa ili wananchi waweze kunufaika na huduma hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA

NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mipata, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumesema wazi kwamba tunajenga, tunaboresha vituo vya afya kwa mara ya kwanza 208 na tutatumia takribani shillingi billioni 156 pamoja na kuimarisha miundombinu mingine hasa ya wahasibu. Hata hivyo, naomba nikiri wazi, juzi juzi tumeweka katika ile *batch* ya mwisho ya vituo 25 na muda siyo mrefu hapa nilikuwa naongea na Mheshimiwa Nkamia kuhusu fedha hizo. Kwa hiyo, tuta-*cross checks* vizuri ili katika maeneo yote tuliyoyapa kipaumbele fedha ziweze kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini katika halmashauri ya Mheshimiwa Mbunge ambapo kulikuwa na changamoto ya ukosefu wa Hospitali ya Wilaya, katika mpango wetu wa Serikali wa kujenga hospitali 67 na wilaya yake tunakwenda kuipatia Hospitali ya Wilaya. Ni kwa imani yangu kubwa kwamba wananchi wa Nkasi kwa ujumla wake watapata huduma nzuri za afya katika maeneo yao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Changamoto za huduma za afya zilizopo Rorrya zinafanana na Jimbo la Nanyamba. Naishukuru Serikali imetupa ujenzi wa vituo vitatu na kituo kimoja cha Dijecha ujenzi umekamilika. Je, ni lini

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Serikali italeta watumishi kwa sababu kituo kile kina watumishi saba na mahitaji ya sasa ni watumishi 41?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata *concern* hii na kwa sababu tunajenga hivi vituo vya afya vipyta 208 au tunaviboresha lengo letu kubwa ni ili viweze kufanya huduma ya upasuaji, tunajua tuna mahitaji makubwa ya wataalam. Hata hivyo, takribani wiki mbili zilizopita tumeshatangaza ajira zipatazo 6,180. Lengo kubwa ni kwamba watu wale tutakapowaajiri tuwapeleke katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, imani yangu Mheshimiwa Chikota wala asihofu kwa sababu Nanyamba vilevile ni mionganini mwa eneo ambalo tunalenga kuja kujenga Hospitali ya Wilaya tunajua mahitaji yatakuwa ni makubwa zaidi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba ni mpango wa Serikali wale watumishi 6,180 tutawagawanya maeneo mbalimbali lakini hata hivyo hatutaishia hapo itabidi tuongeze watumishi wengine kwa lengo la kuwasaidia Watanzania.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo, swali la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Hospitali au Kituo cha Afya cha Sinza maarufu kama Hospitali ya Palestina ilipandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya lakini bado iko katika mazingira madogo sana yaani eneo lake ni dogo sana na hata bajeti yake inakwenda kwenye masuala ya kituo cha afya. Je, ni lini sasa Serikali itatoa bajeti ya kutosha lakini vilevile kupanua

mazingira yake ili wananchi wa Sinza na Ubungo kwa ujumla waweze kupata huduma stahiki? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la dada na mama yangu Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, anachokisema Mheshimiwa Susan ni kweli. Wiki tatu zilizopita nilikuwa katika Kituo hicho cha Palestina, nilikwenda kukagua ujenzi, hasa miundombinu. Pale kulikuwa na ukarabati unafanyika lakini ukarabati ule nilipata mashaka kama *value for money* ipo? Nimekwenda kuangalia pale na *population* niliyoikuta pale ilikuwa ni kubwa sana. Ndiyo maana mpango wa Serikali kwa Wilaya ya Ubungo, kwanza yenyewe haina Hospitali ya Wilaya. Kile Kituo cha Afya hata ukiangalia mazingira yake siyo rafiki zaidi kupandishwa kuwa hospitali ya wilaya. Ndiyo maana mwaka huu sasa katika Jiji la Dar es Salaam tunakwenda kujenga hospitali tatu kuanzia Kigamboni, Ilala maeneo ya Kivule pamoja na Ubungo lakini wenyewe wata-*decide* wapi hospitali hizo zitakwenda kujengwa. Kwa hiyo, ni jukumu letu kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimemweleza pale Mkurugenzi kwamba ukusanyaji wa mapato sikuridhika nao. Leo hii Kituo kile cha Palestina, thamani ya fedha inayokusanywa hailingani na idadi ya watu. Kwa hiyo, maana yake kuna mianya mikubwa ya upotevu wa mapato. Kwa hiyo, nilitoa maagizo, imani yangu kubwa ni kwamba eneo lile marekebisho yatafanyika kwa maslahi mapana ya wakazi wa Ubungo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Kubenea.

Kudhibiti Vyanzo vya Maji Vinavyopeleka Maji Kenya

MHE. SAED A. KUBNEA (K.n.y. MHE. JOSEPH R. SELASINI) aliuliza:-

Vipo vyanzo vya maji kutoka Mlima Kilimanjaro ambavyo vinasemekana vinapeleka maji nchini Kenya kuititia msitu wa Rongai:-

Je, Serikali haioni sababu za kudhibiti vyanzo hivyo ili kuhakikisha kwamba maji hayo yanatumika katika Halmashauri ya Rombo badala ya kwenda nchi jirani ya Kenya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Raman Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ipo miradi ya maji kwa upande wa Kenya inayotumia vyanzo vya maji vilivyopo katika msitu wa Rongai ambapo kuna mito na chemchem 14 inayopeleka maji Loitokitok nchini Kenya. Maji hayo yanachukuliwa kwa vibali vya Bonde la Mto Pangani. Kijiografia wananchi wa Loitokitok hawana sehemu nyingine jirani ambayo wangeweza kupata maji. Upelekaji wa maji Mji wa Loitokitok ni wa kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji uliofanywa na wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo umebaini kuwa maji hayo yalianza kuchukuliwa tangu miaka 1960 ambapo ipo miradi ya maji yenye vibali vya mwaka 1960, 1990, 2000 na baada

ya 2010. Baada ya ufuatiliaji huo, watumiaji wote wametakiwa kuomba vibali upya kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya 2009. Maji yanayochukuliwa ni kutoka kwenye vyanzo vidogo ambavyo haviwezi kutumika katika mji mdogo wa Tarakea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vyanzo hivi kuwa na maji kidogo, kuna uwezekano wa kuchepusha ili kuwasaidia wananchi wetu wa mpakani hasa maeneo ambapo mabomba yanapita ili kudumisha ujirani mwema wa pande zote mbili. Kwa sasa Kampuni ya *Kiliwaterambayo* ndio inayotoa huduma ya majisafi Wilayani Rombo imeomba kibali cha kuchukua maji kutoka Mto Naremuru na tayari kibali cha ujenzi kwenye chanzo hicho kimepatikana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea, swali la nyongeza.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna tatizo la maji kwa wananchi wa maeneo ya Rombo na suala hili limekuwepo tokea miaka ya 1960, ni lini Serikali itaruhusu uchepushaji wa hayo maji ili wananchi wa Rombo ambao wanapata maji kutoka Mlima Kilimanjaro kwa wingi sana waweze kutatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la Rombo linafanana kabisa na suala la Ubungo, hasa katika maeneo ya Kajima, Kimara na Makoka, je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi wa Ubungo kukamilisha mradi mkubwa wa maji ambao umetokea Kibamba hadi maeneo hayo ya Kimara? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, lakini natumia nafasi hii kutambua kwamba tuna changamoto kubwa sana katika maeneo mbalimbali kuhusu suala zima la maji. Serikali kwa kuona haja ya kutatua changamoto hii ya maji, katika Wilaya ya Rombo tumetenga kiasi cha Sh.1,530,000,000 ili kuhakikisha tunatatua tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Ubungo nilifanya ziara pamoja na Mheshimiwa Mbunge na kuna mradi mkubwa wa upanuzi ili kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. Kubwa, mimi kama Naibu Waziri pamoja na viongozi wote wa Wizara tutausimamia mradi huu ili kuhakikisha wananchi wake wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kata ya Kapalambsenga iko jirani na Ziwa Tanganyika lakini haina maji kabisa. Ni lini Serikali itatatua tatizo la kata hiyo kwa kupeleka maji kwa kuyatoa Ziwa Tanganyika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tunatambua kabisa unapokuwa karibu na waridi lazima unukie. Labda nimwombe Mheshimiwa Mbunge tukutane tushauriane na Mkurugenzi wa eneo husika, tuangalie ni kwa namna gani tunaweza tukabuni mradi katika kuhakikisha wananchi wake wa kata hiyo wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kabla ya kuuliza swali naomba uniruhusu niwape pole wananchi wa Jimbo la Buyungu kwa kupoteza Mbunge wao. Naomba wawe watulivu katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Kakonko bado lipo tatizo kubwa la upatikanaji wa maji. Katika mji huo maji hutoka mara tatu kwa wiki katika visima viwili; kimoja ni kisima cha Mbizi ambacho kinatumia pampu na cha pili ni kisima cha Kanyovi kinachotumia *solar*. Nashukuru Serikali katika bajeti hii kwa kutupangia pesa. Je, ni lini sasa mradi huo utaanza katika Mji wa Kakonko? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ya kipekee anavyowapigania wananchi wake katika suala zima la maji. Nitumie nafasi hii kulishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kutuidhinishia kiasi cha Sh.727,345,000,000 yote hii katika kuhakikisha tunaenda kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya bajeti hii kuu kuitishwa sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali.

Na. 354

Hitaji la Maji Safi na Salama – Manyoni

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE aliuliza:-

Uhaba wa maji safi na salama imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Manyoni na Mkoa wa Singida:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha miradi mikubwa ya maji ambayo itahudumia wananchi wa maeneo hayo muda wote?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maji kuititia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu jumla ya miradi minne ya Solya, Kilimatinde, Londoni na Majiri imekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji. Katika awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni inatekeleza miradi ya Mangoli, Itetema, Kasanii, Kintinku, Maweni, Makuru, Nyaranga, Makutupora, Sanza/Ntope, Makanda, Igwamadete, Heka, Chikombo na Mazuchi ambayo ipo katika hatua za utafutaji wa vyanzo na kufanya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mradi mkubwa wa Mbwasa ambaao umeshafanyiwa usanifu na utaanza kutekelezwa katika mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kuhudumia vijiji vya Mbwasa, Mwiboo, Chikuyu, Mtiwe, Chilejeho, Mvumi, Ngaiti, Kintinku na Lusilile.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.3 na Serikali itahakikisha miradi hiyo inatekelezwa na inakamilika mapema na kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa maeneo hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aisharose Matembe, swal la nyongeza.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la kwanza, kwa kuwa kero ya maji katika Mkoa wa Singida ni ya muda mrefu na hii ni kutokana na jiografia yake ya hali ya ukame. Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba mabwawa katika Mkoa wa Singida ili kupunguza makali ya kero hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, kwa kuwa upatikanaji wa maji katika vijiji 13 vya Jimbo la Manyoni Mashariki vikiwemo Mangoli, Ikasi, Magasi, Winamila na Ipenduka imekuwa ni kero kubwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba visima katika vijiji hivyo ili kuwawezesha wananchi kupata maji safi na salama na kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Aisharose, amekuwa ni mpiganaji na amekuwa ni mfuatiliaji wa mara kwa mara katika Wizara yetu ya Maji katika kuhakikisha wananchi wake wa Mkoa wa Singida wanapata maji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua eneo la Singida ni kame, Wizara yetu imekuwa ikishirikiana na wadau

mbalimbali katika kuchimba visima virefu na hata mabwawa katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wanasema unapotembea na kuzuru wengine naomba usinipite, hatutampita katika kuhakikisha wananchi wa Singida wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii lake la pili, Serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya maji kuitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji lakini mpaka sasa miradi 1,469 imekamilika kati ya miradi 1,810. Mkakati wetu wa Wizara ni katika kuhakikisha tunatekeleza miradi 387. Nimhakikishie dada yangu katika miradi hiyo sisi kama Wizara ya Maji tutampa ushirikiano mkubwa sana katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji katika vijiji alivyoviorodhesha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri kashasema hatawapita anapopita, sasa naona mmesimama bado. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, swalii la nyongeza.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali maji ya Benki ya Dunia, viko vijiji ambavyo vilikuwepo kwenye mpango kikiwemo kijiji cha Nakapanya, Majimaji, Muwesi na Mchoteka. Vijiji hivi viliwekwa kwenye mpango na ilionyesha kwamba pesa yake ipo lakini majibu ya Serikali walisema kwamba vyanzo havijapatikana. Nini sasa kauli ya Serikali katika kuendelea kufanya utafiti ili wananchi wale wafaidike na huo mradi? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana lakini nampongeze Mheshimiwa Mbunge, siyo mara yake ya kwanza kuulizia kuhusu suala zima la maji. Kama fedha zipo, namwombwa sana Mhandisi wa Maji wa eneo hilo afanye kazi. Unapokuwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhandisi wa Maji, jukumu lako ni katika kuhakikisha wananchi wanapata maji. Sisi kama Wizara ya Maji tuko tayari hata kutoa watalaam wetu katika kuhakikisha wanatafuta vyanzo vya maji ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mradi wa maji wa Bukindo, Kagunguli Visiwani Ukerewe unatekelezwa kwa ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na kusimamia na *MWAUWASA*. Mradi ule kwa sehemu kubwa umekamilika lakini haujaanza kutoa huduma kwa sababu ya kukosa pesa za kuunganisha umeme. Je, Serikali iko tayari kuwasiliana na *MWAUWASA* ili waweze kusaidia uunganishaji umeme mradi huo uweze kutoa huduma uweze kuwasaldia wananchi wa Kata za Bukindo, Kagunguli na Mtungulu ambao watafaidika na mradi huu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji tupo tayari kufanya mawasiliano na Mkurugenzi wa *MWAUWASA* na ikatakapobidi tufanye jambo hili la haraka ili wananchi wake waweze kupata umeme ili mradi uweze kutekelezeka na wananchi waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Bulembo, swali la nyongeza.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mji wa Bukoba una maji mengi kutohana na Serikali kufanya vizuri, lini Wilaya ya Misenyi itapata maji kutoka kwenye chanzo cha Bukoba Mjini kwa sababu hawana uwezo wa kutumia yale maji yote?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nampongeza mzee wangu Mheshimiwa Bulembo. Moja, nimhakikishie maeneo ambayo sijawahi kufika ni Bukoba, baada ya Bunge hili nitafika Bukoba tunaangalie hali halisi na namna gani tunaweza tukashauriana kuweza kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji, kama nilivyoeleza, Bunge lako Tukufu limetuidhinishia bajeti yetu Sh.727,345,000,00, yote hii ni katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Sisi Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kikubwa Waheshimiwa Wabunge, tunaomba ushirikiano wa dhati katika kusimamia na kufuatilia miradi hii ya maji ambayo tunatekeleza katika maeneo yao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KEISSY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Lini mradi wa maji ambaeo ulipatikana kwa njia ya ujisadi katika Kijiji cha Kamwanda, Kirando utaanza? Maana yake wananchi mpaka sasa wanasubiri, siyo kosa lao, wanateseka siyo kosa lao, wananyanyaswa siyo kosa lao. Lini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Serikali katika kuhakikisha inatatua tatizo la maji na imekuwa ikipeleka fedha nydingi maeneo mbalimbali, lakini kumekuwa na ubabaishaji na wakati mwingine hata baadhi ya wakandarasi kufisadi fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara katika Jimbo la Mheshimiwa Keissy tukagundua ufujaji fedha zile,

tukahakikisha kwamba *TAKUKURU* wanachukua hatua. Sasa hivi kuna hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa na vyombo hivi vya dola. Namwomba nimweleze Mheshimiwa Keissy, katika kipindi hiki sisi kama Wizara ya Maji tutahakikisha wananchi hawa wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza wakati Serikali ikiendelea na suala zima la kuwashikilia wale watu ambao wanawatuhumu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Constatine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swalii lake.

Na. 355

**Ujenzi wa Reli ya Isaka - Keza Kuelekea
Burundi na Rwanda**

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU aliuliza:-

Moja ya sababu zinazochelawesha kuanza kwa Mgodi wa Kabanga Nickel ni umeme na reli:-

Je, ni lini reli ya Isaka – Keza kuelekea Burundi na Rwanda itajengwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Constatine Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia ushirikiano baina ya nchi za Afrika Mashariki inatambua umuhimu wa ujenzi wa reli ya Isaka – Keza kuelekea Burundi na Rwanda,

siyo kwa sababu tu ya kuanza kwa mgodi wa Kabanga *Nickel*, bali pia kuchochea kasi ya usafirishaji wa mizigo na shughuli za kibiasara na hivyo kuinua uchumi wa nchi yetu na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inatambua kuwa kila nchi ina wajibu wa kutekeleza mradi wa kujenga reli hii kwa sehemu yake. Hivyo, ni wajibu wa kila nchi kukamilisha mradi huo ili kuchochea maendeleo yanayotokana na ujenzi wa reli hiyo kwa kukidhi mahitaji makubwa ya ubebaji mizigo kwenda nchi jirani za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*). Aidha, hali hii itasaidia pia usafirishaji wa wananchi kwenda mikoani na nchi hizo za jirani kwa wingi na kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania, tayari imeshaanza kujenga kwa kipande cha kuanzia Dar es Salaam – Morogoro kilometra 202 na Morogoro – Makutupora kilometra 336, ikipitia Makutupora – Tabora kilometra 294, Tabora – Isaka kilometra 133 na Isaka – Mwanza kilometra 254 ikikamilika kwa urefu wa kilometra 1,219; na sehemu nyingine ni kutoka Tabora hadi Kigoma kupitia Mpanda – Kalemela – Tabora na Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujenga reli kutoka Isaka kupitia Kabanga hadi Rusumo na kuingia Kigali nchini Rwanda, Serikali inakamilisha maandalizi ya kujenga reli hiyo. Mkatuba wa usanifu na matayarisho ya zabuni umesainiwa mwezi huu wa Mei, 2018 na Kazi itaanza mwezi Juni, 2018 na zabuni itatangazwa ndani ya mwaka huu wa 2018.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu, swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Swali la kwanza, kiuchumi kukamilika kwa reli hii kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma itakuwa hakuna tija kama kipande cha kutoka Dodoma kwenda Mwanza na kutoka Dodoma kwenda Mpanda na Kigoma kitakuwa hajjakamilika. Tumeshuhudia uwekaji wa

saini mikataba hapa karibuni kwa vipande hivi viwili. Sasa ni lini mikataba hii ya kipande kinachoanzia hapa kwenda Mwanza, Kigoma na Mpanda itasainiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, moja ya sababu ya bidhaa za viwandani kuwa bei kubwa sana katika Mikoa ya Geita na Kagera ni kwa kuwa usafirishaji katika maeneo haya unategemea barabara. Kwa kuwa kipande cha Isaka kwenda Kigali kitakamilika, ni upi mpango wa Serikali kujenga reli ya kutoka kwenye chanzo chochote kwenda Geita na Kagera?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imeshaanza ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro na Morogoro mpaka Makutupora. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari taratibu za kuanza mchakato wa ujenzi wa kipande cha kutoka Makutupora mpaka Tabora umeshaanza. Tayari upembizi yakinifu umekamilika na usanifu wa kina tayari umekamilika, tunatafuta pesa kama Serikali kwa ajili ya kuanza mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, tunao mpango wa kujenga kipande cha Geita – Lusahunga mpaka Uganda na taratibu zitakapokamilika, Mheshimiwa Mbunge atataarifiwa kama inavyopaswa. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali ina mpango gani wa kiuchumi wa kuimarisha barabara za vijijini katika mikoa ambayo hajapitiwa na lami ili kwenda sambamba kiuwiano kiuchumi tunapokwenda kwenye Serikali ya viwanda na uchumi wa kati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la ndugu yangu Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara za vijijini kikawaida unaratibiwa na *TARURA*. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaendelea na michakato, lakini mapendekezo ya ujenzi wa barabara zote za vijijini kama nilivyozungumza huwa unaanzia kwenye Mabaraza ya Madiwani, inakwenda kwenye *RCC* kisha kama Wizara tunapatiwa. Kama linatuhusu Wizara ya Ujenzi, tunalishughulikia kama ipasavyo lakini kama inahusu *TARURA*, basi wenzetu wa Wizara ya TAMISEMI nao wanashughulikia kama inavyopaswa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

Na. 356

**Hitaji la Mawasiliano katika Baadhi ya Kata
za Mufindi Kaskazini**

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD (K.n.y. MHE.
MAHMOUD H. MGIMWA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano katika Kata za Mpanda, Mpangatuzara, Ihanu na Ikweha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa huduma ya mawasiliano nchini, Serikali kwa kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, uliyaainisha maeneo ya Kata za Mapanda na Ikweha na kuyaingiza katika zabuni ya awamu ya pili 'A' kwa ajili ya kuwekewa huduma za mawasiliano. Kata hizo mbili zilipata mzabuni wa kufikisha huduma ambaye ni *Vodacom*. Kazi ya kufikisha huduma ya mawasiliano ilishakamilika ambapo vijiji vya Ugenza, Ukelemi na Uyela katika Kata ya Ikweha vinapata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baadhi ya maeneo ya Kata hiyo hususan Kijiji cha Ikweha hakina mawasiliano. Kwa upande wa Kata ya Mapanda, huduma inapatikana katika baadhi ya maeneo ya Kata hii lakini mengi ya Vijiji vya Mapanda, Chogo, Ukami, Uhafiwa na Ihimbo havina huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itayaainisha maeneo ya Kata za Ihanu zenye Vijiji vya Isipi, Lulanda, Ibwanzi na Kilosa; Kata ya Mpanga yenye Vijiji vya Mpanga, Tazara; Kata ya Ikweha, Kijiji cha Ikweha; na Kata ya Mapanda yenye Vijiji vya Mapanda, Chogo, Ukami, Uhafiwa na Ihimbo na kuyaingiza katika miradi ya mfuko ambayo itakayoteklezwa siku za usoni kwa kadri ya upatikanaji wa fedha hususani kuanzia mwaka huu wa fedha 2018/2019.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, swalii la nyongeza. (*Makof*)

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yenye kutia moyo lakin naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kuna minara imejengwa katika Kata ya Mapanda, Kijiji cha Mapanda na Kata ya Ikweha Kijiji cha Ikweha, lakin mpaka nauliza swali hili hakuna mawasiliano na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa ameonana na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano. Je, ni lini watapata mawasiliano katika kata hizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Bunge hili yuko tayari kwenda katika Kata ya Mapanda, Ikweha, Mpangatazara, Ihanu kujionea mwenyewe matatizo ya mawasiliano yanayowapata wananchi wa maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khadija, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba kuna baadhi ya minara ambayo imewekwa lakini haijaanza kutoa mawasiliano kutohana na sababu mbalimbali. Sababu ya kwanza inaweza ikawa kutokuwepo umeme eneo hilo na wakategemea kutumia *solar* ambapo kama kunatokea hali ya mawingu, basi zile *solar* haziwezei kupeleka umeme wa kutosha kwenye minara na hivyo kusababisha wananchi kutoqua na mawasiliano. Sababu nytingine ni za kijigrafia. Hivyo, nawaelekeza Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote watembelee eneo alilolitaja Mbunge kuhakikisha kwamba wanatambua chanzo cha sababu ya minara hiyo kuwepo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Iakini haitoi mawasiliano. Nami nitafutilia kuhakikisha kwamba minara yote ambayo imewekwa na haina mawasiliano basi inaanza kupeleka mawaliano kwa wananchi kwa kuwa ndiyo lengo kuu la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, niko tayari baada ya Bunge hili na nimeshaahidi hata Wabunge wengine kwamba nitafanya ziara ya miezi miwili na timu yangu ya watu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuhakikisha tunatambua maeneo yote ambayo hayana mawasiliano tuweze kuyapatia mawasiliano. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mendrad Kigola, swali la nyongeza. (*Makof*)

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Wilaya ya Mufindi tuna tatizo kubwa sana la mawasiliano na Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ni kutokana na jioagrafia ilivyo. Vijiji vya Idete, Kasanga, Ihwanza, ni sehemu kubwa sana hawana mawasiliano kabisa na amesema kwamba atakuja na timu yake, je, yuko tayari sasa timu hiyo iende ikafanye *survey* kwenye vijiji hivi ili wananchi wale waweze kupewa mawasiliano?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kigola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, niko tayari kwenda naye kuangalia maeneo hayo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, swali la nyongeza.

MHE MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Serengeti, Kata za Ikoma hususani ndani ya hifadhi maeneo ya Robo, Kata za Sedeko, Nyansurura na Nyambureti, hakuna mawaliano ya simu. Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu kupeleka minara katika maeneo hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba njibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe maelezo kwa ujumla tu kwamba tunayo changamoto kwenye maeneo ambayo yanapakana na Hifadhi ya Taifa na tuko kwenye mawasiliano mazuri sana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yako kwenye hifadhi tunaweka minara kwa mapatano maalum. Tunapata changamoto kwa sababu wanaohudumia ile minara hatuwezi kuwa na *control* nao ya moja kwa moja. Tunajipanga kuhakikisha kwamba tunakuwa na *control/nao* ya moja kwa moja ili hata mnara unapowekwa kwenye hifadhi, basi usalama wa hifadhi zetu unaendelea kuzingatiwa lakini wakati huo huo wananchi wanapata huduma ya mawasiliano bila kukwamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mulugo, swali la nyongeza.

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya mpya ya Songwe maeneo ya Rukwa, Udinde, Guwa na Some hayana kabisa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akanihakikishia ni lini Serikali itaweka mawasiiano katika kata hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la ndugu yangu Mheshimiwa Mulugo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Mulugo kwa jinsi ambavyo anapambana kwa ajili ya Jimbo lake na wananchi wa eneo lake. Nashukuru vilevile kwa kuwa ameshanilettea barua ya maombi ya kuimarisha masuala ya mawasiliano kwenye maeneo aliyoyataja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mulugo kwamba tutafanya ziara baada ya Bunge hili kuhakikisha maeneo yake na maeneo mengine yote ambako Waheshimiwa Wabunge wameandika barua kuomba mawasiliano tunayatembelea na kuhakikisha tunaingiza kwenye bajeti ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ambao tutaanza kuutekeleza kuanzia mwezi Septemba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge wengi kweli inavyoonekana hawana mawasiliano katika maeneo yao.

Mheshimiwa Cosato Chumi, nadhani Mheshimiwa Waziri amesema atakuja Mufindi, kwa hiyo, atapita na Mafinga. Ahsante sana.

Mheshimiwa Jerome Bwabahusi, swali fupi.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kata ya Mchauru, Kata ya Sindano na maeneo ya Njawara na Ntona yako mpakani mwa Tanzania na Msumbiji na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulithibitisha kwamba pembezoni au kwenye mipaka ya nchi yetu watahakikisha minara inajengwa. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atahakikisha kwamba wananchi wale wanapatiwa mawasiliano? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mhweshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Bwanausi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Bwanausi kwamba kati ya Waheshimiwa Wabunge walioleta barua zao mwanzoni kabisa kuhusu masuala ya mawasiliano alikuwa ni yeye. Namshukuru Mungu vilevile kwamba tumeendelea kupokea barua kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wanaoeleza changamoto ya mawasiliano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Bwanausi na wananchi wa Jimbo lake kwamba tutafanya ziara pale, tutaainisha maeneo ambayo tunaweza tukaweka minara kwa sababu siyo lazima ukiomba minara mitano uwekewe mitano. Unaweza ukaomba minara mitano, ukawekewa miili na ikaweza ku-cover eneo kubwa sana; lakini unaweza ukaomba minara mitatu ukawekewa hata mitano kutokana na jiografia. Ndiyo maana naeleza kwamba ni lazima twende tukajiridhishe tukiwa na timu ya wataalam kuhakikisha kwamba tunaweka mawasiliano ambayo yatahakikisha yanawafaidisha wananchi kwa ujumla wao.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya mipakani vilevile kuna programu maalum ambapo tunashirikiana Mfuko wa Mawasiliano na *TCRA* kuhakikisha mawasiliano yanayohusu Watanzania yanabaki kuwa ya Watanzania na yanayohusu nchi nyingine yanaendelea kuwahuusu wao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Ally Saleh.

Na. 357

**Wahitimu Waliomaliza Chuo cha Taifa
cha Utalii Mwaka 2016/2017**

MHE. ALLY SALEH ALLY (K.n.y. MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN) aliuliza:-

Je, Chuo cha Utalii kimetoa wahitimu wangapi wa fani za hoteli za kitalii kwa mwaka 2016/2017?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa maliasili na utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Taifa cha Utalii ni Wakala uliopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii wenye dhamana ya kutoa mafunzo ya ukarimu na utalii nchini. Aidha, chuo kinatoa ushauri wa kitaalam na kufanya utafiti katika fani ya ukarimu na utalii. Chuo cha Taifa cha Utalii kina ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundji (*NACTE*) ili kutoa mafunzo ya ukarimu, usafiri na utalii kwa ngazi za stashahada na astashahada.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa masomo 2016/2017 kupitia kampasi zake tatu za Bustani, Temeke Dar es Salaam na Sakina Arusha, kilitoa mafunzo ya ukarimu, usafiri na utalii kwa wahitimu 329 kama ifuatavyo:-

- (i) Stashahada ya Usafiri na Utalii (*Ordinary Diploma ni Travel and Tourism*) wahitimu 43;
- (ii) Stashahada ya Ukarimu (*Ordinary Diploma in Hospitality Operations*) wahitimu 15;
- (iii) Astashahada ya Ukarimu (*Technician Certificate in Hospitality Operations*) wahitimu 78;
- (iv) Mafunzo ya Muda Mfupi (*Short Courses in Food Production and Pastry and Bakery*) wahitimu 78; na
- (v) Mafunzo ya Uhitaji Maalum (*Tailor Made Courses in Hospitality and Tourism*) wahitimu 79.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo hayo yamekuwa yakinolewa kwa kutumia mitaala inayofuata Mfumo wa Kujenga Ujuzi na Maarifa (*Competence Based Education and Training*) inayosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundis (NACTE).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh, swali la nyongeza.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali la kwanza, Tanzania tunalenga kujiondoa kwa watalii 1,300,000 kwa mwaka na pia kujiondoa kwenye mchango wa utalii katika pato la Taifa kwa asilimia 17.5 na pia kufikia ajira milioni mbili zinazotokana moja kwa moja na utalii. Je, Serikali haioni kiwango cha diploma na *certificate* ni kidogo kwa sasa na kwamba tuende kwenye *degree*? Ni lini Serikali inajipanga kuongeza hadhi chuo hicho kiwe na uwezo wa kutoa *degree*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, injini ya kutawala sekta ya utalii ni elimu na ujuzi katika eneo la menejimenti. Je, ni lini Serikali inapanga kuwezesha Chuo hicho cha Utalii kutoa *course* ya juu ya menejimenti ili kuondoa wageni kutawala sekta hii katika eneo la menejimenti? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Saleh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba mpaka sasa hivi tumekuwa tukitoa stashahada na astashahada lakini hivi sasa Serikali ina mpango wa kuanzisha *degree* katika maeneo hayo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Columbia kutoka Canada. Baada ya kukamilika mitaala na ikishapitishwa, basi tutaanza kutoa hizo *degree* ambazo zitawaandaaa vijana wetu katika hizo fani ambazo Mheshimiwa Mbunge ameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kuhusu masuala ya mafunzo ya menejimenti, ni kweli kabisa tumekuwa na changamoto kubwa katika mafunzo na *course* zinazotolewa kwa ajili ya menejimenti kuwaandaa vijana kuweza kushika nyadhifa mbalimbali katika hoteli zetu na katika maeneo mbalimbali. Hivi sasa Wizara kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 tunategemea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watu mbalimbali, ambayo yatahusu watu zaidi ya 800 katika maeneo ya menejimenti ili kuwaandaa na kuweza kushika nyadhifa mbalimbali na nafasi katika utumishi katika maeneo ya utalii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwamoto, swalii la nyongeza.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Najua nia ya Serikali

ya kuanzisha vyuo hivi ni pamoja na kukuza utalii na kuingiza pato la letu la ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tembo wametoka kwenye Hifadhi ya *Udzungwa National Park* wameshambulia katika Vijiji vya Mailindi, Maghana kwenye Kata ya Mahenge, wananchi wako kwenye hali mbaya na jambo hili limekuwa likijitokeza kila mwaka. Naomba tu Mheshimiwa Waziri aende akaone hali jinsi ilivyo lakini pia ahakikishe kwamba kituo kidogo cha askari wa wanyamapori kinafunguliwa pale. Tatizo hili ni la kila mwaka, namwomba sana Mheshimiwa Waziri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Balozi Venance Mwamboto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwamoto, amekuwa akifuatilia sana hili suala na tumekuwa tukizungumza ni hatua gani ambazo tunaweza kuzichukua. Naomba nimhakikishie kwamba nitakuwa tayari kwenda kuangalia hali halisi katika Kata hiyo ya Mahenge ili kuona ni hatua gani zichukuliwe na Serikali. Moja ya hatua ambazo tunategema kuzichukua ni pamoja na kujenga *out post* katika lile eneo ili wasaidiane na wananchi na Halmashauri ile katika kudhibiti hao tembo ambao wamekuwa wakizagaa katika maeneo mbalimbali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Parezzo, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wabeba mizigo kwenye milima yetu ambao wanatembeza Wazungu wamekuwa hawapewi mafunzo na wanafanya kazi hii kwa uzoefu Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanapatiwa mafunzo haya lakini na maslahi yao kwa ujumla yanatazamwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresto ambalo kwa kweli anataka kujua kwamba ni mpango gani tulionao katika kutoa mafunzo kwa hawa wanaobeba mizigo. Naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejiandaa vya kutosha katika mwaka huu wa fedha unaoanza Julai mwaka 2018, tunategemea kutoa mafunzo mafupi kwa hao watu wote pamoja na wale wanaongoza utalii katika eneo la Mlima Kilimanjaro ili kusudi waweze kutoa zile huduma ambayo wateja wetu wanazitarajia. Kwa hiyo, awe na subira, baada ya mwaka kuanza ataona matunda na mabadiliko makubwa yatakayojitokeza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 358

Kupotea kwa Uoto wa Asili Lushoto

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Wilaya ya Lushoto imezungukwa na misitu lakini misitu mingi imeungua kwa moto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha uoto ule wa asili uliopotea kutohana na misitu kuungua?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, misitu iliyoungua moto katika kipindi cha kuanzia Agosti, 2016 hadi Februari, 2017 ni mitano ambayo ina jumla ya hekta 357.05 kati ya misitu 11 ambayo ina jumla ya hekta 22,855. Misitu hiyo ni Msitu wa Hifadhi Asilia Magamba wenyewe jumla ya hekta 9,381, zilizoungua ni hekta 338; Msitu wa Mkussu wenyewe hekta 3,674, zilizoungua ni hekta 3.8; Msitu wa Shagayu wenyewe hekta 7,830, zilizoungua ni hekta 2.75; Msitu wa Baga I wenyewe hekta 3,572, zilizoungua ni hekta 12; na Msitu wa Ndelemai wenyewe hekta 1,421, zilizoungua ni hekta 10.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, misitu ya asili iliyoungua au kuharibowi inaweza kurejeshwa kwa namna mbili. Mosi, kupanda miti maeneo yaliyoungua; na pili, kuliacha eneo liote miti lenyewe kwa kutofanya shughuli zozote za kibinadamu. Njia ya kwanza hutumika zaidi kwenye misitu ya kupandwa. Kutokana na asili ya eneo la Lushoto, njia nzuri zaidi ya kurudishia miti eneo lilloungua ni kuacha kufanya shughuli zozote za kibinadamu ili uoto wa asili urejee wenyewe. Aidha, kupanda miti isiyo ya asili ndani ya misitu ya hifadhi unaharibu uasilia wa msitu na huenda ukaleta matokeo hasi katika uoto wa asili uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Wakala wa huduma za Misitu Tanzania unaendelea kutoa Elimu kwa jamii ili wananchi wanaoishi jirani na misitu ya hifadhi wawe makini wanapotumia moto wakati wa kusafisha mashamba yao, kwani chanzo kikuu cha moto wote uliounguza misitu katika kipindi hiki umetokana na wananchi kutayarisha mashamba yao bila kuchukua hatua za tahadhari.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimsahihishe Naibu Waziri, amesema Misitu wa Mkussu; siyo Mkusu ni Mkuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa misitu ya Wilaya ya Lushoto iliyoungua tokea mwaka 2004 ni takribani miaka 14 sasa, lakini mpaka sasa hivi miti ile ya asili hajaota, imebaki vichaka tu. Je, nini *commitment* ya Serikali juu ya kurudisha haraka uoto wa asili uliopotea kwa kupanda miti katika maeneo ya misitu iliyoungua pamoja na sehemu za maporoko? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ina vijana wengi wamejingga kwenye vikundi, je, Serikali ipo tayari kuwapa miche ya miti ya asili bure ili kurudisha haraka uoto wa asili uliopotea kwa muda mrefu sasa? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MALI ASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shabaani Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukue nafasi hii kumpongeza sana kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia sekta ya misitu na kwa jinsi ambavyo amekuwa akitoa ushauri kwa namna mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, eneo lolote lile ambalo ni misitu ya asili, ukienda kuanza kupanda miti mingine utaharibu ule uoto wa asili. Tunachofanya sisi ni kuliacha lile eneo kama lilivyo. Tukishaliacha kama lilivyo, ikifika kipindi ile miti itaota yenewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kabisa kwamba katika lile eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge anasema imechukua muda mrefu haijaota, lakini hivi sasa Wakala wa Taifa wa Misitu Tanzania wanafanya utafiti ili wapate mbegu na miche bora ile ya asili iliyokuwepo katika lile eneo ili tuone kama tunaweza tukaipanda katika eneo lile kusudi kurudisha ule uoto wa asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu miche hii ya asili ambayo inaweza ikapandwa katika eneo hili na wale vijana waweze kupata ajira, kama nilivyosema Wakala wa Taifa wa Misitu anafanya utafiti. Tukishakamilisha, tukabaini mbegu au miche mizuri ya asili katika eneo lile, basi tutaenda kuhakikisha kwamba inapandwa katika lile eneo na wale vijana watapata ajira.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali letu la mwisho. Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 359

Faida ya Kuwa na Urithi wa Dunia.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH aliuliza:-

Kilwa ni moja ya miji mikongwe katika Afrika Mashariki tangu Anno Domino (AD) 900 -1700 pamoja na miji mingine ya Lamu, Mombasa, Sofala na Zanzibar. Miji hiyo ilipewa heshima ya jina la Urithi wa Dunia (*World Heritage Site*). Kwa kawaida miji hiyo husaidiwa na Mataifa mbalimbali ikiwemo Marekani, Japan, Ujeruman, Uingereza na Shirika la UNESCO:-

Je, Serikali ya Tanzania imefaidika nini kutoka katika Mataifa hayo yanayosaidia nchi za urithi wa dunia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara yaliorodheshwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia mwaka 1981. Mwaka 2004 eneo la hifadhi la visiwa hivi liliingizwa kwenye orodha ya maeneo yenye urithi ulio hatarini kutoweka (*Endangered Site*). Hatua hiyo ilisababishwa na hali yake ya uhifadhi kutokidhi kiwango cha Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi, Elimu na Utamaduni (*UNESCO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005, Wizara kwa kushirikiana na *UNESCO* na nchi za Ufaransa, Norway, Japan na Marekani iliandaa miradi ya kukarabati magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na mafunzo. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Euro 600,000 kutoka Serikali ya Ufaransa; Mradi wa Dola za Kimarekani 201,390 kutoka Norway; mradi wa Dola 119,000 kutoka Ufaransa na *UNESCO*; mradi wa Dola 66,000 kutoka *ILO*; mradi wa Dola 100,000 kutoka *World Monuments Fund*; mradi wa Dola 700,000 kutoka Ubalozi wa Marekani; na mradi wa Dola 43,900 kutoka *UNESCO*. Kukamilika kwa ukarabati kuliwezesha magofu hayo kuondolewa kwenye orodha ya urithi uliokuwa hatarini kutoweka mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine zilizopatikana ni pamoja na ushauri wa kitalaam na misaada ya vifaa mbalimbali; kuendelezwa kwa miundombinu katika maeneo husika na ongezeko la kipato kwa jamii husika kupitia biashara ya utalii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah, swali la nyongeza.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH. Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu haya ya Serikali. Swali la

kwanza, maeneo haya ni yale ambayo walikaa wakoloni wa mataifa haya makubwa ambayo leo hii wanasaidia. Je, Serikali imesaidia kwa namna gani katika kuendeleza miundombinu ya Kilwa Kisiwani na Msongo Mnara ili kuendeleza utalii wa maeneo haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili la nyongeza, napenda kujua Serikali inasaidiae katika kuhakikisha Kilwa Kisiwani na Msongo Mnara tunaendeleza utalii, maana hali ya kule ni mbaya sana, miundombinu ni mibovu, watalii sasa wanapungua kwa sababu hakuna hoteli, hakuna vifaa vya kuwawezesha watalii kuvuka kwenda Kilwa Kisiwani na Kilwa Msongo kuona haya magofu ya ukoloni? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hamida Abdallah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kutambua mchango wake ambao amekuwa akiutoa katika hii sekta ya utalii kule Lindi. Kwa kweli amekuwa akifanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika lile eneo mimi mwenyewe nimefika Machi na nimeona jinsi miundombinu ambavyo iko kwenye hali mbaya. Hiyo inasababisha watalii wengi washindwe kufika katika lile eneo. Hivi sasa tumeandaa mkakati maalum kwa ajili ya kuboresha ile miundombinu katika vile Visiwa vya Kilwa pamoja na Songo Mnara ili kuhakikisha ile miundombinu inapitika wakati wowote; iwe ni kipindi cha masika au kipindi cha kiangazi, kusudi watalii waweze kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa ambayo iko pale ni pamoja na kutafuta boti ya kisasa itakayokuwa inawavusha watalii kuwapeleka kule katika

Kisiwa. Sasa hili tunashirikiana na Wizara ya Uchukuzi ili tuone namna ambavyo tunaweza tukapata boti nzuri ya kuweza kusaidia katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu namna ya kuimarisha utalii katika eneo lile, mpango mkubwa ambao tunao kama Wizara ni pamoja na kuunganisha na Pori la Akiba la Selous. Tunataka iwe ni *circuit* moja, watalii wanapokwenda kutembelea Selous katika upande ule, basi tuunganishe na hii *circuit* ya Kilwa Kisiwani pamoja na Songo Mnara kusudi vyote kwa pamoja iwe *package* moja. Hiyo tunaamini itasaidia sana katika kuimarisha utalii katika lile eneo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Allan Kiula, swali la nyongeza.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa sababu yapo maeneo mengine ambayo yanaweza na yenyewe kuwa ni urithi wa dunia, kama vile magofu ya Mjerumani ya Mkalama. Wizara inafanya juhudini gani kuyaweka katika orodha hiyo na kuona namna ya kuyaboresha? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Allan Kiula, Mbunge wa Mkalama, rafiki na kaka yangu ambaye tunalingana urefu, hongera sana. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kabisa katika maeneo yale kuna magofu yaliyoachwa na Mjerumani. Katika utaratibu ambao Wizara sasa imeamua kuchukua, tumeamua kuangalia mali kale zote zilizopo na kuziboresha. Ili tuweze kuziboresha, hatua ambazo tumechukua, tumeamua kushirikisha hizi taasisi zilizo chini ya Wizara zenye uwezo kidogo wa kifedha na kuwakabidhi hayo maeneo ili waweze kutengeneza miundombinu mizuri iweze kusaidia

katika kuboresha na kuyatangaza na kuvutia watalii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada hizi, nina imani kabisa yale maeneo ya magofu yatapata ufadhilli mzuri sana na hivyo yataimarika vizuri sana na kuweza kuvutia watalii.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, nitaleta kwenu matangazo yaliyotufikia hapa mezani.

Tunaanza na wageni. Kundu la kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika na hapo kuna Mgeni wa Naibu Spika ambaye ni Chifu Allan Mwaigaga Ndenjela. Huyu ni Mjumbe wa Kamati ya Uchumi na Fedha wa CCM Mkoani Mbeya. Karibu sana Dodoma Chifu wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Wabunge; tutanza na wagemi 15 wa Mheshimiwa Selemani Jafo, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambaao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Kisarawe Mkoani Pwani, wakiongozwa na Ndugu Hiyana Mlawa. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Capt. George Mkuchika ambaye ni Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ambaao ni walimu na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha St. Johns cha hapa Jijini Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Doto Biteko, Naibu Waziri wa Madini, ambaao ni rafiki zake kutoka Jijini Mwanza. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, hawa ni wapiga kura wake kutoka Mbozi, Mkoani Songwe. Karibuni sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Vilevile tunao wageni sita wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu amba ni wachimbaji wadogo kutoka Mgusu, Mkoani Geita. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Janet Mbene amba ni wataalamu kutoka Taasisi ya *Institution for Inclusive Development* ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Sachin Gupta. Karibu sana. (*Makofi*)

Wengine ni wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo amba ni wafanyakazi wa *Shanta Goldmine* pamoja na *Tankol Energy* kutoka Mkoa wa Songwe na Ruvuma wakiongozwa na Ndugu Honest Mrema. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa George Lubeleje amba ni Wajumbe wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) kutoka Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Ritta Kabati amba ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni Sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Fatma Toufiq amba ni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji UWT Mkoa kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dodoma, Ndugu Neema Majule. Karibuni sana akina mama. Ni viongozi wa akina mama hawa kutoka Mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Vilevile tunao wageni wanne wa Mheshimwa Fredy Mwakibete amba ni Walimu wa Shule ya Msingi Mpata kutoka Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya. Karibuni sana jamani, naamini huko Busokelo hawajambo ndugu zetu. (*Makofi*)

Wengine ni wageni walotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 63 kutoka Chuo Kikuu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

cha St. John's cha hapa Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Ngusi Yeriko. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wetu wote tunawakaribisha sana Dodoma, tunaamini kwamba mtajifunza mawili matatu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia kwamba kutakuwa na hafla ya uwasilishwaji wa taarifa za Kamati Maalum alizoziunda Mheshimiwa Spika kuhusu Sekta ya Uvumi wa Bahari Kuu na Gesi Asilia, kesho Jumamosi tarehe 2 Juni, 2018.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika atapokea na kukabidhi Serikalini taarifa za Kamati Maalum za ushauri alizoziunda kuhusu Sekta ya Uvumi wa Bahari Kuu na Gesi Asilia. Hafla hiyo itaanza saa 3.30 asubuhi katika viwanja vya Bunge mbele ya lango kuu la kuingilia ukumbi wa Bunge. Wote mnaalikwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tunaendelea.

MWONGOZO WA SPIKA

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmesimama kwa miongozo lakini leo nitatoa miongozo miwili Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Ndassa. Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nasimama kwa kanuni ya 68(7) lakini naisoma pamoja na Kanuni ya 49, ikikupendeza tupate kauli la Serikali juu ya jambo ambalo nimelisikia likizungumzwa na upande wa pili wa nchi yetu upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa nafuatilia matangazo ya moja kwa moja ya Baraza la Wawakilishi la

Zanzibar na walikuwa wanajadili suala la bajeti ya Wizara ya Maliasili, Kilimo na Uvuvi ya Zanzibar kama sijakosea. Nikasikia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanalamika kwamba Serikali ya Zanzibar inaingia gharama ya kuzuia meli ya uvuvi ambayo imekamatwa Mtwara. Kuna meli ilikuwa inavua kimakosa imekamatwa Mtwara, kwa hiyo, walichokuwa wanakilalamikia Wawakilishi ni kwamba Serikali ya Zanzibar inaingia gharama kubwa kui-*Maintain* ile meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua kama ingekuwa Mheshimiwa Waziri yupo labda ikikupendeza tupate *statement* ya Serikali, kama kuna meli ya uvuvi ilikuwa inavua imekamatwa na tunayo *experience* ya namna hii, basi tungeweza kujua kwamba imekamatwa na ina muda gani na inatumia gharama gani kuwa imezuiwa pale, tukijua kwamba suala la uvuvi wa Bahari Kuu umekuwa na shida na tuna historia ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nipate mwongozo wako kama tungeweza kupata taarifa ya Serikali juu ya jambo hili kwamba ni kitu gani kinaendelea na hiyo meli imezuiwa na kwa nini sasa Serikali ya Zanzibar ndiyo iwe ina-*incur* gharama hizo za kui-*Maintain*.

NAIBU SPIKA: Umeshaeleweka Mheshimiwa. Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 47 na 48(2)(a) kuhusu jambo mahsus.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi Naibu Waziri wa Fedha amewasilisha randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha. Juzi niliomba Bunge lako lipate taarifa kuhusu kinachoendelea hivi sasa na jana kimenitokea mimi mwenyewe kuhusu hizi mashine za kielektroniki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ambazo zipo ni kwamba mashine hizi sasa ni zaidi ya miezi mitatu hazifanyi

kazi inavyotakiwa. Jambo hili limesababisha mapato ya Serikali kuanzia Machi, Aprili na Mei kushuka. Jambo hili tunaweza tukaona kwamba ni dogo lakini ni kubwa kweli kweli, kwa sababu mashine zile tunazitegemea ili kusudi zikusanye mapato ya Serikali, tupate uhalisia wa mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ukweli kuhusu tatizo hili. Tatizo hasa ni nini? Ni lini Wizara ya Fedha italeta taarifa kuhusu kuharibika kwa mashine hizi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijajibu miongozo hiyo miwili, kuna wageni sita wa Mheshimiwa Allan Kiula ambaao ni viongozi wa CCM kutoka Mkalama Singida. Karibuni sana viongozi wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Richard Ndassa. Mwongozo wa Mheshimiwa Bobali anasema, jana amefuatilia majadiliano katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakizungumza kuhusu meli iliyokamatwa na kwamba wanaingia gharama kubwa.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena, Kanuni yetu ya 68(7) inataka usimame kwa Kanuni ile ikiwa unataka mwongozo wa Kiti juu ya jambo lilitotokea hapa ndani, je, linaruhusiwa au haliruhusiwi? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mnapoomba miongozo mingine huwa mnatupa wakati mgumu sana kila wakati kurudia hii Kanuni. Kama kila Mbunge zile nakala mlizogawiwa angekaa nazo awe anasoma hii Kanuni kabla hajasimama kuzungumza, ili tunapolileta jambo ambalo halihusiani na Kanuni hii, tutumie Kanuni zinazohusika. Mheshimiwa Mbunge anayetaka Kauli ya Serikali, hawezni kutumia Kanuni ya 68(7), Kauli ya Serikali tumia Kanuni zinazohusika na ziko nydingi, sio moja tu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mwongozo wa Kiti kama ulivyoombwa na Mheshimiwa Bobali, ni kwamba

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

jambo hilo halijatokea hapa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mtolea, tafadhali. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Ndassa, naye ametumia Kanuni hiyo ya 68(7) kuhusu jambo ambalo alishaliuliza hapa Bungeni na Mheshimiwa Naibu Waziri alipata nafasi ya kutoa maelezo. Wakati huo Kanuni hii ya 68(7) inataka jambo liliotokea hapa Bungeni. Kwa hiyo, hili jambo kwa sababu halijatokea hapa Bungeni, hatutaweza kutumia Kanuni ya 68(7) na kwa hivyo hakutakuwa na mwongozo juu ya jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, lakini Naibu Waziri yuko pale na kwa sababu bajeti yao inakuja, naamini watakuja na majibu ya msingi kabisa kwa sababu juzi ulipoulliza, ulilingia kwa Kanuni ya Jambo la Dharura na Mheshimiwa Naibu Waziri, Kanuni zinasema jambo la dharura linajadaliwa ikiwa hilo jambo haliji katika siku za usoni. Kwa sababu linakuja siku za usoni, naamini mtakapokuja na bajeti yenu mtatoa majibu mahsus ikuhusu jambo hili la *EFD* kwa sababu Serikali inakosa mapato.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu

NDUGU PAMELA PALANJO – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali
kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Madini**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nimeshaletewa orodha na vyama vyenye uwakilishi hapa Bungeni kuhusu Waheshimiwa Wabunge watakokuwa wakichangia siku ya leo kwenye hoja ili yopo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Madini. Tutaanza na Mheshimiwa

Victor Kilasile Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Saed Kubenea ajiandae.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja yetu ambayo iko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wote wawili na Watendaji wote Wizarani kwa kazi kubwa wanayofanya kwenye sekta hii ya madini iweze kuchangia maendeleo ya Watanzania. Mnachapa kazi kweli kweli, nimeona mnafika kila mahali, hata kwangu Chunya mmeefika na huko mnatimiza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako nisome sehemu moja kwenye Kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 22, anasema, "Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia GST na STAMICO chini ya mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali madini, ilikamilisha utafiti wa kina wa kijiosayansi uliohusisha uchorongaji na ukadiriaji wa mbale katika maeneo ya wachimbaji wadogo kwenye maeneo sita ya ujenzi wa vituo vya umahiri vya Katente huko Bukombe, Itumbi Chunya kwangu, Kona - Tanga, Kapanda – Mpanda, Buhemba – Musoma na Kyerwa. Vituo hivyo vitatumika kwa ajili ya mafunzo ya uongezaji thamani madini na uchimbaji salama pamoja na kuongeza uzalishaji, tija na hivyo kuongeza mapato kwa wachimbaji wadogo." (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Wizara kwa jambo hili. Naomba kwenye kituo changu na vituo vingine vyote ambavyo mmevisema, mkivijenga na kuvianzisha, muweke mitambo ya kukodisha wachimbaji wadogo wadogo. Kwa sababu sehemu kama Chunya kwangu Wilaya nzima ni mwamba, dhahabu iko chini ya mwamba. Kwa

hiyo, wachimbaji wadogo wadogo wanashindwa kupata vifaa vya kuweza kuchoronga hiyo miamba na kuweza kufikia dhahabu. Kwa hiyo, naomba kwenye vituo hivi muweke mitambo yote ya kuweza kukodisha ili wachimbaji wadogo waweze kupata huduma hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwamba kwenye kituo changu cha Itumbi ambako anaweka hii *Center of Excellence* wapeleke umeme kwenye awamu hii ya tatu ya REA. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati apeleke umeme kwenye kituo hiki cha Itumbi ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kunufaika na kituo hiki ambacho mnawachimbia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuishukuru Serikali na Wizara, wamenijengea mtambo wa kuchakata na kuvunja miamba na mawe kwenye Kituo cha Matundasi ili kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo. Naishukuru sana Serikali, naomba mwendeleze mpango huu kwa sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya nzima ya Chunya, hata kwenye nyumba ya Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ni leseni za utafutaji. Wilaya nzima ya Chunya imejaa leseni za utafutaji ambapo wenyе leseni hizo wako Dar es Salaam, siyo wachimbaji wadogo wadogo wa Chunya. Leseni yake ikiisha kwa mujibu wa sheria, huyu mtu anakwenda Wizarani kama anarudisha nusu, lakini hairudishi, anaomba kwa kutumia kampuni nyingine ya mtoto wake au ya mjomba wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara kwa huu moto mlionza nao, kupitia Tume ya Madini, mpitie upya leseni zote katika Wilaya ya Chunya. Kuna watu ambao wana leseni ya utafutaji kutoka mwaka 2007/2008 mpaka leo anayo yeye mwenyewe, wakati sheria inasema ikifika miaka minne

hujapata chochote, unarudisha nusu kwa Kamishna wa Madini, unabaki na nusu, hawajafanya hivyo. Naiomba sana Wizara ipitie upya kupitia Tume ya Madini ili leseni hizi zirudishwe wapate wachimbaji wadogo wadogo waweze kujiongezea kipato. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili lifanyike kwa sababu kuanzia Chunya Mjini kwenda Makongolosi, Malangamilo kwenda Ngwala mpaka Mbikatoto, maeneo yote hayo ni leseni za utafutaji na waliokamata leseni hizo ni wajanja ambao wako Dar es Salaam (*speculators*), wana-speculate kwamba atapata lini. Naomba sana Serikali ilishughulikie suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alikuja Chunya nawe ulikuwepo, nashukuru sana kwa ziara ile. Mlitembelea kampuni fulani ya uchimbaji ambayo mliona inatii sheria, hata hii Sheria mpya ya Madini ya 2017 kampuni hiyo inatii. Hiyo kampuni ikaomba iwemo kwenye mchakato wa kujenga *smelter* nchini. Naomba sana Wizara hii ya Madini iifikirie kampuni hiyo ambayo iko Chunya ili *smelter*ya kuweza kuchakata makinikia ijengwe Chunya ili yasiende nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee pia ruzuku kwa wachimbaji wadogo wadogo. Wizara imeanza na ni jambo jema sana. Kwangu Chunya mmetoa kwa wachimbaji wawili, watatu, naomba Wizara iendelee kutoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo zaidi ili waweze kuinua kipato cha nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea na Mheshimiwa Ester Mahawe, ajiandae.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri nikaufahamisha umma kuwa mimi pia ni mmoja kati ya wachimbaji wadogo wa madini. Kwa sura hiyo, naona kabisa kwamba eneo hili likiendelea kutulea wachimbaji, mchango wetu kwa nchi hii utakuwa mkubwa. Mara ya mwisho niliwahi kuzungumza hapa, uzuri wa wachimbaji wadogo, fedha wanayopata hawaendi kuwekeza nje, wanakwenda kuwekeza ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, tukiwaendeleza wachimbaji wadogo kwa ujumla wake, maana yake tunakwenda kuboresha maendeleo ya miji yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa Johannesburg imejengwa kwa fedha ya pale pale. Kwa hiyo, naamini iwe ni Mwanza, Shinyanya, Chunya na Mpanda nakotoka, wachimbaji hawa wadogo wana nafasi kubwa ya kuleta maendeleo katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiona kazi nzuri ya *GST* kwa maana ya suala zima la utafiti. Nina eneo moja la Kapanda pale kwangu ambapo kwa maana ya kitabu hiki inaelezea wakia 47,605 ziliweza kubainika pale Kapanda. Rai yangu, pamoja na tafiti hizo nzuri zinazofanywa na ndugu zetu wa *GST*, eneo lile la Kapanda wameshaelekeza kwamba kitajengwa kituo kwa ajili ya kuendelea kuwasaidia wachimbaji, siiioni kasi ya kufanya zoezi hilo. Kwa hiyo, naomba pamoja na tafiti hizo nzuri ambazo amezifanya, basi ile kasi ya kwenda kujenga kituo pale isomeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nami nizungumzie suala la leseni. Nafahamu utoaji wa leseni hapa katikati tulikuwa tunasubiria Tume. Nashukuru kwamba Tume imepatikana na kuna watendaji mahiri katika Tume hiyo basi

nilichokuwa naomba tu-speed up suala la utoaji leseni. Niseme hivi, utoaji wa leseni ni chanzo kingine cha mapato. Kwa hiyo, tunapochelewa kutoa hizo leseni, pia tunachelewa katika suala la mapato. Tutakapokuwa tukitoa leseni hizo tuiswasahau wachimbaji wa eneo la Kapanda, Dilifu na kwa ujumla wake, maeneo yale ya Mpanda ambapo Serikali iliahidi kuwasaidia wachimbaji hawa wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona suala la migodi ya *STAMICO* pale ambapo inakuwa haifanyi vizuri, basi Serikali ione namna ya kuweza kuwapatia wachimbaji wa katii. Hilo nalo nami naendelea kuishauri Serikali, kama *STAMICO* itakuwa imeshindwa kufanya vizuri, basi mwone nafasi hiyo ya kuweza kuwapatia wachimbaji wa katii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa *smelter*, nafahamu na hapa katika ukurasa wa 38 na 39 inaelezea. Kwa mfano, ukija maeneo ya Mpanda kwa maana tu ya *tailings*, hapa Kiswahili cha *tailings* wanasema visusu, ukija katika suala la *tailings* tu pale maeneo ya Mpanda kuna visusu vya kutosha katika eneo lile, tatizo lake ni teknolojia sahihi ya jinsi ya kuitoa dhahabu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua jiolojia ya Mkoa wa Katavi ni tofauti na ilivyo Mwanza na Chunya, kwa hiyo, kila watu wachukuliwe kwa namna yake. Ndiyo maana leo unaweza ukakuta mchimbaji wa Mpanda pamoja na kuwa na visusu vya kutosha lakini hana uwezo wa kuipata ile dhahabu kwa sababu ya *lack of technology*. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ituangalie kwa jicho hilo la huruma watu wa kanda ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kwa maana ya mwamba wa eneo lile, kuna madini mengi tu. Kwa wakati mmoja anaweza akapata dhahabu, *copper*, fedha na mambo mengine mengi. Kwa hiyo, sasa namna ya ku-

separate, it is an issue. Kwa hiyo, naomba sana hilo nalo liweze kuangaliwa kwa sura hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana naendelea kusisitiza, najua kwa maana ya thamani iongezewe hapa nchini, ujenzi wa *smelter* ni jambo la msingi, ingawa nafahamu uwezekano wa kujenga *smelterinaweza* isifanyike kwa usiku mmoja, ni suala la hatua. Kwa hiyo, wakati tukijipanga kwenda huko, tuendelee kuangalia tunafanyaje na wale ambao tayari wanaendelea na uchimbaji katika sura hiyo nyingine? Najua Mheshimiwa Waziri na Watendaji kwa ujumla wenu na Serikali yangu kwa ujumla wake kwa usikivu huu mtaliangalia suala hilo kwa jicho la pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ruzuku pia, kwa maana ya wachimbaji hawa tunapozungumzia kuwawezesha ni pamoja na kuwapatia ruzuku. Kama kulikuwa na upungufu huko nyuma, naomba tuzitoe zile tofauti lakini tusiache kutoa ruzuku kwa watu hawa. Ni kwa kufanya hivyo tutaongeza mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, najua kuna suala la *local content*, kwa maana ya kuhakikisha wazawa wananaufaika na suala zima la uchimbaji. Mimi naliangalia kwenye sura hii, tutakapojenga uwezo wa wachimbaji wadogo, fedha ambazo watapata watu hawa, mzunguko wake unarudi palepale. Mtu huyu kama akienda sokoni atanunua *materials* ambazo ni za hapa hapa nyumbani, atampeleka mtoto shule na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama unamzungumzia mama lishe, fedha ikitoka mgodini itakuja huku, itamkuta mama lishe, fedha ikitoka mgodini ikija huku itamkuta mchuuzi mwingine sokoni. Kwa hiyo, kwa sura hiyo tunauona mtiririko wote wa suala la fedha kwa watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la ujenzi wa Ofisi ya Kanda ile ya kule kwetu Mpanda. Mpaka leo suala hili la ujenzi wa ofisi sioni dalili. Kwa hiyo, naomba sana na Mheshimiwa Waziri wangu anasikia pale, sisi ni Kanda ya Magharibi, utashangaa Makao Makuu ya Kanda hata ofisi haipo. Kwa hiyo, naomba sana lile zoezi la ujenzi wa ofisi liendelezwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika maeneo tofauti tofauti upelekaji wa fedha katika Wizara inarudishwa kwa kiwango kidogo. Tutaipataje tija kama watu hawa hawapewi fedha za maendeleo? Naomba sana kwa ujumla wake kama ni Wizara ya Fedha tuendelee kuwaangalia watu hawa. Watu ambaao wanachangia kwenye pato la Taifa unaposhindwa kuwarudishia fedha maana yake unakuwa umewakata miguu, hawataweza tena kutoka hapo walipo ili kuongeza mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Saed Kubenea, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Mahawe na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-wataala* kwa kutujalia kufika siku ya leo na kutoa mchango wetu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nimpe pole Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, wananchi wa Buyungu, wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na familia ya Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Bilago kwa kuondokewa na mpendwa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini humu ndani kuna tatizo kubwa la *STAMICO* (Shirika letu la Madini la Taifa). *STAMICO* haina mtaji, imekabidhiwa jukumu kubwa sana la kusimamia madini katika nchi hii lakini Serikali haijawahi kuipa *STAMICO* mtaji wa kutosha wa kufanya shughuli zake. Matokeo yake nchi imekuwa kichaka cha watu kupora madini yetu kwa sababu hatujaijengea uwezo mkubwa *STAMICO* wa kusimamia rasilimali zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika hili la umma ambalo ndio lilikuwa linatarajiwa kubeba dhamana kwa makampuni yote yanayokuja kuwekeza kwenye madini kwenye nchi hii, angalau shirika hili liwe ndio shirika kiongozi, lakini limetupwa na limeachwa yatima. Jambo ambalo limesababisha sasa kuzaliwa kwa makampuni mengi feki na kuchukua rasilimali za nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ilianzisha Kampuni inaitwa Meremeta ambayo siku za nyuma aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayaza Pinda aliliambia Bunge mwaka 2008 kwamba Kampuni hii ni ya Usalama wa Taifa na Kampuni hii inamiliikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, akakataa kutoa taarifa ya Kampuni ndani ya Bunge hili. Kampuni ya Meremeta ilithibitika kwamba asilimia 50 ya wanahisa wake ni watu kutoka nje na kwa hiyo kwa vyovyote vile haiwezi ikawa Kampuni ya Jeshi la Wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi lilishajiondoa tokea mwaka 2002 baada ya Kampuni ya Meremeta kurudishwa Hazina kwa Msajili wa Hazina. Hadi kufikia Juni, 2008 kampuni ya Meremeta lilikuwa na Dola za Marekani zaidi milioni 80 katika akaunti yake iliyofunguliwa Benki ya *NBC* kule Musoma, karibu zaidi ya bilioni 200. Fedha ambazo ni za walipa kodi wa nchi hii na hazijulikani zilivyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa makampuni ya nje kujilingiza katika biashara ya ndani bila kuisaidia *STAMICO* kusimamia miradi ya madini nchini hatutaweza

kufika popote. Kila mwaka tutakuwa tunaibiwa, kila mwaka tutakuwa tunapiga kelele lakini njia pekee ya kusaidia Taifa hili ni kuimarisha *STAMICO*. Njia pekee ya kuondoka hapa tulipo ni kuimarisha *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wageni wanakuja hapa wanachimba madini yetu wanaondoka, wanaacha mashimo, wanaacha uharibifu wa mazingira hakuna mtu nyuma anayeweza kusimamia. Kama *STAMICO* ingekuwa ndiyo shirika letu umma, linamiliki zaidi ya asilimia 50 ya hisa kwa makampuni ambayo yanakuja kuchimba, maana yake kwamba jukumu hili angekabidhiwa *STAMICO*. Leo ukienda kule Nzega kuna kampuni imechimba madini imeondoka imeacha mashimo, imeacha uharibifu wa mazingira, wananchi wanateseka, leo mzigo unabebwa na Serikali na kampuni haikulipa kodimeondoka, mambo kama haya nchi hii haiwezi kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma ripoti ya Kamati, kuna mgodi mmoja uko Mara umetajwa humu, Jeshi la Wananchi limezuia ile kampuni iliyopewa kazi ya kuchimba madini isifike kwenye mgodi. Mimi nilipongeze Jeshi kwa hatua hiyo, nchi yetu Jeshi letu limetumiwa kama kichaka cha watu kuja kuchukua fedha zetu. Kwa hiyo, ni lazima uchunguzi ufanyike kama Jeshi limefunga mkataba na kampuni fulani, huo mkataba uonekane, maslahi ya Taifa letu yaangaliwe kwanza kabla ya kitu chochote kile. Tusije tukatumia Jeshi tukaonekana tunaficha baadhi ya vitu kutumia Jeshi ili vitu hivyo viweze kuondoka kiurahisi kwa sababu Bunge hili au Wabunge hawa hawana mamlaka ya kuingilia mambo ya ndani ya Jeshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kwamba katika kitabu kizima cha Waziri na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, hakuna mahala popote palipozungumzwa makinikia kwa ufasaha wake. Tulitegemea Bunge letu lipewe taarifa ya kina ya mzungumzo yanayoendelea kati ya Serikali na makampuni ya Accacia na mengine ambayo yaliambiwa na *TRA*

hayakulipa kodi ya zaidi ya shilingi triliioni 424. Dola za Marekani bilioni 190 ambazo tuliambiwa nchi hii ingepata kutokana na makinikia, bajeti nzima ya Serikali iliyokuja haizungumzii mahali popote jambo hilo na katika ripoti ya Waziri hakuna mahali popote ambapo amezungumzia jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mmoja wa Wajumbe au Mwenyekiti wa hiyo Kamati yumo humu ndani Profesa Kabudi atuambie makinikia yamefikia wapi. Mchanga ambao ulizuiwa bandari umeondoka? Kama bado upo, upo mpaka lini? Je, leo migodi inasafirisha mchanga kwenda nje ya nchi? Kiwanda cha kuchakachua ule mchanga kinajengwa lini ili Watanzania ambao walikuwa na matumaini ya kupata elimu bure, kila Mtanzania aendeshe Noah yake mwenyewe kwa fedha hizi, kila Mtanzania apate matibabu bure kwa fedha hizi, kila Mtanzania aweze kuishi maisha mazuri kama ambavyo nchi nyingine zinaishi kwa fedha hizi, fedha hizi shilingi triliioni 424 zinapatikana lini? Bajeti ambayo ni zaidi ya miaka 10 ya bajeti ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni muhimu sana tukaelezwa Watanzania makinikia yako wapi. Mazungumzo yamefikia wapi, fedha hizi zinapatikana lini ili sisi tupate kuwaambia wapiga kura wetu kwamba kila Wilaya, kila Kata itapata Kituo cha Afya kwa sababu kuna shilingi triliioni 424 bajeti ya miaka 10 ijayo ya Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi ni nyingi sana na kama tumeibiwa kwa kiasi hiki ni lazima Serikali ijiangalie vizuri. Mimi niwashauri njia pekee tusipige danadana, tuimarishe Shirika la Taifa la Madini (*STAMICO*), tulipe mtaji...

*(Hapa kengele illilia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Mahawe atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mheshimiwa Martha Mlata ajiandae.

MHE. ESTHER A. MAHAWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kutoa mawazo yangu katika bajeti hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba huwezi kuanza kuzungumza habari ya madini na rasilimali za nchi hii pasipo kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufulsi kwa nia yake ya dhati ya kulinda maliasili ya Taifa hili yakiwemo madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yake ya dhati imepelekea kujengwa kwa ukuta katika Mji wa Mererani Mkoani Manyara ambako ndiko nakotokeea mimi. Nia hii ya dhati imepelekea Jeshi letu la Ulinzi kulinda ukuta ule, nimeona watu wanabeza ulinzi wa Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumza suala zima la uzalendo, uzalendo huo unapatikana jeshini kwa asilimia 100. Isingwezekana tuweke ukuta wa gharama kiasi kile halafu tuweke walinzi wa Jadi. Kwa hiyo, mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ujenzi wa ukuta ule na hatimaye kuweka Jeshi letu kulinda maliasili zilizoko pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba bado tunahitaji *CCTV Camera* kwa ajili ya kudhibiti upotevu ama utoroshwaji wa madini kwa namna nyingine, maana eneo lenyewe ni kubwa ni kilometra zaidi ya 24. Kwa hiyo, niombe tu Serikali iendelee na nia yake ya dhati kabisa ya kudhibiti upotevu wa madini, siyo tu madini ya tanzanite yaliyoko Mererani lakini maeneo mengine yote ambako madini ya namna mbalimbali kama dhahabu na madini mengine yanakopatikana ili madini haya yaweze kusaidia uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe pongezi za dhati kwa Mawaziri wa Wizara hii nikianza na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Hawa watu wanafanya kazi, tunawaona muda mwingu wapo *field* na kazi yao inaonekana kusema ule ukweli. Kazi yao imepelekea sasa kuongezeka kwa mapato haya kupitia mauzo ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirudi katika eneo la Mererani ongezeko la pesa ambayo iili kuwepo kabla ya 2017/2018 tumeiona, ongezeko limekuwa kubwa madini haya sasa yanawafaidisha wananchi wa Manyara pamoja na Tanzania kwa ujumla. Niseme hongera kwa Rais, hongera kwa Serikali kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kupongeza Bunge lako Tukufu ambalo iili fanyia marekebisho Sheria ya Madini ya mwaka 2017 na Kanuni zake saba zilizoundwa kwa ajili ya kuhakikisha malengo ya kulinda na kudhibiti rasilimali hii ya madini yanatimia. Mwaka jana tulipitisha hapa Sheria mbili za *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty)na The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms)*, kisa ni kwamba lazima tuhakikishe madini haya yanawanufaisha Watanzania ambao ni wazawa na ndiyo wenye uchungu na madini haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la EPZA pale Mererani. Naomba Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba EPZA wanawavutia wawekezaji ili lile eneo pale liweze kutumika. Tuna eneo kubwa tu ambalo lina *almost* hekari 1,311 ambalo ni kwa ajili ya uwekezaji. Tunaomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Madini pamoja na EPZA waweze kujenga eneo lile ili kuweza kuwavutia wawekezaji ili madini yale yachakatwe, yauzwe mahali pale na ajira na mapato yaweze kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ajira katika sekta ya madini. Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa mwaka 2012 tulikuwa na ajira kati 500,000 mpaka 1,500,000. Nataka

tu kufahamu ni takribani miaka sita sasa tangu tafiti hizo zimefanyika, maana kwenye kitabu hiki sijaona ajira hizo zimeongezeka ama zimepungua kwa kiwango gani kwa mwaka huu 2017/2018. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia dira na dhima ya Wizara hii ya Madini ni kuhakikisha pia wanabuni na kusimamia sera, mikakati na mipango ya kuendeleza sekta ya madini; kusimamia migodi na kuhamasisha shughuli za uchimbaji pamoja na utafutaji wa madini; kuratibu na kusimamia uongezaji wa thamani ya madini kwenye biashara ya madini; kukuza ushiriki wa wazawa yaani *local content* kwenye shughuli za utafutaji; kusimamia na kuratibu shughuli za maendeleo ya wachimbaji wadogo; na kusimamia taasisi na mamlaka zilizoko chini ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dhima ya Wizara hii inajieleza, tuna wachimba wadogowadogo nchi hii. Eneo la Mererani tuna wachimbaji wadogowadogo wanaitwa Apolo, niombe Serikali iweze kusaidia kuwapa elimu ya kijiolojia kwamba madini haya yanapatikana wapi zaidi, ukiacha eneo tu la Mererani lakini pia wapatiwe elimu ya namna ya uchimbaji na ruzuku ili waweze kusaidia familia zao na kuongeza mapato kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma kulikuwa kuna pesa wanapewa wachimbaji wadogowadogo kama ruzuku. Nishauri kwa kuwa zile fedha wakati mwingine utakuta walikuwa wanagawana nusu kwa nusu na hawa waliokuwa wanawapatia hizo fedha zikawa haziwanufaishi kihivyo, wapewe vifaa vya uchimbaji. Hivyo vifaa vya uchimbaji vinaweza vikawasaidia wachimbaji hawa wadogowadogo na kuwainua na hatimaye kuwa wachimbaji wa kati na wakubwa ambao wataongeza thamani ya kazi wanayoifanya na hatimaye kuongeza mapato. Kwa hiyo, niombe sana watu hawa wapatiwe mafunzo ya kutosha ya kiteknolojia ili na wao waweze kuchimba kisasa zaidi kuliko kuchimba kwa njia ambazo ni za kizamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya *smelter* yamesemwa na Wabunge wenzangu na mimi nichangie hilo. Ni muhimu kupata *smeltersasa* kwa sababu katika uchimbaji kwa mfano wa dhahabu ama *tanzanite* kuna madini mengi madogomadogo ambayo yangeweza kuongeza thamani ya madini yetu yanapotea kwa sababu *smelter* hii ilikuwa inatumika nje ya nchi. Niweze kuiomba Serikali na kuiombea Serikali yangu iweze kufanikisha suala la uwekaji wa *smelter* hapa nchini ili tuweze kufaidika na madini yale mengine yanayopatikana baada ya kuchenjuliwa kwa yale madini makubwa kama dhahabu na *tanzanite*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wachimbaji wadogowadogo ambaao ni wanawake, ni nini mkakati wa Serikali katika kuhamasisha na kusaidia kuwapatia wanawake wachimbaji elimu ya kutosha illi na wao waweze kuongezeka kimapato na hata uwezo. Maeneo mengi yanayozunguka madini haya, wanawake kazi yao imekuwa ni kupika ama kufanya biashara ya mama ntilie. Ifike sasa mwanamke pia ainuliwe katika suala zima la uchimbaji wa madini. Wapo wanawake kadhaa tunawafahamu ambaao kwa kweli wameweza kufanya hizi kazi, wamesomesha watoto wao, wamejenga nyumba zao na kusaidia ongezeko la mapato katika Serikali yetu. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie kwa macho mawili suala zima la kumuongezea mwanamke uwezo wa uchimbaji wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado madini haya hayajatangazwa vilivyo duniani ya kwamba yanatokea Tanzania na katika kijiji kidogo hicho ama maeneo madogo haya ya Simanjiro. Niliwahi kusafiri kwenda Marekani mwaka 2011 nikatembelea Taasisi moja inaitwa *Tanzanite Liquidation Channel* iko Austin pale Texas pale Marekani. Taasisi ile nilipofika pale ilikuwa imeajiri Wamarekani 400 wanaofaidi kuititia *tanzanite* inayotoka Mererani lakini karibu kabisa na maeneo ambako *tanzanite* hiyo inatoka, ukifika ukizungukia zile shule zilizoko maeneo yale, mfano shule moja inaitwa Imishie hawana...

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Mahawe kengele mbili zimeshagonga.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Naomba niseme mambo machache kwenye Wizara hili ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina madini mengi sana na pengine Tanzania ingekuwa Korea ya Kusini ingekuwa ni nchi tajiri sana. Nahisi kuna kitu ambacho kama nchi hatujakiona. Tunapambana kuwekeza kwenye vitu ambavyo havina faida, tunaacha kuwekeza kwenye madini ambayo nchi kama Tanzania tungkuwa ni miongoni mwa nchi tajiri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kona ya nchi kuna madini, leo nikimuliza Mheshimiwa Waziri ana-enroll wanafunzi wangapi wanaoenda kusomea madini? Chuo cha Madini kipo hapa Dodoma kina-enroll/wanafunzi 70 kwa mwaka kwa ajili ya diploma, mpo hapa Mawaziri watatu kina-enroll/wanafunzi 70. Kwa hiyo, hatujawekeza vyakutosha kwenye madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kwamba nchi hili kama kuna sehemu tunaweza tukawekeza na tukatoka haraka ni kwenye madini na tuanze na elimu, Watanzania wengi hawajui madini. Hata humu ukiuliza Wabunge wengi dhahabu inafanananje inawezekana physically hawajawahi kuona dhahabu ikoje. Wanaona tu

kwenye mikufu labda na kwenye Siwa hapo lakini yenyewe kama yenyewe hawajawahi kuiona lakini dhahabu iko kila kona. Kwa hiyo, niiombe Wizara hebu wekeni fedha za kutosha kwenye elimu inayohusu madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nchi kama Afrika ya Kusini imeendelea sana kwa sababu waliokuwa wanachimba dhahabu Afrika ya Kusini, wale Makaburi ni wa palepale. Faida yote waliyokuwa wanaipata walikuwa hawapeleki Uingereza walikuwa wanawekeza Afrika ya Kusini. Sisi kama Taifa tumewasaidiaje wazawa kumiliki migodi mikubwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wachimbaji wadogowadogo ukiangalia namna wanavyochimba yaani ni aibu. Kama Taifa tunahangaika kwenda kuwekeza *billions of money* kwenye *bombardier*, lakini fedha hizo tungepeleka tukawasaidia wachimbaji wadogowadogo wakawa na migodi mikubwa, wakawa kama Acacia, wakawa kama GGM, Taifa tungeondokana na umaskini tulionao. Kwa hiyo, namtaka Mheshimiwa Waziri anapokuja kujibu, hebu watusaidie kama Serikali wanawasaidiaje wachimbaji wadogo ili waweze kufikia kiwango cha kuwa wachimbaji wenye migodi mikubwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo pia nataka mje mnipe majibu. Tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani imevuruga soko la madini hususan *gemstone*. Wale mnaofahamu pale Arusha wanunuzi wakubwa walikuwa wanakuja kununuua *gemstone* pale Arusha, baada ya hii purukushani ya Serikali ya Awamu ya Tano wamekimbilia Nairobi. Sasa hivi wachimbaji wadogo wanavyochimba hizi *gemstone* wanaenda kuuza Nairobi, kama Taifa tunakosa mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akija atuambie wana mpango au mkakati gani kwa sababu tangu mlivyoingia madarakani mwaka wa kwanza 2016 mpaka leo soko la *gemstone* halieleweki, soko la madini halieleweki?

Leo *gemstone* za kwetu zinawanufaisha watu wa Kenya, kama Taifa hatulioni hili? Ni miaka mingapi mmesema mnaandaa soko la pamoja pale Arusha ili wanunuzi wanunue hapo, utekelezaji mpaka lini au mpaka Yesu arudi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nipate majibu, tuliambiwa kwamba tunaibiwa sana na ikaundwa Tume ikakuta kwamba tumeibiwa shilingi trilioni 424, hivi ziko wapi? Baadaye nikaona wale Wazungu wamekuja, tukaambiwa eeh, tutawapa shilingi bilioni 700, ziko wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu haya makinkia, Mungu anajua hata kama mkijifanya hamjui, mimi najua haya makinkia ndiyo yalisababisha Mheshimiwa Tundu Lissu kupigwa risasi. Watu walijaa jazba wakasema Mheshimiwa Tundu Lissu ni kibaraka cha Wazungu, kesho yake tunaona Wazungu hao hao mmekaa nao Ikulu. Sasa nataka mtuambie hizi fedha mlisema tunaibiwa na mkatoka kwenye vyombo vyaa habari pale, ziko wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetengeneza sheria ni kweli na ni sahihi kulinda rasilimali zetu za madini, lakini mmekwishakaa na haya makampuni makubwa ya uchimbaji wa madini tuliyonayo hapa Tanzania mkasikia changamoto zao? Mmeshakaa nao? Maana huko pembedi ukipitia wako hapo, mimi nimejaribu kupita nawasikilizia, wanalia, wanalamika, sasa kwa nini msikae nao? Kaeni nao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nikuombe Mheshimiwa Waziri hawa watu wenye haya makampuni na pengine wana chama chao, waje watupe elimu nasi angalau tujue. Hivi unadhani Wabunge wanajua nini hapa, wengi hawajui, sehemu kubwa ya sisi Wabunge hatujui haya mambo ya madini. Kwa hiyo, ni vizuri mkatafuta hata semina kwa Wabunge wote wakajua kuhusu mambo ya madini, lakini mkikaa ninyi wenyewe, tunatunga Sheria ya Madini, madini yenyewe hatuyajui, utatungaje sheria hata hujui unachokitunga? Unatunga Sheria ya Madini, madini yenyewe huyajui, utaratibu wa kuchimba madini huujui. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri mkawa-*empower Wabunge* ili wawe na elimu wajue undani kuhusu haya madini, ili wanavyotunga sheria wanajua wanachotunga. Bila hivyo watatunga sheria ya kukomoa, mwisho wa siku utadhani unawakomoa hawa Wazungu kumbe unawakomoa na Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ryoba Chacha.

Waheshimiwa Wabunge, maonesho ya madini yako pale nyuma, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao hatujawahi kuyaona madini tuyapitie pale nje ili tusije tukawa tunaulizia mikufu ya akina mama. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Martha Mlata naona yeze amebeba madini kifuani leo. (*Kicheko*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyoniona haya ndio madini yetu tunayoenda kuyajadili leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango katika Wizara hii ya Madini ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwanza kabisa kwa kuona umuhimu wa Wizara hii na kuitenganisha kutoka kwenye nishati ikabaki kama Wizara ya Madini. Aliona umuhimu na kweli Wizara hii ina mambo mengi makubwa ambayo yanastahili kuwa na Wizara peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kwa kuweza kumteuwa Waziri, mdogo wangu Mheshimiwa Angella Kairuki kwa sababu nina imani naye. Kwanza ni mwanasheria, lakini ni mzalendo. Wizara hii inatakiwa mtu mzalendo kama

alivyo Waziri, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Doto Biteko shemeji yangu na mwanangu Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Naamini kabisa mtaitendea haki Wizara hii ili tuweze kunufaika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuonesha uzalendo namba moja. Mheshimiwa Rais kabla hajawa Rais alionesa uchungu wa namna gani nchi yetu ilivyokuwa inafilisiwa, madini yalikuwa yanapelekwa nje kwa kisingizio cha mchanga, sijui makinkia, akajitoa mhanga ili kuweza kulinusuru Taifa letu kwenye sekta hii ya madini. Nampongeza sana. Najua aligusa mahali ambapo watu hawakutegemea kuguswa. Ndiyo maana bado kuna vibaraka wanazungumza kutetea yale yaliyokuwa yakinyonya Taifa letu, namtia Mheshimiwa Rais moyo, songa mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Nabu Spika, niliwahi kusema humu ndani, ndiyo maana Mungu aliamua ajitenge mbali na sisi asionekane kwa sababu angeonekana hakika tungemsumbu. Ikiwa ni jua tutamwambia jua linawaka, ikiwa ni mvua tutasema hii mvua ya nini, ikiwa ni kimbunga tutasema kimbunga cha nini, ikiwa ni utulivu tutasema hewa hamna. Ndiyo mwanadamu alivyo, hasa wengine ambao wanaonesha tabia zao hapa ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa kujenga ukuta kwa sababu amelinda mali ambayo tumeona hata kwenye vyombo vya habari watu wanajimilikisha tanzanite ambayo siyo ya kwao. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua ya kujenga ukuta pale Mererani. Hata kama tungejenga kama Mnara wa Babeli ili mradi tunalinda mali yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze pia Tume ambayo ameiunda sasa hivi. Naomba Tume hii iliyoundwa inisikilize kwa makini, kwanza ikafanye kazi, lakini kuna sheria ambayo inasema *first come first served*. Naomba sheria hii ikaangaliwe tena kwa sababu haiwezekani

tukatumia *online* tukawa tunauza madini yetu *online*, unamuuzia mtu ambaye humjui. Mheshimiwa Waziri naomba ulisimamie jambo hili ili *GST*, kwanza nawapongeza kwa vitabu hivi ambavyo wamevitoa, wameonesha kila mkoa na madini yake kila mahali, japokuwa naamini hawajamaliza kwa sababu madini bado ni mengi. Wawezeshwe waende wakafanye utafiti ndipo tuweze kuuza vitalu hivyo baada ya kujuu ardhi hii ina mali gani. Tusiwe tunauza tu unampa mtu yeye eti ndiyo aje akwambie hapa kuna madini kiasi fulani, ndiyo maana tunaibiwa. Tuhakikishe kwamba kwanza hiki kitalu kina madini kiasi gani halafu tuweke mnada. Kwa sababu nchi nyingine wanafanya hata mnada, kwa nini tusifanye mnada wa vitalu yyetu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri badala ya kumpa mtu akatafiti mwenyewe, tutafiti wenyewe halafu ndiyo tufanye mnada. Tuende tukaone nchi nyingine walivyofanya ili tuweze kupata mapato yatakayokidhi kile kilichopo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wananchi wanaoishi kwenye eneo lile jamani, pamoja na kwamba ni mali ya Serikali, lakini wananchi wa eneo lile wafanane basi na madini hayo yaliyopo pale. Kuwe na utaratibu wa kuweza kuwasaidia waondokane na ule umaskini wafanane na madini yanayopatikana pale na huduma ziwekwe pale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri suala la *One Stop Centre*, kwani suala la *Madini House* limeishia wapi? *Madini House* siyo ofisi ya kukaa watu, ni wachimbaji wadogo wapate mahali pa kwenda kuuza madini yao na Serikali mnaweza mkanunua, mkaweka mashine ambazo zitatambua madini yaliyo halali na halisi, inaweza ikasaidia kukuza pato au shilingi yetu ikapanda. Kwa hiyo, naomba tuwe na sehemu moja ya wachimbaji wetu ili waondokane na kulaghaiwa na wale wanunuzi wadogowadogo na pia Tume iweke bei elekezi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwenye shamba kuna mabwana shamba, kuna mabwana nyuki, sijui bwana kilimo, sijui bwana samaki, kwa nini kwenye madini kusiwe na mabwana madini? Hawa wawe washauri wa wachimbaji wetu wadogo ili wao wawe ni washauri tu na watoa leseni wawe watoa leseni. Tumeshuhudia wachimbaji wadogo wanapogundua madini anamuendea mtoa leseni, badala ya kumsaidia anauza kwa mtu mwingine eneo lile lakini kukiwa na bwana madini, bwana madini atatoa ushauri tu ili afuate taratibu za kuweza kupata leseni. Mheshimiwa Waziri naomba sana mabwana madini, kama ilivyo bwana nyama, bwana shamba, bwana kilimo, bwana nyuki na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuwe na bei elekezi. Mbona kwenye kahawa kuna bei elekezi, kwenye korosho kuna bei elekezi na mazao mengine kwa nini hakuna bei elekezi kwenye madini? Kwa hiyo, naomba sana suala hili la bei elekezi nalo liangaliwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, Singida tuna madini yanaitwa zircon , Iramba, niliwahi kuuliza ile zircon imeambatana na almasi lakini wanunuzi wanununua kama zircon, wanawadhulamu wale wachimbaji. Bado naitaka *GST* wafanye utafiti watuambie hiyo ni zircon peke yake au ni pamoja na almasi na wafanyeje? Maana hata Tume ya makinikia iliwhahi kuzungumza jambo hilo. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hilo liweze kushughulikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, wachimbaji wadogo hebu na wao wawe wanaangaliwa kwa sababu wao ndiyo wanakuwa wamegundua lile eneo, lakini anakuja mtu mwingine mnawaambia kwamba hili eneo lilikuwa la utafiti, lakini aliyegundua ni mtu mwingine, matokeo yake mnakuja kutoa leseni kwa watu wengine. Naomba Waziri kwa sababu namwamini sana, naamini atasimamia jambo hilo ili wachimbaji wetu waweze kupata haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Waziri wa Madini, dada yangu Mheshimiwa Angellah na kuwateua mapacha, vijana wazuri na namwomba sana dada yangu Mheshimiwa Angellah awalee hawa vijana, najua yeye ni senior kwao na tunaona kazi wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwhali kusema humu Bungeni ni vizuri sana Waheshimiwa Wabunge, kila mtu ana neema tofauti, ni vizuri sana ukajikita kwenye neema ambayo iko kwenye Jimbo lako kulikoni kuja kuropoka vitu ambavyo huna takwimu na huvielewi na haviwasaidii Watanzania wanaoumia na sekta ya madini. Nimesikia mchangaiji mmoja hapa anaropoka vitu ambavyo ni tofauti kabisa. Ukiangalia Wizara hii kwa sasa na zamani tulivyokuwa tunalalamika, acha Wabunge wananchi tunaowawakilisha, ni tofauti kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu humu ndani wana vitu ambavyo wanaweza kuzungumza wakati Wizara ya Miundombinu ilikuwa hapa, Mbunge mmoja tu nataka nimwambie, angeweza kuchangia kwa nguvu kubwa kwa sababu yeye ana *fly over*ya ghorofa. Kuna Wizara ya Maliasili ni vizuri sana mtu anayemiliki mbuga za wanyama Serengeti akajikita kuchangia kwenye Serengeti kusaidia watu wake kulikoni kuja kupotosha watu. Mtu anamiliki *flyover* anakuja kuchangia mambo ya dhahabu, anapotosha wananchi na

hatusaidii watu ambao tumeumia na sekta hii ya madini. Nadhani wamejielewa watu ninaowazungumza, hiyo ni *preamble*, sasa naenda kuchangia. (*Makofii*)

TAARIFA

MHE. MARWA R. CHACHA: Taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ryoba Chacha na Waheshimiwa Wabunge kwa kuangalia muda nilionao na wachangiaji waliko hapa mbele, hii itakuwa ni taarifa ya mwisho.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa kwamba kila Mbunge aliyeo humu ndani, chochote kinachohusu Tanzania kinamhusu. Natokea Serengeti, *Serengeti National Park* siyo ya Serengeti, Serengeti *National Park* is a *National Park*, hata yeye anaweza akaiongelea. Kinachotokana na *Serengeti National Park* kinakwenda kumsaidia na yeye pale Jimboni kwake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge mpe taarifa ili niweze kumuuliza kama anaipokea au hapokei, ndiyo Kanuni zetu zinavyotaka. Sasa ukiwa unamwelekeza inakuwa ngumu kidogo, zungumza na mimi ili nimuulize kama anaikubali taarifa hiyo, malizia sekunde 30.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, taarifa nayompa ni kwamba hizi rasilimali za Kitaifa, kwa mfano *Serengeti National Park*, mapato yote yanayotokana na *Serengeti National Park* yanaenda Hazina baadaye yanakuja hapa Bunge tunayagawanya yanaenda kote.

NAIBU SPIKA: Sawa, ahsante sana. Mheshimiwa Musukuma unapokea taarifa hiyo?

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo siyo taarifa wala siipokei. Hawa ndiyo wasomi tunaowategemea, huyo ni Mwalimu, ndiyo maana huwa nalalamika kila siku tuchunguze vyeti. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia sasa kwenye agenda halisi za Wizara ya Madini. Watu wa Geita tumekuwa tukilalamika muda mrefu kuhusiana na Mgodi wa *GGM* na kumekuwa na kutokuelewana. Kwa vile Wizara na dada yangu Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ni wasikivu, mje mkae na Madiwani wa Halmashauri za Geita kwa kina, siyo kwa harakaharaka siku moja, mtusikilize mtoe maamuzi ili hili suala la kudaiana katika wananchi wa Geita na Mgodi liweze kuisha. Mnavyokuja tu mna-*rush*, mnatuma barua, hawa watu hawatusikilizi, ndiyo maana tunafika mpaka mahali tunasema tijichukulie sheria mkononi, siyo vizuri, namshauri sana Mheshimiwa Waziri hebu atafute muda aje atusikilize na aweze kufikia mwisho wa kulimaliza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui huu mgodi au sisi watu wa Geita tuna tatizo gani? Tulilalamika kuhusu tanzanite, Mheshimiwa Spika akaunda Tume. Kumekuwa na Tume ya Makinikia, watu wa Geita tumeomba mara nydingi kwa nini isiundwe Tume kwa ajili ya kuuchunguza Mgodi wa Geita *GGM*? Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Rais ameshawapa tu mwongozo kwamba muangalie, mgodi ule ulikuwa unatoa dhahabu bila kuchunguzwa, sasa hivi tunaingia mpaka Halmashauri kuna tofauti kubwa, muanzie hapa ili muweze kuunda Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine wako watu ambao wamekutwa na leseni ya mgodi, Mheshimiwa Kanyasu jana alizungumza vizuri. Wameenda Mahakamani, wamehukumiwa tarehe 19 Desemba, 2016, tarehe 20 baada ya hukumu ya Majaji sita, mgodi ukaandika tena *warning* ya kuwatoa wachimbaji wale. Jana Mheshimiwa Kanyasu alivyochangia tu, leo ninayo barua hapa jana mgodi unaandika kuwafukuza watu ndani ya eneo lao ambalo Majaji sita wamewapa haki ya kukaa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge tuna haki ya kutetea watu wetu, Mheshimiwa Kanyasu amechangia jana leo kuna barua ya kuwafukuza, siku saba. Najua *GGM* wako hapa, Mheshimiwa Waziri akija hapa nataka atuambie kama *GGM* ni zaidi ya Serikali na ni zaidi ya mhimili wa Majaji sita tuelewe, lakini kama si sahihi basi naomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua ya kuweza kuwasaidia watu hawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mhimili ambao tunautegemea baada ya Serikali na Bunge kushindana ni Mahakama. Kama Mahakama ya Majaji sita, tena Majaji wanaoaminika Tanzania wametoa hukumu ya kuwapa haki wananchi hawa, inatokeaje mtu mmoja tu *GGM* anatoa siku saba kuwafukuza watu baada ya Mbunge kuchangia, hii ni dharau. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi na ana vijana shapu wanaweza kwenda hata kwa basi kusikiliza kesi hizi. Namwomba sana aende akatoe maamuzi kwenye hili suala hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Mgodi wa Buhemba, niombe sana Mheshimiwa Waziri katika vitu ambavyo tutakosea ni kuangusha wawekezaji wawili ambao mimi kama mfanyakiasha wa hiyo dhahabu, Mgodi wa Baraka na Mgodi wa Mauza, watu hawa tukifika mahali tukawafanya wakafilisika hatutakaa tupate mwekezaji Mtanzania atakayeweza kufanya kazi ya dhahabu. Sisi kama Kamati tumeenda tumeona, sawa kulikuwa na mwingiliano wa Jeshi lakini nataka niwaambie tu kwamba mazungumzo kama yanaendelea vizuri, ni vizuri tukawasaidia hawa watu wamewekeza zaidi ya dola milioni 25. Mtanzania wa kawaida amekopa, anaumiza kichwa tena darasa la saba, kitu ambacho hata watu wenye *ma-degree* wanaoropokaropoka humu hawawezi kufanya hivyo vitu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tusije tukafanya hiyo dhambi ya kuwaangusha hawa wawekezaji wazawa. Hata kama kulikuwa na makosa kwenye Wizara ya Madini na Wizara ya Ulinzi kaeni mmalize migogoro yenu watu hawa wapewe

leseni waweze kuendelea na shughuli zao. Hata kama leseni inachukua *process* ndefu kuna njia nyingine mnayoweza kuitumia ili aweze ku-cover hayo mambo aliyonayo. Hawa watu wanadaiwa na mabenki, tukiwa-*ignore* hawa hamtamkuza Mtanzania yeote kwenye biashara hii ya dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kutoa ushauri...

*(Hapa kengele illilia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, muda wako umekwisha.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja lakini dada yangu kwenye shilingi ujaribu kuja na majibu mazuri naweza nikaondoka nayo. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Vedasto Ngombale, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Kiza Mayeye ajiandae. Wachangiaji wote kutoka Chama cha Wananchi (*CUF*) mtachangia dakika saba saba kwa sababu nafasi zenu ni mbili na majina mmeleta matatu.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala zima la makinikia. Mheshimiwa Biteko alikuwa Mwenyekiti na taarifa yake ilikuwa *very hot* na baada ya taarifa ile matumaini ya Watanzania kupata mafanikio makubwa na pesa nyingi yalikuwa makubwa, lakini mpaka sasa tunavyozungumza hatujui yale matumaini na zile taratibu zimepotelea wapi. Tulitumainishwa kwamba tungepata nyingine lakini mpaka sasa naona mambo yako kimya. Mtakapokuja kuhitimisha Mheshimiwa Waziri tunaomba muwafafanulie Watanzania habari za makinikia na hatima yake imefikia wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la elimu ya madini kwa Waheshimiwa Wabunge. Elimu hii ya madini kwa Waheshimiwa Wabunge haitoshi na siyo Wabunge wote tunatoka katika kanda za madini, wale ambao wanatoka katika Kanda za Madini wana uelewa zaidi kuliko ambao hatutoki katika kanda za madini. Wakati mwingine *scope* yetu ya kutoa michango inabanwa kutokana na hilo. Kwa hiyo, niombe Waziri basi atutengenezee mazingira tupate semina tuwe na uelewa zaidi katika madini ili basi tuwe tunaweza kuchangia vizuri katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vitabu vyta wizara tumeelekezwa aina za madini zinazopatikana katika maeneo tofauti tofauti. Naomba nishauri utafiti ufanyike zaidi kwa sababu naamini Tanzania ni tajiri kwa madini na madini yanaweza yakapatikana sehemu yoyote. Kwa hiyo, kama utafiti utafanyika zaidi basi upo uwezekano wa kuweza kugundua madini katika sehemu tofauti tofauti hata kule kwangu Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilwa kwetu tukizungumza madini tunazungumzia *gypsum*, chumvi na gesi, niseme kuhusiana na *gypsum*. *Gypsum* inachimbwa Kilwa kwa ajili ya *material* ya viwanda vyta *cement* lakini kuna changamoto kubwa ambayo ni ghamama ya uzalishaji na bei ya soko ya *gypsum*. Gharama ya uchimbaji wa tani moja ya *gypsum* ni Sh.27,000, bei ya *gypsum* kwa viwanda vyta *cement* vyta Dar es Salaam ni kati ya Sh.80,000 au Sh.90,000 ukichanganya na gharama nyininge za usafirishaji na ushuru wa Serikali na kodi maana yake hawa wafanyabiashara wa *gypsum* wanafanya shughuli zao katika mazingira magumu. Tunaomba sana Serikali ije na bei elekezi ya *gypsum* ili basi wajasiriamali wetu wawze kufanya kazi ambayo inaweza ikawaleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaja madini basi akili zetu moja kwa moja zinatuelekeza kwenye jambo ambalo lina pesa nydingi lakini mchango wa madini katika bajeti ya Serikali ni finyu sana. Nitoe ushauri kwa Serikali bado ipo haja ya kuwekeza ili basi tuweze kuyatumia midini yetu ipasavyo na yatoe mchango mkubwa kwa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la madini ya gesi. Madini haya gesi ambayo kwa sisi watu wa Kilwa kwa mara ya kwanza gesi ilipatikana katika Kisiwa cha Songosongo mpaka sasa kuna changamoto kubwa katika madini ya gesi, watu wa Kilwa hatujafaidika nayo moja kwa moja, imefikia hatua hata wale ambao walitakiwa walipwe fidia kutokana na kupisha mradi ule wa bomba la gesi mpaka sasa hawajapata fidia zao. Nichukue nafasi hii kuishauri Serikali iwaangalie wadau wengine ambao walitakiwa wapate tija kutokana na madini haya ya gesi ili basi nao waweze kufaidi matunda hayo ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Serikali iwe wazi kuhusiana na madini ya gesi, ni aina gani ya gesi tulioipata. Gesi tulioipata ndiyo hii tunayotumia kupikia majumbani maana wananchi wakiona gesi hizi zinazouzwa wanafikiri ndiyo gesi ambayo tumeipata kutoka kule Songosongo. Tuwe wazi ni gesi hii au ni gesi tofauti, wananchi wafahamishwe maana kuna sitomfahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaambiwa uwezekano wa kupata mafuta upo, je, katika machimbo hayo ya gesi yaliyofanyika kuna dalili ya kupata mafuta? Serikali itueleze ni wapi tunaweza tukapata mafuta maana tumetumia gharama kubwa kuchimba gesi kama tulikuwa na tumaini la kupata mafuta Serikali iko kimya haijatueleza chochote kama tutakuja kupata mafuta au lah, maana tunaelezwa gesi na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala zima la madini ya chumvi. Sisi tunazalisha chumvi lakini gharama za uzalishaji wa chumvi na tozo zilizowekwa katika uzalishaji wa chumvi ni nyingi sana wajasiriamali wetu ambao wanajishughulisha na shughuli ile hawapati faida. Kwa hiyo, niombe Serikali ipunguze hizo tozo ili basi hawa wajasiriamali wetu waweze kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atachangia dakika kumi atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga dakika kumi, Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia Wizara hii ya Madini. Awali ya yote, nichukue fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Spika na wananchi wa Buyungu pamoja na Viongozi wa CHADEMA kwa kupoteza mwakilishi hapa Bungeni, mwakilishi makini na mahiri. Mwenyenzi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuwataka Mawaziri wote watatu wazingaties sana ushauri uliotolewa na Kamati na Nishati na Madini kwani umesheheni mambo muhimu sana. Yapo mambo kumi na moja nimeyaona pale ni muhimu sana, kama kweli dhamira ni kuiondoa nchi hapa ilipo kuelekea kwenye uchumi wa katibasi huu ushauri uzingatiwe sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijikite kwenye shughuli za utafiti wa madini kama mchangiaji aliyejita amesema kwamba hii tasnia ya madini elimu yake bado ni ndogo sana. Hawa watafiti wa madini wanapoingia kwenye Halmashuri zetu elimu haipo yaani wananchi wanashindwa kujua mipaka ya watafiti ni ipi na wao wananaufaikaje, kwa sababu mwisho wa siku wanaachiwa mashimo au mahandaki. Wanakijiji wanakuwa bado hawaelewi ni kwa namna gani wanaweza kufaidika na hizi shughuli za utafiti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano katika Kijiji cha Lilombe, kuna machimbo ya muda mrefu sana, yale machimbo yana zaidi ya miaka kumi, kuna madini ya *sapphire* na dhahabu lakini mpaka leo wananchi wa kijiji kile hawaelewi chochote zaidi na kuambulia mashimo. Nilikwenda kwa Mheshimiwa Waziri kumuulizia akaniambia kwamba ameshindwa kuweka mtu katika Mji wa Liwale kufungua soko pale ili na sisi tupate kunufaika na uwepo wa

madini, wakasema yale madini pale wachimbaji wale ni wachache, halafu madini yenyewe siyo mengi kwa hiyo hakuna haja ya kuweka Kamishna pale wa Madini. Jambo hili niungane na mchangiaji mmoja alisema kwamba kuwepo na watu kwenye Halmashauri zetu wanaoshughulika na mambo ya madini iwe ni kwa ajili ya kutoa elimu watu wakajua mahali ambapo madini yanapopatikana wao wanawajibika vipi na kusaidia hawa wachimbaji wadogowadogo ambao wanahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kutoka Liwale kwenda Tunduru ambako ndiyo kuna soko, kuna umbali wa zaidi ya kilomita 200, mtu anachukua madini kutoka Liwale mpaka Tunduru akaenda kuza kwa hiyo wanaonufaika na ushuru na mambo mengine ni wale walioko kule, je, kule ambako kuna mashimo kunaachwa nini. Kwa hiyo, jambo hilli nalo ifanyiwe marekebiso ili tuone kwamba kuna umuhimu Halmashauri zetu kuwepo na watu wanaoshughulika na mambo ya madini katika kutoa elimu pamoja na mambo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba Sheria ya Madini ifanyiwe marekebiso hasa kwenye madini haya kama mchanga, kokoto na mawe. Panapotokea ujenzi wa barabara kumetuletea migogoro sana na hasa hasa ghamama kubwa ya ujenzi wa barabara inatokana na kodi za madini. Ili kujenga barabara unatakiwa upate kifusi, kokoto lakini zenyewe unakwenda kuzilipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mkandarasi anatenda ile barabara aki-*include* ghamama hiso. Sasa barabara inayojengwa ni Serikali, hayo madini ya Serikali, ifike wakati Serikali iangallie namna ya kurekebisha hii sheria labda kuwa na *exemption* kwamba kwenye madini ambayo yanakwenda kufanya kazi za kiserikali basi kuwe na *exemption* yasitozwe kodi na kama yanatozwa kodi basi iwe ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niongelee Ofisi ya Madini Kanda ya Kusini ambayo iko Tunduru na

wamejenga tawi lao pale Nachingwea lakini bado upatikanaji wa leseni ni mgumu sana hasa kwa wale wachimbaji wadogo wanaotoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Liwale. Ni mgumu kwa sababu ni lazima waende Nachingwea wakapate hiyo leseni. Hata vile wanaporudi na hizo leseni soko nalo linawapa shida vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la uwepo wa madini. Jana nimezungukia kwenye mabanda yale kule nyuma, nimekuta kule kwetu katika Wilaya Liwale na Ruangwa kuna hiyo wanaita *green garnet* na nikaambiwa haya madini thamani yake ni mara kumi ya tanzanite. Sasa nataka njue Wizara kupitia kile Kitengo cha Utafiti wa Madini wameyatangaza kwa kiwango gani na mkakati upi umewekezwa kutafuta wawekezaji ili upande wa Kusini uchumi wetu ukaimarika kwa sababu ya upatikanaji wa hayo madini ambayo yameonekana kwamba yenye yana thamani kubwa kuliko tanzanite.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli napata ukakasi kidogo, nimesoma kwenye kitabu kile cha Mheshimiwa Waziri kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 inaonyesha kama maduhuli yameongezeka, imekusanya maduhuli zaidi ya asilimia 103 lakini sasa unakuja kwenye fedha za maendeleo zimekwenda asilimia 0.8. Nashindwa kuelewa inawezekana vipi ng'ombe huyo ambaye unaona ametoa maziwa ya kutosha ndiyo anayenyimwa malisho, tunadhamiria nini, mwisho wa siku tunataka kwenda wapi? Kama Wizara inaweza kukusanya maduhuli ikapindukia lakini kwenye fedha za maendeleo wakawa hawapewi fedha. Bado sijapata ufahamu vizuri tunakwenda wapi, yaani dhamira yetu ni ipi katika hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Dakika kumi zimeisha?

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tukiendelea na uchangiaji niwakumbushe kwamba salamu za kuhusu Mbunge mwenzetu ambaye amefariki alishazitoa Mheshimiwa Spika na hivyo Kikanuni hairuhisiwa tena Mbunge mwingine kuzungumzia jambo hili. Niwakumbushe kwamba hairuhusiwi kutoa pole maana nimeshawasikia Wabunge wawili, watatu sasa nalazimika kuwakumbusha Kanuni zetu zinasemaje. Pole ama pongezi zikishatolewa na Spika zinakuwa ni kwa niaba ya Wabunge wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Goodluck Mlinga atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda, Mheshimiwa Julius Kalanga ajiandae.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naomba ni-*declare interest* kuwa na mimi ni mchimbaji ambaye mpaka leo bado sijafanikiwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Rais kwa mpango wake wa kuzuia makinikia kupekwa nje ya nchi. Kwa nini nasema hivyo? Tanzania ni nchi ya nne kwa uzalishaji wa dhahabu nyingi katika Bara la Afrika na nchi ya 16 duniani tukitanguliwa na China, Australia na Russia. Katika orodha ya nchi matajiri wa uzalishaji wa mali tupo lakini mafanikio ya Serikali na wananchi yako chini. Kwa hiyo, hapa nimeona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kujenga ukuta katika mgodi wa Mererani kwa sababu haya ni madini adimu katika dunia hii yanatoka Tanzania tu. Licha ya hivyo,

Tanzania pia ni nchi ya nne kwa uzalishaji wa gesi katika Bara la Afrika na ni ya 22 katika dunia katika uzalishaji wa gesi. Hapo ndipo unapoona dhamira ya Mheshimiwa Rais katika kulinda rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Spika naye kwa kuona kuwa suala la gesi ni muhimu kwa sababu nchi matajiri duniani ndiyo zinaongoza katika utoaji wa gesi na madini ya aina mbalimbali. Katika orodha za nchi maskini duniani Tanzania ni ya 25 toka mwisho tukitanguliwa na *Central/Africa*, Congo na Malawi. Kwa suala la madini nchi yetu ipo juu, vinara katika kutoa madini lakini katika nchi maskini na kwenyewe tuko juu, ndiyo tunaona kuwa Mheshimiwa Rais ana dhamira nzuri na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri pia Mheshimiwa Rais afanye pia *reshuffle* katika Wizara ya Madini kwa sababu watendaji wa Wizara ndiyo waliopelekea nchi hii kufika hapa leo hii. Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri tunajua mnafanya kazi vizuri lakini nawapa angalizo watendaji wa Wizara zenu ni wapigaji, nimeshaongea hapa tangu mwanzo kuweni nao makini hasa wanasheria. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili naomba nije kwenye Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro na Wilaya zake za Ulanga, Malinyi, Kilosa, Mvomero, Morogoro Vijijiini, Matombo ni wilaya tajiri, tunatoa dhahabu tena dhahabu zake siyo kama za Wasukuma kule, dhahabu zetu sisi ni asilimia 98. Tunatoa rubi, *graphite*, *copper*, *uranium* kwa hiyo mkoa wetu ni tajiri kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa angalizo kwa Serikali hasa Wizara, kuna watumishi wa Wizara ya Madini wamehodhi maeneo makubwa kwa kutumia majina mengine. Anapotokea mtu anapotaka kuchimba unasikia eneo hili lina mtu, kumbe mtu mwenyewe ni mfanyakazi wa Wizara ya Madini. Kwa hiyo, tunaomba leseni zote ambazo ziko Mkoa wa Morogoro zifuatiliwe kwa undani zinachimbwa au lah, wamiliki halisi ni watu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa Ulanga. Jimbo langu la Ulanga miaka ya 90 kuna kijiji kimoja kinaitwa Lukande kilikuwa kinajulikana Thailand. Thailand walikuwa wanajua Lukande kuliko Dar es Salaam, lakini kijiji hicho mpaka leo hii kimechimbwa madini yameachwa mashimo tu hawajanufaika lolote. Sasa hivi chini ya uongozi wa Mbunge wao kijana machachari nahakikisha hamna wizi wowote wa madini utakaofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu lina makampuni makubwa mawili ya uchimbaji wa graphite ambayo ni *TanzGraphite* na Mahenge Resource. Mahenge Resource ndio tumeitambulisha juzi, inaanza mchakato wa kutaka kuongea na wananchi ili kuwaahamisha na kufanya malipo, *TanzGraphite* ina miaka sita lakini bado ina ubabaishaji, wamefanya uthamini wa mali za wananchi mwaka mmoja na mwezi mmoja, leo hii wanataka kuja kuanza kulipa. Sheria inamtaka ukishafanya uthamini miezi sita ina-expire lakini wao imepita mwaka mmoja na mwezi mmoja wanataka kulipa, wanataka kulipa kwa mkataba upi wakati tayari ile tathmini imesha-expire.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu, nimewaambia wao wenyewe kuwa uthamini unatakiwa ufanywe upya, maana tukiongea sisi Wabunge wanasema wameongea wanasiasa, tafadhali naomba tusidharauliane kwenye kazi, wafanyakazi yao na mimi kama Mbunge niwatetee wananchi wangu. Nahikikisha hakuna mwekezaji atakayewekeza kwa kukiuka sheria. Nawahakikisha wananchi wangu wa Ulanga na wananchi wa Ipanko walale usingizi mzuri, hakuna uwezekazaji mpaka wananchi wote wamelipwa haki yao inayostahili kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine kwa wananchi wa Ulanga, tunaomba ofisi ya Madini ifunguliwe katika Wilaya ya Ulanga. Ulanga tuna madini mengi, lakini hakuna Afisa Madini ambaye anayeishi huko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia kuhusu wachimbaji wadogowadogo, Mheshimiwa Waziri tumeshaongea sana kuhusu wachimbaji wadogowadogo, hasa wa *gemstone* nikiwemo na mimi ambaye mpaka leo hii sijanufaika. Uchimbaji wa madini ni kama kamari lakini Serikali unapochimba haiangalii umewekeza shilingi ngapi na umepata kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nimechimba miaka miwili, nimetumia shilingi milioni mia moja, siku napata jiwe la shilingi milioni ishirini, Serikali inataka kodi hapo hapo, hajui mimi nimewekezaje. Ndiyo maana tunawaambia, mtoe semina na muwekeze kwa wachimbaji wadogowadogo, muwe nao karibu mtajua matatizo gani wanayapata. Sasa wewe hujui mtu amewekeza kiasi gani, haujui amepata kiasi gani, unaenda kumdai kodi, kwa mfumo huo hamtopata kodi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana leo hii Mererani mmjenga ukuta sawa, lakini wale wachimbaji wadogo wadogo wanawapiga chenga. Cha msingi ni kuwafanya wawe marafiki inakuwa rahisi hata wao kujitolea kutoa kodi kwenu, kwa sababu inakuwa tayari mmeshawajengea mazingira ya ukaribu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuliongelea ni kuhusu kujenga ule mtambo wa kuchenjua dhahabu. Serikali ituambie sasa ni lini mtambo huo utakuwa tayari, kwa sababu tunajua dhahabu bado kabisa haijachimbwa Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kidogo mpaka Waziri aje na majibu ya hoja zangu. (*Kicheko/Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Sixtus Mapunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga, Mheshimiwa Jumanne Kishimba ajiandae.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kumpongeza sana, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiangalia hii sekta ya madini. Kuchimba madini katika *status* yetu ya sasa siyo jambo ambalo ni *too early* au *too late*, maana yake kuna wengine wanalamika tumeibiwa au tumefanyiwa nini, ukiangalia Tanzania ilivyo na madini ya kila aina kuanzia Mto Ruvuma kupakana na Msumbiji, mpaka North Mara, kila mkoa utakaogusa vitu villiyoko chini havijawahi kuguswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukurupuka tu kwenda kuanza kwenda kuchimba leo bila kutengeneza mifumo mzuri ya kisheria na ya kiutendaji katika sekta ya madini, hatutafanikiwa. Nimshukuru Rais na naishukuru sana Wizara, nimpongeze Waziri anafanya kazi vizuri sana na Naibu Mawaziri wake wawili, kila siku unawaona wanasililiza wachimbaji wadogowadogo, unaona wako na wachimbaji wakubwa, unaona kabisa kuna vitu wanakusudia kututoa hapa tulipo kutupelekeea mbele zaldi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo mwanzo tuko kwenye mpito, kutengeneza mfumo bora wa kujinuifaisha na madini yetu lakini wakati huo Serikali lazima ipate mapato kwa ajili ya kuleta shughuli za maendeleo kuendeleza watu wake. Haya mambo yote yanahitaji utulivu wa akili, ushirikiano na kupeana moyo. Huu mfumo ni mpya, hakuna mtu asiyejua biashara ya dhahabu ni ya familia kubwa duniani, wote tunajua, jinsi ya kuingilia hili lazima utumie ubongo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu walianza hii biashara wanasema Karne ya 5 baada ya Kristo mpaka leo

wameendelea kuchukua dhahabu na ndiyo wenye stock kubwa ya dhahabu duniani, Uingereza na Marekani. Kwa hiyo, unapoingia kupambana na hawa watu, lazima uwe na mfumo mzuri wa kisheria vilevile uelewa wa watu wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa minajili hiyo, naishauri Serikali kwamba inapoendelea na kazi yake nzuri ya kutengeneza mifumo, kwa namna yoyote ile mikataba inayotengenezwa na hao waliokuwa wakitunyonya siku zote na ndiyo tunaowategemea wanunue madini yetu, kwa haraka hawa hawawezi wakakubali kiurahisi, lazima kuna maeneo watatuhujumu. Lazima tuende na mpango 'B' kipindi tunategemea wawekezaji kuja, Serikali kwa dhati kwa sababu dhahabu haiozi hata ikachimbwa ikahifadhiwa hapa hapa kuna siku thamani yake itakua, niiombe Serikali ijielekeze kwa wachimbaji wadogo wadogo kwenye yale maeneo ambayo tumekwisha kuyaainisha, kwa sababu tumekwisha kuthibitisha kwamba wachimbaji wadogowadogo ndiyo wale wanaoleta tafsiri ya maendeleo, maendeleo *is a social centred*. Kila sehemu wachimbaji wadogo wadogo walipofanya kazi zao vizuri maeneo yale yalithibitika kuonekana yakiendelea sana watu wakijenga nyumba vizuri na kadhalika. Tukii-*paralyse* hii sekta ya wachimbaji wadogowadogo hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Wizara, inafanya vizuri katika kuwasaidia ruzuku lakini iwasaidie vilevile katika elimu, itoe elimu ya biashara ya madini lakini itoe elimu ya madini katika ujumla wake. Niliwahi kuongea na mtu mmoja anafanya kazi katika sekta ya madini huko China, akasema Tanzania mna bahati ya kuwa na maliasili za kutosha lakini hamjasomesha vya kutosha watu wakawa na uelewa wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali watu wale 20, 30 tunaowapeleka kila mwaka kusoma nje, kwa rasilimali tulizokuwa nazo ni wachache sana, tuongeze nguvu ya kutosha tuwapate wengi ili kila mkoa uwe na wataalam na tufanye *assessment* vizuri, hata kama mwekezaji akifika

tunajua *exactly* anakwenda kwenye madini ya aina gani. Wakija kufanya *assessment* wao matokeo yake wanatupunja na kutuibia nchi yetu inaendelea kuwa shamba la bibi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa sehemu moja, nimepitia hotuba ya Waziri, kwenye sehemu ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Hii taasisi ni muhimu sana katika sekta ya madini. Nimeangalia hapa, maduhuli yao ni shilingi milioni 350, mwaka uliopita walikusanya shilingi milioni 294, tafsiri yake hiyo ndiyo watumie kwenda kufanya *research* nchi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wana majukumu tisa, yote ni mazito, ila niyaseme mawili tu. Jukumu la nne wanasema, kuwasaidia wachimbaji wadogowadogo hasa katika kubaini umbile na aina ya mbale, kutambua aina na ubora wa madini, pamoja na namna bora ya uchenjuaji. Hili jambo ni kubwa, shilingi milioni 350 haiwezi ikatosha hawa wakaweza kuifanya kazi hii nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wana kazi nyingine ya kisayansi *very technical*, ya tano, kuratibu majanga asilia ya jiolojia kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volcano, maporomoko ya ardhi na kutoa ushauri wa namna bora kujikinga. Kwa bajeti ya shilingi milioni 350 hawawezi wakaweza *ku-predict* leo Oldonyolengai lini ile volcano *it-erupt*. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijaribu kuwaangalia hawa ndiyo watakaotusaidia kujua nchi yetu tuna rasilimali kiasi gani, ziko wapi, zenyе thamani gani na zichimbwe vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Julius Kalanga atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Oran Njeza, ajiandae.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii, kwa kweli niwe muungwana kwamba mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Historia ya uchumi wa madini kwenye nchi yetu kuanzia siku za nyuma na hapa tulikofika, hauwezi kabisa kuacha kutambua juhudini zinazofanywa na Serikali katika kudhibiti utoroshaji wa madini nchini kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dhamira ya kweli katika kushughulikia jambo hili. Hata hivyo, katika dhamira hiyo hiyo ni lazima tutambue kwamba misingi ya wizi wa madini kwenye nchi yetu ulianzia wapi na hatuwezi kulinda rasimali za nchi hii kwa mtutu wa bunduki wala kwenye majukwaa ya siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa naloliona ni sheria zetu haziko katika mazingira mazuri ya kulinda rasimali ya Taifa. Kwa hiyo, naamini katika nia njema hii ya Serikali, ni lazima tutambue sheria zetu ndiyo kinga pekee katika vizazi vyote kusaidia kusimamia rasilimali ya Taifa hili. Inawezekana Rais huyo akawa na nia njema lakini kama hatujaweka misingi imara kwa ajili ya kusimamia rasilimali zetu hizi, atakuja Rais mwagine tutarudi kule kule tulikotoka. Kwa hiyo, hatutamani ulinzi wa rasilimali zetu utokane na utashi wa mtu mmoja au kikundi cha watu wachache. Tunatamani ulinzi wa rasilimali zetu utokane na utashi na sheria za nchi ambazo zimesimamiwa vizuri na ambazo zinalazimisha viongozi kusimamia sheria hizi. Tusije tukatoka mahali ambapo tunaenda mbele tunarudi nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba niseme mambo machache. Ukiangalia katika ahadi ya makenikia ya dola milioni 300, ambapo mpaka sasa hivi hatujapokea, hii ni kwa sababu ilikuwa ni utashi wa wale wenye maknikia kuahidi, lakini ingekuwa ni jambo la kisheria fedha zetu tungeshapata, hatujapata kwa sababu ilikuwa inaonekana kama ni hisani. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema,

lazima tuwe na sheria ambazo zinalinda rasilimali zetu.
(Makofî)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kidogo kwenye changamoto zinazowakabili wachimbaji wadogo na ni muhimu Mawaziri wakatuelewa katika hili. Hatuchukii kabisa walioko katika maeneo yale Serikali kukusanya kodi. Kwa mfano, madini ya ruby ambayo bei yake imeshuka kwa sababu ninyi mnataka tukate kama inavyokatwa tanzanite, madini haya hayafai kukatwa na ninyi mnachukua muda mwingu sana kutoa mwelekeo kwamba ni namna gani mnataka madini yale yasimamiwe. *(Makofî)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuja Naibu Mawaziri wawili kule Longido kwetu, wakatoa ahadi za kutosha mpaka leo hawajatekeleza. Ni muhimu sana mkashughullikia jambo hili kwa haraka, siyo mnafanya ziara tu tunakuja tunawapokea mnatupa matumaini na matumaini hayo hamyatekelezi. Wachimbaji walioko kwenye maeneo yetu wanapata changamoto nyingi sana kwa sababu madini haya yameshuka bei kule Mundarara na mpaka leo hatujaua nini msimamo wa Serikali katika hilo. Wamekuja watu wawili ni vijana wakatuahidi kwamba tutaleta hizi sheria mara moja, hakuna kitu. Naomba leo waniambie hili suala la Mundarara linamalizika lini. Tena Waziri akasema Wamasai tunajenga, tunajenga kweli, sisi hatuo kama Wasukuma, sisi tukipata fedha tunajenga, tunanunua vitu vingine, sasa watuambie ni lini suala hili la Mundarara litafika mwisho kuhusu madini ya ruby ili wananchi wetu waweze kunufaika na madini haya. *(Makofî)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye hilo, eneo la madini ya Mererani. Naomba Wizara waseme, nani anayepaswa kusimamia wachimbaji wadogo, Polisi wamegeuza wachimbaji wadogo wa Mererani kuwa chanzo chao cha kupata fedha. Wale wanaofanya biashara ya madini siyo wachimbaji, wanununua wakauze, lakini wakishatoka kununua yake madini watu wanakamatwa

wanaambiwa lipa kodi. Sasa anayekusanya kodi ni *TRA* au Polisi? Wasaidieni wananchi hawa, wanaumizwa kabisa barabarani na bahati mbaya wale Polisi wamejua maeneo yao, akikutwa na jiwe anaambiwa lipa kodi, sasa analipaje kodi wakati hajauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule ni ujasiriamali tu, kuna wanaochimba lakini kuna wale wanaookota kwenda kuuza. Ni utafutaji wa riziki, watu wanateseka katika kutafuta lakini wanachajija kodi ambayo hauna sababu ya msingi. Lazima mtupe maelekezo ya wale wachimbaji wadogo na wale wafanyabiashara wa madini watakavyonufaika na watakavyolipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, Mheshimiwa Waziri Rais alivahi kusema kwamba suala la utoaji wa leseni lizingatie wananchi wanaokaa kwenye maeneo yale. Tuna tatizo la mchanga wa kujengea wale watu wanaenda kushika PRkwenye mashamba ya wananchi, kwenye vyanzo vya maji, wanapewa huko kwenye Kanda wakija huku hawaelewi chochote, hawasilikilizi wananchi, wanawaondoa wananchi, hatuna manufaa nayo, wanatuachia mashimo. Ni muhimu mbadilishe ile sheria ili mtu anayetaka leseni ya madini kwenye eneo fulani aanzie kule kijijini na hakutakuwa tena migogoro kwa sababu wananchi watakuwa wameshiriki kuanzia mwanzo mpaka mwisho, kuliko kuja kuingia kwenye migogoro ambayo hauna sababu ya msingi. Hii sheria naomba muipitie muone namna ambayo mnavyoweza mkafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tuna tatizo la ujisadi katika Wizara hii katika sehemu ya watumishi. Wako Makamishna Wasaidizi 12, miezi sita sasa wamesimamishwa kazi na Katibu Mkuu wa Wizara na wameajiriwa watu wengine katika nafasi hiyo, kwa hiyo, kuna malipo mara mbili, yaani wale walioko kazini na wale ambao hawako kazini. Kama Serikali inaona Makamishna hawa hawatoshi, wastaafisheni kwa maslahi ya umma muwalipe mafao yao,

kuliko kuwalipa Makamishana Wasaidizi 24 kwa wakati mmoja, wakati uhitaji wenyewe ni 12. Wale ambao mmewarudhisha nyumbani, wapeni maslahi yao, kama hamuwapi, warudisheni kazini, kuliko kuwaweka nyumbani halafu, wengine wanalipwa. Hii ni hasara kwa Serikali kwa kulipa watumishi pasipokuwa na sababu ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, ni suala hili la makinikia na ulinzi wa ukuta wa Mererani. Ukuta wa Mererani ni hatua ya kwanza ya kudhibiti rasilimali zetu na madini haya nami naiunga mkono, lakini tukiendelea na utaratibu huo hivi huo ukuta tutalinda kwa mtutu mpaka lini, tutalinda na Jeshi mpaka lini? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda umeisha, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Jumanne Kishimba atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye dhahabu. Katika Jimbo langu la Kahama ni mionganoni mwa maeneo ambayo yana machimbo mengi sana madogo madogo, pamoja na mgodi mkubwa wa Buzwagi na jirani yangu Bulyanhulu. Kinachosumbua sasa hivi, kule ni Sheria ya Madini ambayo watu wa migodi mikubwa wanatumia sheria hiyo hiyo na wachimbaji wadogo wadogo wanatumia sheria hiyo hiyo. Sasa hivi wachimbaji wadogo wadogo, akitoa mifuko 10 ya mawe ya dhahabu, anatoa mfuko mmoja kwa ajili ya madini, mfuko mmoja kwa ajili ya

TRA, mfuko mmoja kwa ajili ya Halmashauri na mfuko mmoja kwa ajili ya mwenye shamba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu huyu akimaliza tena kusaga mchanga ule kwenda kutoa dhahabu analipa tena, mchanga ule tena ukienda kuchenjuliwa unalipiwa tena lakini huyu mwenye mgodi mkubwa akilipa ushuru wake yeye atarekebisha kwenye hesabu zake za *TRA* atapunguza zile gharama alizolipia, lakini huyu mchimbaji mdogo hana mahali ambapo anaweza kwenda *ku-claim* fedha aliylipa. Matokeo yake inasababisha kuwa na rushwa na migogoro mingi sana maeneo yale. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ya Madini ni vizuri ikaoanisha kati ya sheria ya migodi mikubwa na sheria ya wachimbaji wadogo wadogo amba ni kama wakulima wadogo wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala hili la dhahabu nafikiri Serikali ingetamka wazi kwamba inataka kufanya kweli kazi ya dhahabu au ni kama tunataka kuruhusu uchawi lakini wakati tukiona bundi au fisi tunaogopa. Tanzania haina elimu ya biashara ya madini ina elimu ya miamba na tunachoibwi na matatizo yetu makubwa yako kwenye elimu ya biashara ya madini ambayo haiko shulenii. Kwa hiyo, ni vizuri kama tunaamua kuruhusu biashara ya madini ionekane kwamba madini yameruhusiwa lakini hata tukiunda Tume 100, kama hatujasema wazi kabisa tunataka nini kwenye madini, bado tuna wakati mgumu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Uganda leo ina-charge service *levy ya export* 0.5%; Rwanda wana-charge 0.6%; Burundi 1%; Tanzania tuna-charge 14%. Mheshimiwa Waziri hata kama ni wewe unaweza ukapata dhahabu ya Sh.10,000,000 ukalipa Sh.1,400,000, inawezekana? Umechimba peke yako, ukapata dhahabu ya Sh.10,000,000 ukabebe kupelekea Serikalini Sh.1,400,000, inawezekana? Wafanyabiashara hawa wanafanya biashara ya madini zaidi ya miaka 10 hata mke wake hajawahi kuiona dhahabu, ni vipi Serikali inawezekana? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ya wachimbaji wadogo wadogo imeajiri zaidi ya watu milioni 5. Kwa hiyo, ni kweli Serikali kwenye kitabu inaonesha wamechangia asilimia 2 lakini tunapoteza zaidi ya tani 2 au 3 za dhahabu kila wiki. Kwa nini Serikali isiruhusu dhahabu ikawa 1% na ali pe anaye-*export* ili hawa wachimbaji wadogo wadogo waondokane na huu msururu wa usumbufu walionao halafu wale wenye migodi mikubwa waendelee na *procedure* ya kawaida ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia hata jirani zetu ambao wana madini wanaweza kuyaleta hapa kwetu. Ni vizuri Serikali ikafikiria sana kuruhusu madini kutoka nje. Ni kweli tuna mikataba ambayo inasema lazima wapate *certificate of original* lakini ni kweli sisi tunapokea wakimbizi kutoka Congo, tunapokea kila aina ya matatizo kutoka nchi jirani, tunaweza kupata ebola, mbona tunakataa kupo kea dhahabu na tuko tayari kupo kea dola? Ni vizuri Serikali ikafikiria upya maana dhahabu haina alama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini watu hawa watanunua mali hapa na sisi tutapata pesa kutoka kwenye kodi. Sisi hatufanyi *service* Msumbiji, hatutengenezi barabara Congo ina maana tutapata pesa ya bure. Kwa kuwa Mwanasheria wa Serikali na Waziri wa Sheria wapo hapa waiangalie sana hii Sheria ya Madini ambapo dhahabu ni moja lakini inapatikana kutoka kwenye vyanzo viwili tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nahitimisha mchango wangu, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Selemani Kakoso ajiandae.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Madini. Ni kweli hii Wizara

ndiyo inayosimamia rasilimali zetu muhimu sana ambazo Mwenyezi Mungu ametupatia sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri mwenyewe na Naibu wake wawili wanafanya kazi nzuri sana. Pia nimpongeze Katibu Mkuu na uongozi mzima wa Wizara. Hawa watu nimeshuhudia mwenyewe wanafanya kazi *long hours*. Walinipa *appointment* na mkutano na wao saa 2.00, nikauliza saa 2.00 ya asubuhi wakasema hapana ni saa 2.00 usiku. Kweli tumefanya mkutano saa 2.00 usiku mpaka *midnight*. Nilipotoka nikawauliza walinzi hivi hawa ndiyo *style* yao ya kufanya kazi wakasema ndiyo na tunategemea watatoka saa mbili baadaye. Kwa kweli hiyo ni ishara nzuri, hii Wizara ni mpya, ina mambo mengi mageni, inahitaji watu wenye moyo wa aina hii, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata kwenye matokeo ya Wizara, tulitegemea wangkusanya kama shilingi bilioni 194 lakini kwa miezi tisa wamekusanya shilingi bilioni 225, hilo ni ongezeko kubwa sana. Kwa miezi tisa kama ni shilingi bilioni 225, nina imani kwa mwaka mzima kama makusanyo yanaendelea *evenly*kwa miezi itakuwa ni shilingi bilioni 300. Hili ni ongezeko kubwa ambalo ni karibu asilimia 54, kwa kweli huu ni utendaji mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Kamati uchambuzi wao ni mzuri sana, umesema matokeo mazuri haya yametokana kwanza na udhibiti wa utoroshaji wa madini, pia ongezeko la mrabaha na kuna 1% ya makusanyo ambayo hiyo ni kodi mpya. Nafikiri imetuletea matokeo mazuri na mimi nafikiri tukijikita katika haya machache tu, kwa vile haya ndiyo yatakuwa makusanyo yenye uhakika kwa muda mrefu yatatuletea *sustainable growth* kwa muda mrefu kuliko yale *one off* ambayo labda tunategemea tutapata makusanyo kiasi hiki hayatatusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nikubaliane na maoni ya Kamati. Kwa muda mrefu tumeona utendaji wa *STAMICO* si mzuri. Mimi ningombaa sana Serikali katika hizi

Wizara ingeangalia majukumu yao ya kimsingi, yale ambayo ni *operational*/wayaache. *STAMICO*sasa hivi inapata hasara kubwa sana, madeni ya shilingi bilioni 60 na sijaangalia *balance sheet* yao huko inaonesha ina shimo la kiasi gani. Sasa ukiwa na hali ya namna hiyo huna haja ya kuyalea mashirika ya aina hii. Zile shilingi bilioni 8.6 ambazo wametengewa na Wizara nafikiri Wizara ingeangalia kupeleka mahali pazuri zaidi ambapo kutaisaidia Wizara kuongeza mapato na maduhuli ya shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyo-recommend Kamati, nafikiri hiyo migodi ambayo ilikuwa inaendeshwa na *STAMICO* wapewe Watanzania wazawa, wachimbaji wadogo wadogo na wachimbaji wa kat. Nina imani kuwa Serikali itapata mapato makubwa kupitia kwa hawa kuliko tukitegemea kuendelea na *STAMICO*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kuikumbusha Wizara tu, nafikiri ilikuwa ni *overlook*. Kuna mgodi wa Niobium kule Mbeya unaitwa *Panda Hill Niobium Project*. Mgodi huu thamani yake ni dola kama bilioni 6.8, project nzima na tunategemea Serikali kama ukianza utaleta kodi kama ya dola bilioni 1.4 ambazo nafikiri ni pesa nyngi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimelisema hilo? Ni kwa sababu huu mgodi si wa leo ni wa siku nyngi, uligunduliwa mwaka 1953. Hii kampuni mpya imepewa *license* ya mgodi huu mwaka 2013 na wameshawekeza zaidi ya dola milioni 28 sasa hivi walikuwa wanajipanga kuanza. Huu mgodi ni muhimu kwa Tanzania lakini ni mgodi pekee Afrika wa Niobium, migodi ya aina hii iko mitatu duniani; migodi miwili iko Brazil na mgodi mmoja Canada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika biashara ya madini hatuko peke yetu inategemea *speedy*ya kuingia sokoni. Nina imani huu mgodi ukianza haraka utailetea Serikali pesa nyngi sana. Dola bilioni 1.2 si ndogo, ni nyngi, zikiongezwa kwenye mfuko wa Serikali, nafikiri itaipunguzia mzigo hata Wizara ya Fedha tunapolia maji kuna hela huku zimebaki. Kwa hiyo,

naiomba Wizara iharakishe *process*, kwanza ukiangalia Wizara ni mpya hii inaweza kuwa *project* kubwa ya kwanza ya madini kwa mwaka huu ukiachilia mbali za miaka mingi za dhahabu, almasi na tanzanite.

Mheshimiwa Naibu Spika, orodha ya madini ambayo nimeikuta pale nje kwenye maonesho ni kubwa mno, ni namna gani twende haraka sokoni. Madini vilevile yanaendana na teknolojia. Tusubiria dhahabu na tanzanite lakini teknolojia iki-*change* unaweza kukuta yakabaki kama mawe tu tunayoangalia huko nje milimani. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara ijitahidi kufanya haraka ili hizi rasilimali zetu tuzitimie vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wote kwa jinsi wanavyofanya vizuri. Naomba pia kumpa pongezi Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kuiona hii sekta ya madini ni muhimu sana na jinsi anavyoiedeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niongelee Mkoa wangu wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro una madini mbalimbali. Kwa mfano, Wilaya ya Morogoro Vijijini kule Mkuyuni pamoja na Matombo kuna madini ya dhahabu. Madini haya ya dhahabu yanachimbwa na wachimbaji wadogo wadogo. Hawa wachimbaji wadogo wadogo hawana elimu na mara kwa mara wanachimba na kusafishia kwenye mto mkubwa uliopo hapo hapo Mkuyuni na wanatumlia zebaki ambayo wakati mwingine si nzuri kwa binadamu. Kwenye kitabu cha Wizara sikuona vizuri kama Mkuyuni na Matombo imeonekana kuwa tuna dhahabu na wanachimba sana na ipo miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ulanga kuna rubi nayo ni ya muda mrefu, miaka nenda rudi. Kwa hiyo, naomba itambuliwe kuwa Ulanga kuna rubi na inachimbwa na wachimbaji wadogo na inaonekana hawana elimu na soko. Naomba sana hawa wachimbaji wadogo waweze kupatiwa teknolojia nzuri ya uchimbaji wa madini na kupatiwa soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Afisa Madini wa Mkoa, naamini mikoa mingi au kila mkoa kuna Afisa Madini, lakini nilivyosikia na navyojuja hakuna Maafisa Madini wa kutosha kwenye wilaya zetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hilo aliangalie kwa sababu hawa Maafisa Madini ndiyo wanapaswa watoe elimu kwa wale wachimbaji wadogo ili waweze kuelewa wachimbeje madini hayo na wauze wapi. Kwa sababu hawana elimu wanajichimbia wenyewe, hawana vifaa, wakiona jiwe hawaelewi kuwa ni kitu gani wanaendelea wenyewe bila ya kuelewa. Kwa hiyo, naomba hawa Maafisa Madini waweze kupelekwa mpaka huko wilayani ambako madini yanachimbwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kilosa, kuna madini mengi hata mengine siyajui, ni majina ya watu kama Felista nilikuwa sijui kuna madini yanaitwa Felista. Felista ni jina la mama yangu, sasa nakuta kuwa kuna madini yanaitwa Felista. Pia kuna madini ya rubi, *red garnet, moonstone* lakini sikusikia kama yametajwa, naomba Mheshimiwa Waziri ayafanyie kazi. Mkoa wa Morogoro ni tajiri kwa madini naomba wauangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, nimeona kwenye kitabu Mheshimiwa Waziri amesema kwamba utafiti wa awali umefanyika kwenye Mkoa wa Morogoro ila sikuona kama haya madini yametajwa kuwa yanatoka kwenye Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, naomba iangaliwe kuwa tunatoa madini na tuweze kupata wawekezaji kusudi tuweze kuwa na maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wadogo hawana elimu, wapewe elimu na ruzuku ili kusudi

waendelee vizuri na uchimbaji wao na waweze kuongeza mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa unafahamu kuna Chama cha Wanawake Wachimbaji naomba nao waweze kupatiwa elimu kusudi waweze kuchimba. Unajua ukimuendeza mwanamke hasa kwenye machimbo na sasa hivi tumesema kazi yoyote hakuna mwanaume hakuna mwanamke yejote yule anaweza akafanya kazi hii, naomba Mheshimiwa Waziri awaangalie hawa wachimbaji wanawake waweze kuendeleza nchi yetu na kujiletea mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Morogoro kuna wawekezaji wamekuja, kuna mazungumzo yanaendelea hasa Ulanga. Naomba sana waangaliwe kwa sababu hawa wawekezaji tunaomba wawekeze lakini wasiwasumbue wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wapate nafasi yao na hawa wawekezaji waweze kupata nafasi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *graphite*, sijui kama Mheshimiwa Waziri anajua kuwa Ulanga kuna *graphite*. Kwa hiyo, naomba Waziri aangalie na Ulanga ili iweze kuendelea na kunufaika na madini yanayopatikana huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ujenzi wa ukuta wa Mererani. Kwa kweli amefanya jambo zuri katika kudhibiti utoroshaji wa tanzanite ambayo ilikuwa inatorosha inaunzwa nje na haifahamiki kuwa imetoka Tanzania inafahamika imetoka mahali popote pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninalokazia sana ni kuhusu soko la madini hapa nchini. Nashauri Waziri ahakikishe soko la madini linakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *tin* kule Cherwa ambayo tangu nazaliwa naisikia kule lakini mpaka sasa hivi hakuna kitu chochote kimefanyika kuhusu madini haya.

Mheshimiwa Waziri anafahamu madini ya *tin*, naomba sana nayo yaangaliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia hoja hii muhimu sana. Ni hoja muhimu kwa sababu ni madini ambayo yanaongeza pato la Taifa. Kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hatua mbalimbali ambazo amezichukua kuweza kuboresha sekta hii ya madini na mpaka sasa hivi tunaanza kuona faida yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kifupi sana utaona Wizara hii kazi ambayo imefanya ni kubwa sana kwa sababu imeweza kuongeza pato la Taifa kwa asilimia 4.8. Hii ni kutokana na uimarishaji wa mifumo mbalimbali ya madini ambayo imefanyika kwa haraka sana, uangalajji wa mikataba mbalimbali ambao umefanyika pia kwa haraka sana na utungaji wa sheria mbalimbali ili kuweza kuendana na hali ambayo inaweza kurahisisha kufanya mchango huu wa madini uweze kuongeza pato la Taifa na uboreshaji wa biashara hii ya madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameunda Tume mbalimbali kwa lengo la kuweza kusaidia uimarishaji huu ambapo kwa kweli manufaa yake yanaanza kuonekana sasa hivi. Utoroshaji ulikuwa ni mkubwa sana na sasa hivi udhibiti ambao umefanyika ni mzuri sana. Nashauri Wizara na Mheshimiwa Waziri muendelee na kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo napenda kushauri ni kuhusu tanzanite kule Mererani. Nafahamu kwamba ukuta umejengwa, ni kazi nzuri sana ambayo

imefanyika. Kwa kipindi kifupi tu cha miezi mitatu ukuta ule umeweza kujengwa ambao ni mkubwa sana na umeweza kuzaa matunda kwa sababu sasa udhibiti wa tanzanite umeanza kuonekana. Tanzanite ilikuwa unatoroshwa sana na kama unaona takwimu ambazo zimetokea kwenye mitandao mbalimbali India imeonekana kuna tanzanite nyingi sana, ikifuatiwa na Kenya na sisi ambao ndiyo wazalishaji hatuna tanzanite au kiwango chake ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeshauri kama nilivyoshauri Kamati kwamba *camera'sziwekwe* na ziwekwe kuanzia kwenye ulipuaji kule chini ili kila kitu kiweze kuonekana. Hivi ni viboresho ambavyo vitaongeza udhibiti pale pamoja na ule ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, kuna suala la kujenga kituo ambacho kinakuwa *one stop* pale pale kwenye mlango pale kwamba baada ya kutoka waingie kwenye kile kituo waweze kukaguliwa au kukabidhi kama ni leseni au ni *export license*, kama ni masuala ya benki yaweze kufanyika pale pale. Kwa hiyo, hicho kituo ni muhimu sana vinginevyo wanaweza wakatoka pale halafu ikaingia mjini. Kwa hiyo, tunataka ikitoka tanzanite pale Mererani basi moja kwa moja inakwenda *airport* kwa ajili ya usafirishaji. Hilo ni suala muhimu sana ambalo ningeomba Waziri aliangalie na liko kwenye mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni ujenzi wa kiwanda cha *ku-add value* kwenye madini yetu ambayo yanapatikana, si tanzanite tu bali hata dhahabu na almasi. Nimeona kwenye hotuba ya Waziri na hotuba ya Waziri wa Viwanda, lakini ni muhimu suala hili likajengwa haraka ili liende sambamba na hizi juhudhi ambazo zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuliongelea ni kwenye Jimbo langu Amani. Kule tuna aidha dhahabu, kwa sababu watu wengi sana wanakwenda kuchimba na imekuwa ni tabu sana kwa sababu wananchi wa Amani, Muheza wanasumbuliwa mara

kwa mara kukamatwa na kufukuzwa. Kule kuna safu za milima ya Sakale, tunaamini kabisa kwamba kwenye hiyo milima ya dhahabu, ndio maana wananchi wanakwenda wanafukuzwa na wanayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kuongea na Naibu Waziri, Mheshimiwa Doto, nafikiri analifanyia kazi. Ni muhimu tupate wataalam waende wakakague ili waweze kuwashauri wananchi wa Muheza waweze kujua kwamba tunachimba dhahabu na iko kiasi gani na waweze kupata leseni kihalali kabisa badala ya kukamatwa kamatwa na kusumbuliwa kama inavyofanyika sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kuna maeneo ambayo watu wameyahodhi, mengi tu na wengine wana leseni na wanalipia lakini hawayafanyii kazi. Wengine wanayaweka kwa lengo ya kuyauza, sasa wanapokuja wawekezaji wanataka kuwekeza inakuwa ni tabu kwa sababu wanakosa ardhi, wanakosa sehemu ya kuwekeza na inaleta matatizo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka niliwahi kuleta wawekezaji na wakaambiwa hakuna sehemu yenye madini, sasa inakuwa ni tabu, ukitaka muone mtu fulani. Sasa ni suala ambalo linatakiwa kuangaliwa. Hili shirika letu la STAMICO lipewe huo uwezo, wawe na maeneo ambayo ni maalum kabisa mtu ambaye anataka kuwekeza anakwenda STAMICO anaambiwa nenda mahali fulani utalikuta hilo eneo, kaangalie, kapime endelea na hiyo kazi. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na maeneo maalum ambayo yataweza kuwasaidia wawekezaji *whether* ni wa hapa nchini au wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ajiandae.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii nyeti sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sekta ya madini mimi nilitarajia ingechangia kiasi kikubwa sana cha pato la Taifa lakini nasikitika kwamba inachangia 4.8% tu wakati madini tunayo mengi sana hapa nchini. Mheshimiwa Waziri itabidi alieleze Bunge hili kwa nini sekta ya madini inachangia kidogo sana katika pato la Taifa? Nadhani madini mengi yanatoroshwa na ndiyo maana sekta hii inachangia kidogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nashauri kwamba maeneo yote ambayo wanachimba madini basi wale wananchi wanufaikie, angalau watengenezewa barabara, wajengewe shule, zahanati, lakini hawanufaiki na jambo lolote wanaachiwa mashimo tu. Wilaya ya Mpwapwa ina madini, kuna rubi eneo la Winza, *copper* eneo la Kata ya Mlembule na Kata ya Matomondo, Vijiji vya Tambi, Mlembule Nnana, Majami, Mwenzele wanachimba sana *copper*. Ukienda kwenye vijiji vile hakuna chochote, barabara haitengenezwi wala hawawasaidii wananchi kwenye suala zima la shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri vilevile hawa wachimbaji wadogo wadogo hebu tuwaangalie, tuwape vifaa vya kisasa, tuwape mikopo ili waweze kuboresha uchimbaji wao kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, wapewe mikopo ili waweze kununua vifaa vya kisasa na si kuchimba kwa kutumia sululu na majembe waweze kuchimba na mitambo ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa umenipa dakika tano, nakushukuru sana, huo ndiyo mchango wangu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni ulinzi wa madini yetu. Kutokana na Serikali kuona ni vyema kulinda madini yetu kwa faida ya wananchi wa Tanzania imeweza kujenga ukuta huko Mererani. Napenda kujua, katika uchimbaji wa madini haiwezekani kutokea mtu kuruka ukuta huo huo chini kwa chini? Kuna mkakati gani wa kuhakikisha wachimbaji hao hawatokezi mbali nje ya ukuta huo? Kama ulinzi huo kwa tanzanite unafaa, je, Serikali ina mpango gani kuhusu migodi mingine ya dhahabu, kwa mfano Buzwagi na kwingineko?

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya ujenzi kodi zake ni za juu kiasi cha kusababisha wananchi kushindwa kugharamia ununuzi wa madini hayo kwa ajili ya ujenzi wa makazi bora na salama kwa wananchi. Napenda kuishauri Serikali kuliangalia hilo kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini ya Liganga na Mchuchuma, napenda kushauri Serikali kuharakisha mchakato wa uchimbaji kwani chuma au nondo tunazojengea sasa hivi siyo imara, zinatokana na vipande chakavu vinavyookotwa na kuyeyushwa, hivyo vinasababisha nyumba nyingi za kawaida kuporomoka na maghorofa pia. Naishauri Serikali kulishughulikia hili kwa ukaribu kwani nondo za nje ni ghali sana na za hapa ni dhaifu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia kwa wananchi wanaopisha wawekezaji, natambua kwamba madini mengi huvumbuliwa na wananchi, hivyo badala ya kuwaondoa wazawa wangeongezewa uwezo kwa kukopeshwa vifaa vya uchimbaji ili waweze kujiongezea pato kwani wawekezaji wanapopewa uwekezaji hawataki

kuwashirikisha wazawa wanawafanya vibarua na kuwanyanya. Niishauri Serikali iliangalie hili kwa faida ya wachimbaji wadogo wadogo kwani wanasaidia mzunguko wa fedha hapa nchini na kukuza uchumi wa nchi tofauti na wawekezaji wanatorosha fedha hii kwa manufaa ya nchi zao.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini Mchuchuma, ni muda mrefu sasa mradi huu wa makaa ya mawe huko Mchuchuma Serikali imekuwa ikiahidi kuanza lakini bado haujaanza. Nataka kujua ni kwa nini ahadi hizi za Serikali hazitekelezeki miaka nenda rudi. Naomba Waziri atakapotoa majumuisho atueleze kwa uhakika ni lini mradi huo wa uchimbaji wa makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa maeneo ya Mchuchuma na Liganga wameondolewa lakini bado hawaijalipwa fidia zao. Naomba Waziri atueleze kwa uhakikia ni lini wananchi hao watalipwa fidia zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaosafirisha kokoto, matofali na mchanga wanasumbuliwa sana na kodi nyingi wakati vifaa hivyo ni vya kuwasaidia wananchi ili wajenge nyumba bora lakini wanabanwa sana na watu wa madini. Naomba kodi zisizo na tija zipunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wachimbaji wadogo wapewe leseni ili waweze kujipatia kipato halali, hasa wachimbaji wadogo wadogo wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo hawana mitaji, Serikali itoe ruzuku kwa wachimbaji hawa ili wachimbe kwa tija na kuweza kuleta

maendeleo ya nchi hii, tofauti na wachimbaji wakubwa wanaonufaisha nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kwa Tume ya Madini kuhusu Maafisa wa Madini wa Mikoa au Wilaya ili kulinda heshima lakini pia mali wanazosimamia, rasilimali ya madini, nashauri, ma-RMO, wote kabla ya kupewa ajira wafanyiwe *vetting*, lakini waapishwe (wale kiapo cha uaminifu), wajaze fomu za maadili ili kujua mali wanazomiliki. Mheshimiwa Rais wetu amewapa heshima kubwa Tume ya Madini kwa kutambua kuwa sekta ya madini itatoa mchango mkubwa katika mfuko wa Taifa.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uzima nami nikaweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Madini. Pili, napenda kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Angellah Kairuki pamoja na Naibu Mawaziri wake, kwa utendaji wao mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ndicho chanzo kikubwa cha mapato katika nchi yetu. Tuna madini mengi sana katika nchi yetu lakini bado nchi yetu haijaongeza pato la Taifa kwa kiasi kikubwa kwa sababu Serikali haijajipanga kudhibiti madini haya. Bado tuna watu wasioitakia mema nchi yetu, wanayatorosha madini yetu na kuyapeleka nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijenge viwanda vyta kuchakata madini ili watu wetu waweze kupata ajira. Tuna vijana wengi ambao hawana ajira, wamekaa vijiweni hawana shughuli ya kufanya. Hivyo, naishauri Serikali iwape mafunzo hawa wachimbaji wadogo wadogo ili na wenzao wakiona hawa vijana wamefanikiwa nao wataacha kukaa vijiweni watajishughulisha na huu uchimbaji na watajikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namalizia kwa kusema kwamba mikataba ya madini iangaliwe upya imepitwa na wakati haileti maslahi kwa Watanzania.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudhi kubwa ambazo zimefanywa lakini bado kuna mambo kadhaa yanahitaji umakini mkubwa wakati wa utekelezaji wake ili kuruhusu sekta hii kukua zaidi na kulipatia Taifa pato kubwa na stahiki. Naomba kushauri mambo muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iongeze bajeti katika Chuo chetu cha Madini pamoja na kuhakikisha kwamba kunakuwa na wataalam wa madini na wanaandaliwa kikamilifu ili kukidhi haja ya kupata pato la kutosha katika sekta ya madini hapa nchini. Je, Wizara inashindwa kuanda wataalam wengi zaidi na kuwa na Maafisa wa Madini angalau kwenye kila tarafa katika nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na *deposit* ya kutosha ya madini, ukiacha yale ya vito vya thamani, lakini yapo pia madini ya chumvi, mchanga, *gypsum* ambayo yametapakaa kila sehemu ya nchi yetu. Namna bora ya kuwa na uratibu mzuri wa sekta hii ni kuwa na maafisa wake katika ngazi za chini za utawala. Sekta ya madini imekuwa *centralised* mno, ikiwa tatizo ni uchache wa wataalam basi dawa yake ni kuanda wataalam zaidi kuititia chuo chetu cha madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu utaratibu wa kukata madini hapa hapa nchini. Jambo hili ni jema sana na likifanywa kwa weledi mkubwa litaipatia nchi mapato makubwa sana. Tatizo ninaloliona hapa ni kwamba hizo mashine zenyewe za kukatia madini hapa nchini ni chache mno na bado zinatumia teknolojia ya zamani kidogo. Jambo hili linasababisha kuwa na foleni kubwa katika maeneo ya kukatia madini na kuongeza kasi ya utoroshaji wa madini hivyo Serikali kupoteza mapato yake mengi. Jambo hili ni jema, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, lakini linahitaji *perfect and gradual changes* na si haraka

haraka tu, bila kuimarisha mifumo yetu ya ndani katika kuliratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kutoipatia fedha za maendeleo Wizara hii. Kiwango cha asilimia 3 pekee cha fedha za maendeleo ni kidogo mno kwa mustakabali wa maendeleo ya sekta hii muhimu. Wizara inapaswa kuwa na mkakati maalum na mahsus wa kuhakikisha kuwa fedha za bajeti zilizopitishwa na Bunge zinapatikana ili sekta hii ijikwamue. Wizara ishirikiane na halmashauri za wilaya nchini katika kuhakikisha kuwa machimbo yake ya madini na mchanga yanatambuliwa na kuratibiwa vizuri ili mapato yake yawe *registered* vizuri na yafike kila sehemu inayohusika kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kuhusu zoezi la utoaji wa leseni za uchimbaji wa madini ya mchanga na *gypsum*. Madini haya yapo maeneo mengi ya nchi yetu, watu wengi wanatamani kufanya biashara ya madini haya, lakini utaratibu wa kupata leseni bado ni mrefu. Tunaomba leseni za uchimbaji wa madini haya ziwe zinapatikana katika ngazi ya halmashauri.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Madini. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya na uzima wa kufikia siku ya leo na kutoa michango yetu katika Wizara hii muhimu kwa uchumi wa Taifa letu na tunafaidika na baraka hii aliyotupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara hii kwa ujumla, kuanzia Waziri wa Madini, Mheshimiwa Angella Kairuki, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Biteko, pamoja na Katibu Mkuu na watendaji na wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mzuri na weledi, hata kama Wizara hii ni mpya lakini wamefanya mambo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani na pongezi hizo, sasa nianze kutoa mchango wangu. Mkoa wa

Morogoro ni miongoni mwa mikoa michache nchini yenye madini mengi na ya kila aina ikiwemo Wilaya ya Morogoro, hususan Morogoro Vijijini, Iliipo Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Miongoni mwa madini yanayopatikana ni *marble*, *ruby*, *dhahabu*, *graphite*, *manganese*, *garnet*, *emerald*, *corundum*, *ulanga*, *limestone*, *urani* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wingi wa madini hayo katika maeneo yetu, lakini bado hayajatunufaisha ipasavyo wananchi wa maeneo hayo. Tumewahamasisha wachimbaji wadogo wadogo kujiunga pamoja ili kutambulika kisheria na kuweza kuaminika na kujipatia mtaji wa pamoja kutoka katika taasisi za fedha na mabenki na kuweza kujipatia vifaa vya kisasa na kuchimba kwa tija na faida kubwa na kujiongezea kipato chao na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo mpaka sasa vikundi hivi havijapata vibali na leseni kutoka Wizarani kwa muda mrefu na kurushwa kama mpira mara waende wilayani, mkoani, Dodoma au Wizarani Dar-es-Salaam. Namuomba Mheshimiwa Waziri wakati anafunga hoja anieleze tatizo ni nini hata inachukua muda mrefu kuvipa vibali na leseni vikundi hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kuhusu Sheria mpya ya Madini ya kutosafirisha nje ya nchi madini ghafi mpaka yawe yameongezwa thamani ndani ya nchi. Pamoja na nia hiyo nzuri kwa Serikali yenye lengo la kuongeza ajira kwa Watanzania, pato la fedha za kigeni, pamoja na kuitangaza nchi yetu nje ya Tanzania katika soko la kimataifa, nashauri Serikali ikaliangalie suala hili kwa upana zaidi kwa sababu, kuna madini mengine kama *ruby* na *marble* yanatumika kutengeneza bidhaa za mwisho tofautitofauti. *Ruby* ukiikata unapunguza thamani na inapatikana sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba ya Kamati ya Madini, lakini pia naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa hakuna shughuli za uchimbaji mdogo mdogo wa madini wala uchimbaji mkubwa. Hii ni kutokana na kutokufanyika kwa utafiti wa kujua aina ya madini yanayoweza kupatikana kule. Naamini kazi ya utafutaji ingefanyika wananchi wa Rukwa wangeweza kunufaika na rasilimali hii muhimu, tafadhalii Wizara fanyeni hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa usimamizi wake muhimu katika eneo hili. Leo tanzanite inaanza kulitangaza Taifa. Udhibiti uliowekwa kwa kujenga wigo utapandisha mapato ya nchi kwa tanzanite.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua, ni lini fedha za makinikia zitapatikana? Je, ndiyo mwisho? Kwa vile Serikali ilituambia hapa kuwa kutapatikana fedha ingetamkwa wananchi wajue ili waone juhudhi za Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kuna mgodi wa makaa ya mawe jimboni kwangu unaitwa Mkomolo unaofanywa na mwekezaji Edenville. Naomba utaratibu ufanyike ili ikiwezekana waweze kufua umeme na uingie kwenye Gridi ya Taifa. Hii itasaidia kuwa na vyanzo tofauti tofauti vya nishati na huenda kwa kufanya hivyo bei ya nishati ya umeme inaweza kupungua na kuimarisha huduma ya upatikanaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rukwa Kusini kuna *helium*, Tanganyika kuna mafuta, tuanze basi kuchimba rasilimali hizi ili kukuza uchumi wa taifa na Mkoa kwa ujumla.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa. Niipongeze Wizara kwa jitihada kubwa za usimamizi wa sekta hii ambayo imeongeza mapato ya Serikali hii, ni jambo la kupongeza sana. Hata hivyo, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ukurasa

wa 25 katika marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017, Majukumu ya Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (*TMAA*) na baadhi ya majukumu ya Kamishna yamehamishiwa Tume ya Madini, hili ni jambo jema pia. Ofisi zilizokuwa za Kanda na Maafisa Madini wakazi zipo chini ya Madini. Aidha, kila Mkoa utakuwa na Afisa Madini Mkazi na kila mgodi mkubwa na wa kati utakuwa na Afisa Mgodi Mkazi. Swali hapa ni kuwa, kwa wachimbaji wadogo wadogo, mfano Jimbo langu la Kilindi je, Serikali haijaona umuhimu wa kuwa na Afisa wa kusimamia? Mheshimiwa Waziri naomba kupata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wadogo wana mchango mkubwa sana katika kuongeza patola Taifa. Nashauri Kamisheni hii ya Madini ihakikishe kuwa katika maeneo yote ya wachimbaji wadogo wadogo pawepo na utaratibu wa Afisa Madini kwani watasaldia kutoa elimu na kutatua migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuimarisha usimamizi wa mapato ya Serikali, kwa mfano katika hotuba hii ukurasa wa 72 inaonesha makusanyo katika Wilaya ya Handeni hadi Machi 2018 ambao wanasmamia na Kilindi waliweza kukusanya Sh.191,177,340 tu. Hiki ni kiasi kidogo sana na hii imesababishwa na usimamizi mdogo na pengine baadhi ya watumishi kukosa uaminifu kwa kushirikiana na wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara kuwa, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Madini waone umuhimu wa kuleta Maafisa Madini katika maeneo ambayo yana wachimbaji wadogo wadogo. Hivi leo Afisa Madini yupo Tanga ambako kiukweli hakuna shughuli za uchimbaji, Serikali itakuwa na dhamira ya kusimamia mapato kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuishauri Wizara kuzingatia ushauri wote uliotolewa na Kamati ya Bunge ya

Nishati na Madini kwani pamoja na kuwa nchi yetu kuwa ya nne (4) Barani Afrika kwa kuwa na aina nyingi za madini, lakini sekta hii haijapewa msukumo wa kutosha ili kuleta tija inayokusudiwa. Bado mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa haulingani na uhalisia. Hivyo basi, Serikali ikafanye uwekezaji wa kutosha katika sekta ya madini ikishirikisha wawekezaji wenye mitaji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, machimbo ya Kitowelo kwenye Kata ya Lilombe ni ya muda mrefu sana lakini hadi leo Halmashauri hajianufaika na chochote. Hii ni kwa sababu soko la madini hayo liko Tunduru Mkoani Ruvuma, hivyo wachimbaji huenda Tunduru bila kupitia kwenye kata au kijiji, hivyo kijiji kukosa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo kuna kampuni ya utafutaji wa madini, kampuni ya GWENA, kampuni hii mkataba wake haujulikani wala haina ushirikiano na vijiji uchimbaji huo unakofanyika kwani elimu ni ndogo sana kwa jamii hivyo kushindwa kusimamia vyema utafutaji huu wa madini. Hivyo Wizara sasa ione umuhimu wa kuwa na Afisa Madini kila halmashauri kwani hapa nchini hakuna halmashauri ambayo haifanyi biashara ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa madini aina ya *green garnet* katika Wilaya ya Ruangwa na Liwale. Serikali haijafanya utangazaji wa kutosha ili kupata wawekezaji katika uchimbaji wa *green garnet*, hivyo kukosa tija iliyokusudia. Hata hivyo, naishauri Serikali kuangalia upya leseni za utafutaji wa madini kwani wapo wenye hizi leseni wanazitumia kufanya uchimbaji wa madini na si utafutaji au utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali haijawekeza vya kutosha kwa wachimbaji wadogo wadogo. Sekta hii imeshindwa kuongeza ajira nchini kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo hawajapewa mitaji ili kupata vifaa na kuboresha mazingira ya kazi zao. Sheria vilevile ikaangaliwe ili kuwe na uwanja sawa kati ya wachimbaji wakubwa na

wadogo kwani sasa wachimbaji wananyanyasika sana katika tasnia hii ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Sheria ya Madini ikaangaliwe ili kufanya madini yanayotumika katika ujenzi wa barabara ikiwezekana tozo hizi na ushuru mbalimbali zikafutwa ili kupunguza gharama za ujenzi wa barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kupatiwa majina ya wachimbaji na watafutaji wa madini walioko katika Wilaya ya Liwale. Kwani hadi sasa shughuli hiyo hufanywa holela, hata Mkurugenzi wa Halmashauri hana hiyo takwimu, hivyo hata yeye hajui chochote. Jambo hili haliwezi kuwa sawa kwa kuwa kazi hizi zimekuwa zikifanywa kwenye eneo lake la utawala. Bila kusahau *status* ya Kampuni ya GWENA na machimbo ya Kitowelo.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mungu kunijalia afya njema na kuweza kuchangia katika Wizara ya Madini. Niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Tanga kwa kunituma kuja kuwasemea katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu marehemu Mwalimu Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Jimbo la Buyungu Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe masikitiko yangu kidogo kwa kuwa leo ni siku ya Bajeti ya Wizara ya Madini lakini sijawaona wawakilishi wa wachimbaji wadogo wadogo wa Tanzania, hususan Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini Wanawake na Chama cha Wachimbaji Wadogowadogo wa Madini Tanzania. Ushauri wangu kwa Serikali, katika bajeti ya mwakani, Wizara itoe mwaliko kwa wadau wa madini, wachimbaji wadogo, vyama vyao na kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa wachimbaji wadogo na Serikali. Wachimbaji wadogo duniani kote ndiyo wagunduzi wa kwanza wa madini na baadaye ndipo

hupatikana wachimbaji wakubwa (wawekezaji) na kuingia mikataba na Serikali na kulipa kodi za Serikali zinazojulikana kama mrabaha. Niwape pole kwa kuwa wanagundua madini kisha Serikali wanakuja kuwafukuza na kuwaweka wawekezaji wageni (matajiri). Jambo hili si sawa kwa kuwa wachimbaji ndiyo wagunduzi wa kwanza, Serikali ingewathamini na wageni wangewathamini, ikibidi wenye migodi waingie ubia na wenyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali badala ya kuwapelekea *FFU* (*Field Force Unit*) na kuwafukuza kwa mabomu ya machozi (*tear gas*), iwawekee utaratibu wa kuwaelimisha na waweze kuona madini ni mali ya Taifa. Vilevile wachimbaji wadogo wapewe ajira katika kampuni za uwekezaji kutoka nje na wachimbaji wapewe mikopo na benki. Watananzania wazawa wakiajiriwa wanaweza kuwa ni askari kanzu (*intelligence unit*) kujua wawekezaji wabaya (*bad investors*) ambao wanatorosha madini yetu na kuweza kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya tanzanite na madini ya vito. Tanzania tumejaliwa madini ya thamani ya aina nyingi mno kama vile tanzanite yanayopatikana Tanzania tu, ruby, sapphire (pink, white and red), rhodolite, alexandrite, rose, change colour, green garnet, red garnet, green tourmaline, ammolite, moonstones. Madini yote haya yana thamani na ni ajira kwa vijana wa Kitanzania, endapo patafanyika mipango ya makusudi ya kuanzisha viwanda vya kuchakata madini (*mines cater center*). Pia madini haya tungepata taarifa zake kwamba kila aina imeingiza/ inaingiza kiasi gani kwa mwaka na iwepo *data base* ya *precious stone*.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya tanzanite yanapatika nchini mwetu tu, duniani kote hakuna. Hivyo ni vyema yakafanyiwa matangazo ya kutosha kwani itakuwa ndiyo *symbol* ya nchi yetu kama ilivyo *Mount Kilimanjaro* kwa kuwa dunia nzima ipo Kilimanjaro moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, majanga katika uchimbaji madini. Katika migodi mikubwa na midogo duniani kuna changamoto kubwa ya ajali za moto, kufukiwa na vifusi, kuishiwa hewa ya *oxygen*, tetemeko la ardhi na mafuriko. Katika nchi za wenzetu kwa kuwa madini ni uchumi wamewekeza fedha nyingi lakini zipo *rescue teams* za uhakika ili kuweza kuokoa wachimbaji pale inapotokea dharura za ajali kama nilivyozitaja. Nashauri Serikali iweke utaratibu wa kuwa na *rescue teams* katika migodi yote mikubwa na midogo nchini Tanzania. Serikali inunue *ambulance/helicopter* ambayo itasaidia kuokoa maisha ya wachimbaji kwa kuwahahaha watakaokutwa na ajali katika hospital zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini madini yanatoroshwa? Madini yanatoroshwa kwa sababu mbalimbali kama: Foleni zinazosababishwa na uchache/muda/teknolojia ndogo zinazosababisha wafanyabiashara wa madini kuyatorosha nje kwa kuwa ukataji unatumia muda mwingi kukata madini machache; *technology* iliyopo Tanzania ni ya kizamani na pia imepitwa na wakati; na mashine (*mineral cutters machines*) zipo chache mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nashauri Serikali yafuatayo:-

(i) Iwekeze katika vyuo vya madini ili vyuo vizalishe wataalam watakaosaidia wachimbaji wadogo.

(ii) Ianzishe *course* za masomo ya ukataji wa madini na aina za madini katika vyuo vyetu vya VETA. Kwa mfano, katika ziara ya Kamati ya PAC Shinyanga tulikutu *course* ya ukataji madini katika Chuo cha VETA Shinyanga. Ada ya *course* hizi ziwe kiwango cha chini kuwavutia wanafunzi.

(iii) Mashine za ukataji madini ziwekewe kodi ndogo ili kufanya bei ya ukataji iwe ndogo na kuweza kuongeza thamani ya madini yetu baada ya kukatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki kutowaamini wachimbaji. Benki na taasisi za fedha haziwaamini wachimbaji wadogo kwa kuwa haziwakopeshi na ama kuna masharti magumu mno. Nashauri Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Iweke mpango wa kuwakopesha vifaa (mitambo) wachimbaji wadogo kwa ajili ya uchimbaji badala ya fedha.

(ii) Mpango wa kuwawezesha wachimbaji wadogo US\$50,000 (Sh.100,000,000) hadi US\$100 (Sh.200,000,000) uwekwe wazi na vigezo vinavyotumika, wachimbaji waelimishwe ili wajue na kuweza kufaidika na mpango huu.

(iii) Benki zote zipewe maelekezo na namna ya kuwakopesha wachimbaji wadogo mitambo/fedha na uwepo uwazi.

(iv) Wizara itoe takwimu za wachimbaji wadogo wote waliowezeshwa na maeneo walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya ujenzi/viwandani. Wizara katika taarifa yake haijatoa takwimu za madini ya uranium yanayotumika katika utengenezaji wa silaha za *nuclear*. Naomba tupatiwe taarifa kwa hapa nchini yapo maeneo gani na yapo kwa ujazo wa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya bati, ni madini ambayo Serikali kama ingetilia maanani kwa kununua mtambo wa kuchakata bati, wananchi wetu wasingekuwa na sababu ya kuishi katika nyumba za nyasi, tembe na bei isingekuwa kubwa. Naiomba Serikali inunue mtambo wa kuchakata bati kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara katika maeneo yenye madini katika Jiji na Mkoa wa Tanga katika maeneo yafuatayo ili kutambua kero za wachimbaji.

Na.	Eneo la Mgodi	Sehemu Ulipo	Aina ya Madini
1	Kalalani / Kigwase	Tarafa Daluni - Korogwe	Madini ya Vito
2	Ng'ombeni, Umba	"	
3	Amboni	Kata ya Mzizima - Tanga	Kokoto/ Mawe/ Chokaa
4	Maweni	Kata ya Maweni Jiji la Tanga	Kokoto na Mawe ya ujenzi

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia hoja ya hotuba ya Wizara ya Madini. Namshukuru Mungu kwa kibali hiki. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Angellah Jasmine Kairuki kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Madini na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Biteko na Mheshimiwa Nyongo. Nawapongeza pia kwa hotuba nzuri iliyozingatia masuala yote muhimu pamoja na taarifa za ziada walizotupatia kwenye makabrasha maalum na maonesho yallyoletwa kwenye viwanja vya Bunge ambayo yanetuungezea uelewa wetu juu ya sekta hii muhimu sana kwa uchumi, lakini pia kutuwezesha kutambua changamoto zake na nini kinafanyika kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa hatua madhubuti alizochukua kuhakikisha kunakuwa na usimamizi na udhibiti mzuri wa rasilimali za sekta hii kwa kuunda Kamati za kukagua makinikia yanayotokana na uchimbaji wa madini na vito na hatimaye kuitishaa sheria za kimapinduzi zinazoliwezesha Taifa kuipitilia upya mikataba yote ya madini na vito ambayo ilikuwa ina vipengele vyenye kutiliwa mashaka ili irekebishwe na Taifa lipate mapato stahiki kutokana na sekta hii ambayo kwa muda mrefu Taifa limekuwa likipoteza mapato mengi sana. Tunamwomba Rais zoezi hili lifanywe kwa rasilimali zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu sasa nizungumzie suala la migodi ya makaa ya mawe ambayo yanapatikana maeneo ya Kiwira Wilaya ya lleje, Ludewa, Ruvuma, Mbinga na Songea. Makaa ya Mawe ya Ngaka, Mbinga, Ruvuma yana ubora wa juu zaidi duniani. Mgodi huo una zaidi ya tani milioni 400 za makaa ya mawe na yanaweza kuchimbwa

kwa miaka 100. Kwa hivyo, ni rasilimali ya uhakika na kutegemewa sana katika mkakati wa kuzalisha chuma kwa ajili ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Serikali haitilii mkazo mradi huu ambao utafungua Taifa kiuchumi na kiviwanda? Hili ni eneo ambalo Serikali itakuwa na kila sababu ya kuingia ubia mkubwa na wawekezaji wa sekta binafsi na hata kuchukua mkopo ili kuendeleza migodi hii yenye kuleta faida kubwa na mapato makubwa kwa Taifa na kuongeza umeme kwa asilimia 40 kama takwimu za dunia zinavyoonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, makaa ya mawe ni nishati kubwa kwa kutengeneza *cement*, kuzalisha karatasi na kwenye viwanda vya nguo na bidhaa nyininge nydingi za viwandani pamoja na uzalishaji wa umeme. Hii pia itaokoa fedha ya kigeni iliyokuwa ikitumika kuagiza makaa ya mawe toka Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *STAMICO* ndiyo iliyokabidhiwa Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira na taarifa zilizowasilishwa kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 45 imainisha kwamba *STAMICO*imeanza rasmi kuuza makaa ya mawe yanayozalishwa katika Mgodi wa Kabulo uliopo lleje – Songwe kwa matumizi ya watumiaji wa viwanda wa ndani ikiwemo viwanda vya saruji na nguo. Uzalishaji wa majaribio ulioanza kwenye Kijiji cha Kapeta, lleje tangu Aprili 30, 2017 na mpaka sasa imezalisha tani 6,197. Kiasi gani cha makaa haya yameshanunuliwa na lleje kama Wilaya ina gawio la asilimia ngapi kutokana na mauzo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lleje inahitaji daraja la kwenye Mto Mwalisi linalounganisha lleje na Mgodi wa Kiwira ili ipunguze gharama za kusafirisha makaa kupitia Kyela na kuwezesha makaa hayo kuhifadhiwa lleje na villevile kupitishwa lleje wakati wa kupeleka kwenye viwanda vya *cement*na hata vya nguo vitakapoanza. Tunaomba Wizara itenye bajeti ndogo kujenga daraja hili fupi la kilomita 7 kuokoa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi napenda kuona Mgodi wa Kiwira na Kabulo ungeendelezwa sasa na kuajiri watu 7,000 wanaotegemewa huku ingeongeza mapato lleje na Songwe kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri atueleze mikataba gani ipo sasa kuendesha Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira na ile ya katiba ya Halmashauri ya lleje na *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo ni sehemu muhimu katika tasnia hii ya madini na wanachangia kwa kiasi kikubwa kwenye soko la ajira na kuliletea mapato Taifa na kuondoa umaskini. Wachimbaji wadogo wathaminiwe na kuwezeshwa. Maeneo wanayochimba wapewe leseni kwenye maeneo yaliyokwishapimwa rasmi na *GSI* ili wasifanye uchimbaji wa kuhamahama unaoharibu mazingira na usiokuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la kutumia Tanzania kuwa kitovu cha vito na madini yetu ni zuri na linalohitaji kufanyiwa kazi kwa haraka. Kila eneo lenye uzalishaji wa vito lijengwe eneo la kucharanga vito na kuuza vito na mikufu, pete na vitu vya thamani. Vijana wetu wapewe mafunzo nje na ndani ya nchi kwenye usonara, *design* na wasaidiwe kupata vifaa na mitaji ya kujidendeza kiajira na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la migogoro ya maeneo ya wachimbaji wa tanzanite wadogo na wawekezaji wakubwa lifanyiwe kazi ili lisije umiza wawekezaji wadogo. Iko haja ya Wizara kuwa na kanzi data ya kila aina za madini na vito na kiasi kilichopo na thamani yake ili ituwezeshe kujua utajiri tulionao kama nchi na jinsi ya kuhakikisha kuwa inasaidia maendeleo ya kiuchumi ya Watanzania kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa za Serikali kusaidia wachimbaji wadogo, bado liko tatizo kubwa la watoto wanaofanya kazi kwenye migodi na ambao wanatumia zebaki kuchambua dhahabu na hii ni sumu ambayo wanaishika na inapochomwa pia inaingia kwenye mazingira. Watoto hawa vilevile huingia kwenye mashimo

ya migodi iliyochimbwa kienyeji bila kinga zozote na hutumia kamba tu kuingia ndani ya mgodi na hii ni hatari sana kwa maisha yao. Licha ya kuwa wanakosa elimu, vilevile watoto wako kwenye kuvunja kokoto na kwenye vito Mererani. Wizara ishirikiane na Wizara ya Ajira, Mazingira, Elimu, Ustawi wa Jamii kuwaondoa watoto migodini.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na kunipa fursa ya kuchangia siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu ambaye ameamua kuleta mapinduzi kwenye sekta hii ya madini. Tunampongeza kuanzisha Wizara kamili ya Madini na Wizara ya Nishati. Kote sasa tunapata ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze wote, Waziri Mheshimiwa Angella Kairuki, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Doto pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya. Pia pongezi kubwa kwa Prof. Kikula kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Madini pamoja na *team* nzima ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia kwanza kwa kushauri Kituo cha Mafunzo cha Arusha (*TGC*), kiwezeshwe sana kwa vifaa vya kufundishia. Wanahitaji mashine 100 za kufundishia na sasa wanazo 45 tu. Pia nipongeze kwa kuwa na mitaala ya kufundishia kozi ya Diploma itakayoanza Agosti, 2018. Nashauri kuwe na *short course (Certificate in Lapidary)* ya kuchonga vito. Ni kozi ya miezi sita kote duniani, wala haihitaji msomi, hata mtu asiyejua kusoma, anaweza kuwa mchongaji mzuri. Tukiwa na mashine 100 za mafunzo, tunaweza kuzalisha wataalam mia 400 kwa miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashauri pia kwenye leseni za utafiti (*Prospecting License*) au leseni kubwa, paruhusiwe kuwa na leseni za madini ya ujenzi kama

mchanga, mawe, moramu na marumaru. Kwa sasa pamoja na kuwa tulirekebisha sheria kuruhusu kuwepo leseni hizo haifuatwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nashauri katika madini ya chumvi, Serikali iangalie namna ya kupunguza kama siyo kuondoa kodi, tozo na ada kubwa wanatozwa tofauti na thamani ya madini hayo. Leo hii wanatozwa sawa na madini yenye thamani kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, nashauri Wizara itupe tafsiri ya neno “*raw mineral*” leo hii kila mtaalam ana tafsiri yake ili wakati wa *ku-export* madini suala la kisheria ya kodi lisiletet tatizo. Pia naomba nishauri Serikali ikae kama Serikali moja na siyo Wizara ya Madini tu, kufanya juhudzi za pamoja ya kuboresha mazingira ya kufanya Tanzania hususan Arusha kuwa kitovu cha ubora katika biashara ya vito Afrika. Tayari tulianza vizuri na tulianza kuwa maarufu lakini sera za kikodi na usumbufu mwingine ulifanya tupoteze sifa na kudorora kwa biashara hiyo Arusha na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizotuzunguka pamoja na zingine nje ya hapo wenye madini mengi walishaanza kuzoea kuja Tanzania kuuza madini yao katika mnada wetu. Walikuwa wanakumbana na usumbufu wa *TRA* kwenye ushuru wa *import duty*, *VAT* na pia madini ambayo hayakuuzwa ilikuwa ni usumbufu kurudisha kwao. Tofauti na nchi zingine kama Thailand, Belgium, India na kadhalika ambazo hawatozi kodi ya *import* na *VAT*. Pia wananaufaika kutokana na biashara hizo katika sekta zingine kama katika *service industry*, hoteli, chakula, usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie namna ya kuondoa *VAT* kwenye madini yanayouzwa ndani ya nchi kama dhahabu, fedha, vito ili biashara hii ikue na magendo katika madini yaishe. Sisi kama Tanzania hatupangi bei ya madini kama dhahabu na fedha pamoja na vito (*VAT on local sales of gemstone and jewellery*), leo hii Dubai inatoza 5% ya mrabaha kwenye dhahabu, Tanzania ni asilimia 18 *VAT* pamoja na ada na tozo zingine. Nashauri tuweke mrabaha

wa hata 7% ili biashara ihalalishwe na Serikali ipate mapato na madini yetu yasitoroshwe.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi nyngi kwa Waziri na Naibu Mawaziri kwa utendaji na ushirikiano wao kufanikisha malengo ya Serikali. Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais Joseph Pombe Magufuli kwa uthubutu wake wa kulinda maliasili za Taifa ili nchi na vizazi vijavyo viweze kufaidi. Mheshimiwa Rais amefanya mabadiliko katika Sheria za Madini pia sheria mpya za *Permanent Sovereignty Unconscionable Terms* ambazo zitasaidia kupitia mikataba isiyokuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambao wanahangaika sana kutafuta kipato. Hivyo, Serikali ifanye mpango wa kuwa na maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na watambuliwe kwa kusajiliwa na wapewe leseni za bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilisimamisha utoaji wa ruzuku kwa wachimbaji wadogo miaka miwili imepita. Fedha hizo zilikuwa zinasaidia wananchi na kuwainua kiuchumi. Hivyo, tunaomba Serikali irudishe ruzuku hiyo na kuweka mpango mzuri ambao utanufaisha wachimbaji wadogo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufadhili wa uchimbaji bora kwa vituo saba. Tangu 2016 Serikali ilitoa taarifa kuwa kutakuwa na vituo saba vya mfano ili kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo na moja ya kituo hicho ni Ibindi, Jimbo la Nsimbo, Wilaya ya Mpanda, Katavi. Tunaomba kauli ya Serikali mpango huu wa *World Bank* utafanikiwa lini? Je, Serikali ina mkakati gani wa kuuendeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, *service levy* za *councils* na soko huru. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, kila aina ya biashara katika Halmashauri wanatakiwa kulipa *service levy*, lakini changamoto ili yopo ni usiri wa mauzo kwa wafanyabiashara wa madini ambapo huwa hakuna uwazi katika kununua na kuuza inapelekea Serikali kupoteza

mapato. Hivyo basi, nashauri Serikali ianzishe soko huru kwa maeneo yote ili Serikali ipate mapato pia Serikali za Mitaa zipate *service levy*. Halmashauri ya Nsimbo ina wachimbaji wadogo wengi 98% ambao hawana uwazi na Halmashauri inapoteza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji maeneo kwa kigezo cha aina ya madini. Mkao wa Katavi maeneo mengi yana madini aina tofauti tofauti, ukanda wa Wilaya Tanganyika ndio umepangwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo lakini ukanda huo zaidi ni madini ya shaba ndiyo yanapatikana kwa wingi lakini Wilaya ya Mpanda, Jimbo la Nsimbo ndiyo kuna dhahabu, hivyo eneo hilo linafaa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha sheria, sera na kanuni ili kufikia malengo. Serikali iendelee kuboresha sheria, sera na kanuni kwa kuzingatia pande zote za kulinda maliasili na uwekezaji kuendelea kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iongeze kasi katika kutekeleza uwekezaji wa mashine ya uchenjuaji (*smelter*) ili kuokoa upotevu wa maliasili na kuongeza ajira nchini. Waziri atoe taarifa uwekezaji wa *smelter* umefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kwa nafasi.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, madini ni chanzo kizuri cha mapato kwa Taifa letu. Pongezi kwa Rais Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Mawaziri wote na Makatibu wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Ifungue Ofisi za Utafiti kila Wilaya ili kufanya utafiti maeneo yote yenye viashiria vyta madini.

- (ii) Vibali vitolewe kwa watu wenye mitaji ya kutosha.
- (iii) Usimamizi na ufuatiliaji wa walipa kodi katika sekta ya madini uboreshwa.
- (iv) Elimu kwa wachimbaji wadogo wadogo itolewe na vifaa vyta kuchimbia wachimbaji wadogo wapewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni baadhi ya ushauri wangu kwa Serikali ili madini yetu yawe na faida kwa Taifa letu. Naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kufika mahali hapa nami kushiriki katika kikao hiki cha bajeti ya Wizara ya Madini ya mwaka 2018/2019. Naipongeza Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri itakayokwenda kuboresha sekta hii yenye changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuimarisha usimamizi katika sekta ya madini ili kuwezesha sekta hiyo kuchangia kikamilifu katika uchumi wa nchi, kuongeza mapato ya Serikali na kuzalisha ajira. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kukusanya taarifa za uzalishaji wa madini, kuimarisha ukaguzi wa uzalishaji na mauzo kwenye migodi mikubwa na midogo na kufuatilia ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha naipongeza kwa zoezi la ukaguzi lililowezesha kukamatwa kwa madini yaliyokuwa yakitoroshwa yenye thamani ya Dola za Marekani takribani 898,523 na shilingi milioni 557. Kwa taarifa za Serikali, ni kwamba katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 maduhuli ya Serikali yaliyokusanya kutoka sekta ya madini yalifilia shilingi bilioni 180.4. Pamoja na mambo mengine, mafanikio hayo yametokana na usimamizi makini katika sekta ya madini na uamuzi wa Serikali kufungua soko la tanzanite

nchini. Hatua hizi ni nzuri na ziwe endelevu kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeimarisha soko la madini nchini kwa kuhakikisha kuwa madini yanauzwa kwa ushindani ili kuyaongeza thamani na kulipatia Taifa fedha kwa kupitia kodi. Hata hivyo, itakumbukwa kwamba tarehe 20 Septemba, 2017, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza ujengwe ukuta katika eneo linalozunguka Mgodi wa Tanzanite uliopo Mererani ili kuimarisha ulinzi na kudhibiti utoroshaji wa madini hayo, ujenzi wa ukuta huo wenge mzunguko wa kilomita 24.5 umekamilika. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza viongozi na watendaji wote walioshiriki katika ujenzi huo, kwani umesaidia sasa madini yetu ambayo ni ya pekee kwa kuwa yanapatikana Tanzania tu kuwa salama ukililinganisha na hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali kwa kuja na mkakati katika mwaka 2018/2019, kuwa Serikali itaendelea kuwajengea uwezo wazawa ili washiriki kikamilifu katika sekta ya madini, kwani uwezeshaji huo utakwenda sambamba na utoaji mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu teknolojia mbadala ya uchenjuaji dhahabu kwa lengo la kupunguza athari za mazingira na maafa katika maeneo ya migodi. Hatua hizi zote hapo juu ni za kuipongeza kwani ni hatua muhimu kwa kuhakikisha sekta hii muhimu inaliingizia pato Taifa na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kwenye mafanikio hapakosi changamoto na changamoto hizo huzichukua kama fursa ili kuboresha maeneo husika. Bado tuna changamoto kubwa hasa kwa wachimbaji wadogo kutopata elimu ya kutosha na kufanya uchimbaji wenge tija na usioleta athari za kimazingira. Wachimbaji hawa wanapaswa kupewa elimu ili uchimbaji wao ulete tija na Serikali iweze kukusanya kodi zake. Naishauri Serikali kuwapa elimu wachimbaji wadogo kama nilivyosema hapo awali katika kuwapa elimu ya teknolojia mbadala ya uchenjuaji dhahabu na pia iwape elimu ya uchimbaji wenge tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali inapaswa sasa kuwaangalia hawa wachimbaji wadogo pindi wanapoagiza vifaa kazi namna ya kuwapunguzia kodi. Kufanya hivyo kutawasaidia kufanya kazi kisasa na kuongeza uzalishaji na kupelekea Serikali kupata kodi yake ipasavyo bila shaka yoyote. Aidha, naishauri Serikali kuendelea kusimamia ipasavyo rasilimali zetu zote katika sekta hii kwani tumeshuhudia mambo mengi ya hovyo yakifanywa na baadhi ya watendaji wetu wasiokuwa waaminifu wakishirikiana na baadhi ya wawekezaji ambao nao sio waaminifu kutudidimiza na kujipatia faida kubwa huku Taifa likiambulia patupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwepo na changamoto ya wachimbaji wadogo kuondolewa katika maeneo yao na kutokupewa maeneo mbadala. Ni wajibu wa Serikali kuwalinda wachimbaji wadogo kwani sekta hiyo imetoa ajira kwa watu wetu katika maeneo husika ya machimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ya migogoro baina ya wawekezaji na wachimbaji wadogo, ni vema ikaangaliwa na kutatuliwa kwa wakati ili pande zote mbili husika wakaendelea na majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Nimechangia kwa kuongea, hata hivyo ipo hoja nyingine muhimu ambayo sikuzungumza kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Jemedari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ni kuona sekta ya madini inatoa mchango stahiki katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma hii ni nzuri lakini takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa Serikali haina wathamini

(*Government Valuer*) wa madini wa kutosha na hali hii imesababisha wawekezaji na wachimbaji wa madini kutoa takwimu za thamani ya madini kadri wanavyoona inafaa. Nashauri Serikali isomeshe wathamini wa kutosha na naomba wakati wa kuhitimisha hoja Bunge lielezwe hatua zilizochukuliwa katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua ni lini gesi ya *helium* iliyogunduliwa katika Ziwa Rukwa itaanza kuchimbwa. Tunaambiwa gesi hiyo ni adimu sana duniani na ina thamani kubwa. Ni sababu zipi zinatufanya tuchelewewe kuanza kuichimba?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. LOESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kutoa pongezi kwa hotuba nzuri inayogusa maisha ya Watanzania hasa walioko kwenye sekta ya madini. Hongera sana Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Madini bila kuwasahau Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote wawili na watendaji wote wa Serikali. Hotuba imewatendea haki wananchi wa Jimbo la Busanda hasa wachimbaji wadogo wa madini wa maeneo yote ya Nyarugusu, Nyamyeye, Lwamgasa, Kaseme na Magenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 49 na 50 hotuba imeongea bayana juu ya ujenzi wa mgodi wa mfano katika eneo la Lwamgasa. Tunashukuru sana kwa hatua iliyofikia ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napongeza kwa mpango wa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia upya mkataba wa ubia kati ya *STAMICO* na Kampuni ya *TANZAM* 2000. Naunga mkono

sababu za Wizara kuchukua hatua maana ni kweli kabisa kampuni hii imeanza kufanya kazi kwa muda mrefu, miaka nane sasa lakini hakuna uzalishaji wowote. Jambo hili limekuwa kero kubwa kwa wananchi wa maeneo husika maana maeneo mengi ya wananchi yamechukuliwa na mpaka sasa hawajalipwa fidia. Naomba Wizara ifuatilie suala hili kwani ni kinyume na taratibu na sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa kipekee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi na juhudini kubwa anayoifanya ya kusimamia na kulinda rasilimali za nchi yetu ya Tanzania. Kwa kipindi cha miezi michache ya utekelezaji matokeo mazuri yameonekana. Hongera sana Mheshimiwa Rais, Mwenyezi Mungu akulinde wewe na Serikali yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Madini, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, taasisi zote zilizo katika sekta hii ya madini na watendaji wote wa Wizara hii ambao wameshiriki katika kufanikisha kazi nzuri. Kipekee, niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Madini na Manaibu wake wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii na kufuatilia kwa ukaribu sana maeneo mengi ya migodi na kutatua changamoto zilizoko katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nichangie mambo au maoni machache kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itafute uwezekano wa kuainisha aina zote za madini zinazopatikana hapa nchini na ionyeshe faida zake na masoko yake nje ya nchi. Pia kuwe na maonesho ya mara kwa mara ya uelewa na kuweza kuchukua fursa ambazo zinaweza kutoa ajira nyingi zaidi kwa vijana kwa kuza vito na madini mengine ya ujenzi na malighafi na kadhalika.

(ii) Naomba Serikali itoe mafunzo ya vitendo kwa wachimbaji wadogo wadogo na wa kati ili waweze kuongeza ujuzi wa kuchenjua madini ya aina mbalimbali.

(iii) *STAMICO* ijengewe uwezo kwa kupatiwa fedha za kutosha ili iweze kujiendesha kwa ufanisi na tija.

(iv) Ufanyike uhakiki/sensa kwa wachimbaji wote wadogo wadogo ili Serikali na Shirikisho la *FEMATA* waweweze kuwatambua kwa kuwapatia vitambulisho maalum. Hii itasaidia kuzuia watu wasio Watanzania kuvamia migodi yetu bila utaratibu wa kisheria na wakati mwiningine baadhi yao hufanya uhalifu na kukimbilia nchi jirani bila kujulikana.

(v) Madini ya ujenzi kama kokoto, *gypsum*, madini ya kutengeneza marumaru (*tiles*), changa na kadhalika. Migodi ya aina hii inapaswa kusimamiwa kwa ukamilifu kama yalivyo madini mengine ikizingatiwa matumizi yake ni makubwa mno. Migodi hii hypoteza kiasi kikubwa cha fedha za Serikali kwa kutokuwa na utaratibu mzuri wa uchimbaji na usimamizi pia hata utozaji wa ushuru katika madini hayo.

(vi) Viongozi wa ngazi za aina zote wawe na lugha zinazoleta au kuashiria utaifa kuliko kutumia lugha kibaguzi kwa kutumia madini, mazao, vitega uchumi na kadhalika. Mara nyingine baadhi ya viongozi hutoa lugha ya kusema madini haya ni ya mkoa fulani hayawezi kuuzwa mkoa fulani au mazao fulani yauzwe kuititia bandari fulani. Lugha hizi zinabomoa nchi na ni hatari sana kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100%.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoiongoza nchi yetu na kwa hatua kubwa alioifanya katika kurekebisha mifumo mingi ya Wizara hii na sekta ya madini kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Madini na Naibu wake wote wawili kwa jinsi wanavyotendea haki nafasi zao pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa Wizara hii ni kama ifuatavyo:-

(a) Tunaomba sana Serikali itazame upya mikataba ya uchimbaji wa madini kote nchini ili kuona ni kwa namna gani nchi yetu inanufaika kupitia rasilimali hii ya asili kutoka kwa Mungu.

(b) Serikali itazame mpango wa kuwasomesha wataalam wabobezi wa sekta hii.

(c) Serikali ifanye mpango wa kutumia wataalam watakaobaini maeneo yalipo madini nchini hasa katika maeneo ya wachimbaji wadogo kote nchini.

(d) Kwa kuwa wachimbaji wadogo kwa sasa wanachimba kwa kubahatisha basi Serikali yetu itumie wataalam wake ili kurahisishia wachimbaji hao wadogo nchini kutumia njia bora.

(e) Kwa kuwa maeneo mengi nchini yanasemekana kuwa na leseni na kwa kuwa maeneo hayo yanashikiliwa na watu hao ambao hawachangii Taifa letu mapato ya uhakika basi Serikali ifanye mapitio au tathmini ili kuona njia bora na zenye manufaa katika kurekebisha suala hili.

(f) Nimuombe Mheshimiwa Waziri afanye ziara katika Jimbo la Mbulu Mjini kwenye machimbo ya Tsawa, Kata ya Gehandu, Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho natanguliza shukurani zangu na naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuipongeza hotuba ya Waziri wa Madini. Pia nwapongeza Waziri na Naibu wote wa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri wangu kidogo kuhusiana na upotevu mkubwa wa mapato yatokanayo na madini ya dhahabu. Mfano, kuna wachimbaji wadogo Wilayani Nyang'hwale ambao wanachimba na kupata dhahabu bila ya kulipa mapato ya Serikali. Sababu kuu ni kutowapatia leseni ya uchimbaji au kutowatambua lakini yako maeneo mengi yanayochimbwa kama Kijiji cha Chibaranga, Ifugandi, Bululu, Isonda, Nundu, Nyamalapa, Iyenze, Ujulu, Isekelyugwa, Nyijundu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, kwa kuwa Wilaya ya Nyang'hwale haina maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Maeneo nilliyoyataja yapimwe na kutolewa leseni ili Serikali iweze kukusanya mapato kirahisi pia kuwaepusha wachimbaji kusumbuliwa na kuhamahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudzi zote Serikali inazochukua za kudhibiti utoroshaji wa madini yetu kama uimarishaji wa mifumo ya ulinzi sehemu mbalimbali zenye madini; uboreshaji wa mikataba mbalimbali ya madini na sheria; na uboreshaji na kuinua biashara ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa ukuta wa Mererani ambao umesaidia kudhibiti madini ya tanzanite, ila *CCTV cameras* ijengwe kuanzia sehemu ya ulipuaji; kituo kimoja kitakachokidhi mambo yote kwa pamoja kijengwe hapohapo karibu na mlango wa kutokea, pawepo na benki na sekta zote muhimu. Aidha, mnada wa tanzanite uboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanda cha kusafisha/kuchakata madini ufanywe kwa haraka ili kuongeza thamani ya madini yetu badala ya kupeleka India.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muheza maeneo ya Amani – Sakale, Kata ya Mbomole kuna madini ya dhahabu na wananchi kila mara wanakamatwakamatwa na kufukuzwa. Nimemuomba Naibu Waziri, Mheshimiwa Doto, wiki iliyopita anitumie wataalam tujue tuna madini kiasi gani, je, yapo Milima ya Sakale? Je, yapo katika Mto Kihara? Kama ni hivyo tutengeneze utaratibu mzuri wananchi wa Muheza waanze kuchimba huko Mlimani Sakale.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalam wote kwa mwelekeo wa mabadiliko makubwa katika Sekta ya Madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kuititia Sheria ya Mabadiliko ya Mwaka 2017 ambayo sasa yanatarajiwa, yakitekelezwa vyema, yataboresha tija katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa usimamizi wa sekta ya madini kwa mujibu wa Sheria ya 2017 (mabadiliko). Nashauri Serikali iweze kusogezza huduma za ushauri wa kitaalam, usimamizi na kadhalika na uwepo wa wataalam wa kutosha na wenye weledi stahiki kama ilivyositisizwa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2011/2012 - 2015/2016 na 2016/2017 - 2020/2021. Kwa Tunduru tuenze kwa kupatiwa Mthamini wa Madini haraka. Tunaomba Serikali iongeze/iboreshe bajeti kwa Wizara hii muhimu kwa uchumi wa nchi, iwe ni mbegu tayari kwa mavuno zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ielekeze nguvu zaidi katika madini ya vito (*gemstones*). Madini makuu yaliyozoleka ni muhimu kama yale ya vito. Hata hivyo, bado

kama Taifa tunahitaji kuelekeza nguvu katika uchimbaji na shughuli zote husika za madini ya vito ikiwemo uongezaji thamani. Katika kutekeleza haya, Serikali ilekeze nguvu katika maeneo yenye *potential/au* yaliyogundulika kuwa na aina na viwango (*types and quantities*) za madini ya vito.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iandae/iboresha kanzidata ya maeneo yenye madini ya vito (aina na viwango) katika maeneo yote nchini. Tunduru inayo madini ya vito ya *alexandrite* ambayo kwa Tanzania, kwa mujibu wa Taarifa ya *GST* ya mwaka 2011, yanapatikana Tunduru, Mbulu na Nachingwea. Madini haya ni mionganoni mwa yale adimu duniani ambapo Tanzania ni mionganoni mwa nchi chache duniani zenye madini haya, nchi yetu ikiwa ni mionganoni mwa nchi 10 bora zenye viwango vya madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini hayo ya *alexandrite* ni yenye thamani kubwa yakiwa ni ya sita duniani ikitanguliwa na *red diamond, taaffeite, grandidierite, serendibite na diamond*. *Alexandrite* ina thamani ya Dola za Kimarekani 12,000 kwa karati moja. Ni muhimu sasa kwa Serikali kuweka nguvu kubwa vya kutosha kwa shughuli za madini ya *alexandrite*. Tafsiri nyepesi ni kwamba maeneo yenye madini haya yapewe umuhimu katika uboreshaji wa shughuli za madini hususan madini ya vito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduru, zaidi ya *alexandrite* inayo madini ya vito mengine ya dhahabu, *dismuth* na *Sapphire* kwa mujibu wa *GST*(2011). Taarifa kwenye mitandao zinaonesha uwepo wa madini ya vito zaidi Tunduru kama ifuatavyo: *Chrysoberyl, chrysoberyl var; alexandrite, corundum, corundum var, ruby, corundum var, sapphire, diamond, garnet group, magnesio taaffeite – 2N' 2S, Magnesio Taaffeite – 6N 3S, spinel, tourmaline na zircon*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Serikali kuititia *GST* ifanye utafiti wa kina vizuri zaidi ili kuthibitisha taarifa hizi. Ikithibitika, eneo la Tunduru liorodheshwe kuwa eneo lenye uwezo wa kuchangia Pato

la Taifa, lakini pia Halmashauri iboreshe bajeti yake, hivyo nguvu zaidi iwekwe huko Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hali hii maana yake ni utafiti zaidi, vifaa zaidi, wataalam zaidi na kadhalika ambapo kwa ufupi ni bajeti zaidi. Serikali iboreshe bajeti ya Wizara ya Madini.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uzima asubuhi hii. Vilevile napenda kuwapa pole wananchi wa Buyungu kwa kuondokewa na Mbunge wao. Mwenyezi Mungu atawapa subra katika kipindi hiki kigumu walichokipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sina budi kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Naibu wake, pamoja na Watendaji wake wote kwa bidii wanayoionyesha katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania siyo nchi maskini lakini kuna baadhi ya wananchi na hata wawekezaji wanatuongezea umaskini. Madini tuliyonayo ni ya aina mbalimbali ambazo kama zitafuatiliwa vizuri, Taifa letu lingeneemeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya wachimbaji hawauzi bidhaa zao katika masoko husika ila wanauzwa katika njia za panya. Naomba Serikali iwe madhubuti, wachimbaji wakubwa na wadogo wauze bidhaa zao katika masoko yanayotambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ajali za mara kwa mara zinatokea katika migodi ikiwamo wananchi kuangukiwa na kifusi au migodi kujaa maji. Serikali ina mkakati gani kuhakikisha hali hii ya hatari haitokei mara kwa mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya pekee ambayo hayapo nchi yoyote duniani ni *tanzanite*. Madini haya

Wakenya huyanunua sana na kuyapeleka nje na kujifanya kuwa wao ndiyo wachimbaji wa madini haya. Naiomba Serikali itangaze madini yetu na pia iileweshe dunia kuwa *tanzanite* ni madini yanayopatikana Tanzania tu, siyo nchi yoyote katika dunia hii.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanzaa, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kuandika na kuwakilisha hotuba hii kwa ufasaha na kwa utaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa hatua inazozichukua juu ya uendelezaji wa wachimbaji wadogo. Kama inavyojulikana kuwa kundi hili la wachimbaji ni kubwa sana katika nchi yetu kuliko kundi la wachimbaji wengine. Kundi hili linaigusa moja kwa moja jamii ya kipato kidogo ambao wanahitaji msukumo wa kipekee ili waweze kumudu maisha yao na kuweza kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika hili ni kuwa Wizara iendelee kuwawezesha kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu pamoja na kuwapatia elimu juu ya kazi hii ili waweze kufanya kazi hii kitaalamu badala ya kuendelea kufanya kazi hii kimazoea. Ikiwa Serikali itawasaidia wachimbaji hawa, wanaweza kwa kiasi kikubwa kuchangia Mfuko wa Serikali kwa kumudu kulipa tozo zitakazowekwa kwa mujibu wa utaratibu wa sheria. Pia Serikali kwa kushirikiana na Wizara hii iweke mpango maalum wa malengo ya kuazimia kuwaondoa wachimbaji hawa katika ngazi ya wachimbaji wadogo mpaka kufikia kuwa wachimbaji wakubwa.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukurani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kukubaliana na ushauri wa kuzitenganisha Wizara ya Nishati na Madini kwa maslahi ya Taifa. Hii yote ni jitihada ya kupambana kwa kufahamu rasilimali za nchi zenyé maslahi ya wananchi na kunufaika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeza kwa uteuzi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu. Ni watu wenye mwitikio wa kujituma, kujitoa kwa uzalendo uliotukuka kwa maendeleo ya nchi na utendaji wao ambaó unaunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, *STAMICO* nimeisikia muda mrefu nchini ikiwa inahusika na madini, lakini matunda yake hayana afya kwa maendeleo ya nchi yetu. Ni vyema ikaangaliwa upya katika mfumo wake wa utendaji na usimamizi kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina madini kadhaa na wananchi wengi wanajihuisha na uchimbaji mdogo mdogo wa kupata madini yanayofahamika na yasiyofahamika na hapa ndipo wananchi ambaó ni wachimbaji wadogo wanadhuluiwa na watalaamu wachache tulionao. Mkoa wa Rukwa kuna wachimbaji wadogo kwenye milima ndani ya Kijiji cha Kastuka, hawayafahamu hayo madini lakini wachimbapo wanayaleta Dar es Salaam na bado wanaendelea na kazi hiyo, ndiyo kusema wataalaam wameyafahamu. Tunaomba Wizara iweke utaratibu wa kitengo maalum kuzungukia nchi nzima na kubaini madini yanayopatikana kila Mkoa na kuwekwa takwimu sahihi ya madini tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ijipange vyema na suala zima la uchenjuaji wa madini hayo kwa kuyaongeza thamani na kutambua kwa kuchanganua aina za madini moja moja. Kwa umakini huu, ukizingatiwa, tutafahamu thamani ya madini yetu na kuwa na mchango mkubwa kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na njia nyingi za panya za kutorosha madini yetu katika kutafuta soko zuri kwa wachimaji wadogo. Tunaomba Serikali kurejesha utaratibu wa Soko la Dhahabu la Benki Kuu kwani wanatapeliwa na walanguzi na bei wanayoipata ni ndogo, huku kazi waifanyayo hadi kuipata mali hiyo ni ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa 21 wa hotuba ya Wizara, pamezungumzia suala la usimamizi wa matumizi ya baruti na udhibiti wa matumizi ya baruti kwenye shughuli hizo mbalimbali kwa kuhakikisha shughuli hizo zinafanyika kwa usalama na kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Sikuona ni namna gani wananchi wanaozunguka maeneo yanayotumia baruti na majengo yao kuathirika, wanalipwaje fidia na wahusika au wanahudumiwa vipi na wahusika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa tuna hao wahusika wa matumizi ya baruti katika kupasua mawe na kutengeneza kokoto, changarawe na kadhalika. Wananchi wanaozunguka eneo hilo, nyumba zao zimepata nyufa kadhaa na kupunguza uimara. Ni vyema Serikali ikaona namna ya kuwaangalia wahanga hawa. Pia uwepo msukumo wa hao wahusika kwa mchango wao kwa maendeleo ya huduma za jamii kuwa nilazima, siyo hiari au mahusiano ya viongozi kwa matakwa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa madini yanaonekana kuwa na uwezo mkubwa wa kuchangia pato la Taifa, hivyo tunaomba Wizara ya Fedha kuweka jitihada ya makusanyo na kuwapelekea Wizara ya Madini bajeti ya Maendeleo ya shilingi 19,620,964,000 ambazo asilimia kubwa ni fedha za ndani. Ni matumaini yetu kwamba wachimbaji wadogo na wananchi wetu watanufaika na kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujengewa ofisi ya madini kwenye mikoa yenye madini kuliko kuwa na Ofisi Dar es Salaam, ndipo Wizara itakuwa na shinikizo la kuandaa wataalam na kuwasambaza mikoani au kwenye kanda kwa kuanzia. Tutaimarisha wachimbaji wetu, tutawadhibiti

walanguzi na matapeli na mapato yatafahamika na kuyasimamia kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Angellah Kairuki; Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo; na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kuwasilisha hotuba yao ili tuweze kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali na kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuamua kufanyike marekebisho ya Sheria za Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Wananchi kwa ujenzi wa ukuta wa Mererani ambao umeweza hata kupandisha thamani ya madini ya *tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu elimu katika maeneo ya machimbo. Katika machimbo, wachimbaji wadogo hawana elimu ya kutosha kuhusu hatari zilizopo machimboni. Pia kuna maambukizi makubwa sana ya UKIMWI. Je, ni mkakati gani Serikali inaweka ili kuwanusuru vijana wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yanapoanzishwa machimbo mapya kama machimbo ya Nyakavangala yaliyopo Jimbo la Ismani Mkoa wa Iringa, ni utaratibu gani unafanywa ili kuwaelimisha wananchi walio katika machimbo ili kujua fursa zilizopo katika eneo lao? Kwa sababu kuna watu wanakuja kutoka maeneo mbalimbali kufuata fursa wakati waliopo katika maeneo hayo wanakuwa hawajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika machimbo mapya kuna tatizo kubwa sana la huduma za kijamii kama ulinzi, vyoo, zahanati na kadhalika. Halmashauri hazina uwezo, je, Wizara huwa inawasaidiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu fedha kutopelekwa katika vyuo vya madini. Vyuo vyetu ya madini vina changamoto kubwa sana ya fedha kutopelekwa kwa wakati. Naomba kama Serikali ina dhamira ya dhati ya kusaidia sekta hii, itoe fedha kwa wakati ili kuboresha vyuo vyetu ili viweze kuwa na mazingira mazuri ya kuzalisha watalaam wetu wa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni watoto wadogo kutumika katika machimbo. Pamoja na kuwa ipo sheria ya kumlinda mtoto kutoajiriwa au kutumika kufanya kazi, lakini tumeona umekuwa ni utaratibu wa baadhi ya wananchi na makampuni kuwatumia watoto wadogo kufanyishwa kazi migodini. Je, hatua gani zinawekwa na Serikali kukomesha tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua, je, Serikali inaisaidiaje *STAMICO* ili kuiwezesha kupata fedha ya kutosha ili shirika hili liweze kufanya kazi yake kama ilivyokusudiwa katika uanzishwaji wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na Manaibu wote. Nina imani kwa juhudii yao watainua sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Tumemaliza uchangiaji, sasa ni zamu ya Mawaziri kuhitimisha na tunaanza na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atafuatiwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mezani. Mimi nitajielekeza zaidi katika masuala ya kisheria kwa sababu katika michango mbalimbali iliyotolewa kwa maandishi na kwa mdomo umeonyeshwa wasiwasi tofauti tofauti kuhusu hasa hizi sheria mpya tulizotunga mwaka jana za *Permanent Sovereignty* na

ile ya Reviewya Mikataba. Kwa hiyo, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali nafikiri ninao wajibu wa kutoa maelezo kidogo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu katika maelezo yangu haya niirejee kidogo historia. Kuna wakati fulani hapa Waziri wa Katiba na Sheria aliwahi kuzungumza umuhimu wa historia ya sheria na mara nyingi mambo mengi tunakuwa hatuyaelewi kwa sababu historia ya kitu husika tunakuwa hatukifahamu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria yetu ya Madini imeanza wakati wa Mjerumani. Mwaka 1895 Mjerumani alitunga sheria iliyokuwa inagusa masuala ya ardhi na akasema kwamba kwa sehemu kubwa ya ardhi ya iliyokuwa *German East Africa*, Tanganyika baadaye, iliwekwa chini ya Mfalme wa Ujerumani, lakin hiyo ikiwa ni pamoja na madini yote yaliyokuwa katika ardhi ile. Pia akatoa leseni za uchimbaji wa madini, palikuwa na uchimbaji tayari maeneo mbalimbali ikiwemo Geita na akayapa makampuni ya Ujerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, alivyochukua utawala Muingereza akatunga sheria na kati ya sheria za kwanza kabisa kutunga ilikuwa ni sheria inayogusa masuala ya madini. Kwa ufupi katika sheria hizo aliyaweka madini yote yanayopatikana Tanganyika wakati ule na kwa sasa Tanzania chini ya Mfalme wa Uingereza wakati huo. Pia aliweka taratibu ambazo zilihakikisha kwamba ni makampuni kwa kweli kwa sehemu kubwa ya Uingereza au ambayo yalikuwa na *connection* ya Uingereza ndiyo yangeweza kuchimba madini katika nchi hii. Kwa hiyo, kwa ufupi huo ndiyo ukawa msimamo wake wa kwanza katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1929 sheria ikabadilishwa na alikuwa bado Mkoloni ni huyo huyo Muingereza lakini ilibakiza misingi ile ile; kwamba madini yote ni mali ya Mfalme wa Uingereza na kampuni za kuchimba madini yale sehemu kubwa yanatoka Uingereza na huo ndio ukawa msimamo. Pia ulikuwa msimamo kwa ujumla katika

sheria zinazosimamia uwekezaji kwa maana ya kwamba sehemu kubwa ya wale waliopewa nafasi ya kuwekeza katika nchi, hii ikiwa ni pamoja na kuchimba madini, walitoka Uingereza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1959 miaka miwili kabla ya Uhuru, *World Bank*wakijua kwamba Tanzania wakati ule Tanganyika itapata uhuru walifanya ziara ya kuja kumuona Mwalimu, wakamwambia Mwalimu tunafikiri ni vema nchi yako ikabadiilisha sheria zinazohusu uwekezaji na ambayo ingegusa pia uwekezaji katika madini. Akawauliza mnataka nifanye nini? Wakasema inabidi uzirekebishe sheria hizi ili ziweze kuruhusu na kutoa uwazi kwa makampuni mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali waweze kuja kuwekeza hapa. Mwalimu akawauliza akasema mbona hizi sheria zimekuwepo toka Muungereza na Mjerumani alipokuwepo na zina shida gani sasa, kama ni hivyo basi tutaziacha hizo hizo sheria ziendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uhuru nchi ilichukua hatua na kupitia katika Katiba ya *TANU* ya mwaka 1965 ilianza kuweka vipengele vinavyosema sasa hizi maliasili zilizoko Tanzania yakiwemo madini ni mali za watu wote, ni mali za Watanzania. Mwaka 1967 kama tunavyofahamu kulikuwa na Azimio la Arusha na katika lile Azimio baadhi ya athari zake ilikuwa ni kwamba uwekezaji mkubwa ni lazima urudi mikononi mwa wananchi, mikononi mwa Taifa na msimamo huo ukaathiri pia sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1977 tulipopata Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 walau vipengele vinavyohusu rasilimali vikaingia katika Katiba hasa katika Ibara ya 9 na Ibara ya 27. Mwaka 1979 tukafanya mabadiliko mengine makubwa ya Sheria ya Madini na haya ni baada ya uhuru. Katika mabadiliko hayo, maana shinikizo lilikuwa limeshaanza wakati ule basi tukaruhusu kampuni kuanza tena kurudi kuwekeza katika masuala ya rasilimali na hasa madini; maana mwaka 1967 msimamo wa sera ulikuwa kama unayaondoa yale makampuni lakini pia tukaruhusu wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya 80 na 90 mwanzoni kukatokea kitu kinaitwa *Washington Consensus*. Kwenye *Washington Consensus* ambayo ilisimamiwa na *World Bank*, *IMF* na Marekani pamoja na mataifa mengine makubwa uliwekwa mkakati wa makusudi wa kurudi Afrika na kuyadhibiti tena madini ya Afrika. Kwa sababu nchi nydingi za Afrika miaka ya 60 zilikuwa zimechukua misimamo ambayo ilikuwa inayanyima makampuni kutoka nje nafasi ya kuyaendeleza au kuya-exploit madini hayo. Hiyo ndio ilitupelekeea kwenye Sheria yetu ya Madini ya mwaka 1998 ambayo kwa kweli kwa kiasi kikubwa ilikuwa na *influence* ya mtazamo wa *World Bank*. Baada ya hapo palikuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kwa ujumla, ndio ikapelekeea mabadiliko fulani ya msingi yaliyofanyika miaka ya 2010 hususani katika Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze kwa ufupi, hizi sheria mbili tulizotunga mwaka jana chimbuko lake ni nini, pamekuwa na maswali, sasa tumetunga sheria, tumebadilisha sheria, tumewa-*discourage investors*, tumewa-*disappoint investors*, hizo sheria zimetokea wapi? Sheria hizi kimsingi zilikuwepo kupitia maamuzi ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Hayo Matamko ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1952, mwaka 1958, 1962, 1966, 1974 na kuendelea na baadaye yaliingia katika mikataba ya kimataifa ikiwemo zile *International Covenant on Civil and Political Rights*, *International Covenant on Economic and Social Right* ya mwaka 1966. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha msingi cha kuzungumza hapa na ambacho tunakipata sasa katika hizi sheria mbili za mwaka jana ni zile haki nne (4) kuu muhimu ambazo unazikuta katika haya Matamko ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa pamoja na ile Mikataba ya Kimataifa iliyotungwa katika uelekeo huo. Ya kwanza, haki ya nchi kutambuliwa kwamba inamiliki maliasili. Nimeeleza Muingereza na Mjerumani walivyochukua nchi jambo la kwanza walisema rasilimali zote za madini ni mali ya Mfalme au yako chini ya Mfalme.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya pili ni haki ya kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa rasilimali hizi. Hii ni ya msingi sana kwa sababu kuna haki ya kutunga sheria, kuna haki ya kuangalia uendelezaji, kuna haki ya kuangalia *processing*, kuna haki ya kuangalia masoko, uuzaaji na kila kitu. Hizi haki zote ziko humu ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya tatu, ni haki ya nchi na watu wake kushiriki katika uendelezaji. Naweza nikasema kwa uhakika kabisa kwamba sheria na mfumo uliokuwa umewekwa wakati wa Muungereza na kwa mtazamo wa *Washington Consensus* ulikuwa umewekwa kwa namna ambayo hauipi nchi na watu wake nafasi ya kushiriki katika kuendeleza hizo rasilimali. Haki ya nne ni haki ya nchi kufaidika na rasilimali hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo manne utayakuta vizuri sana katika hizi sheria mbili tulizozitunga mwaka jana. Kwa hiyo, kimsingi sheria zilikuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee dakika moja na nusu kwa sababu nazungumzia masuala mazito ya kisheria, sheria hizi ni sheria msingi kwa maana kwamba zinakuwa na *effect* kwenye sheria nyinginezo za nchi hii ambazo zinagusa rasilimali na ndiyo maana zikawekwa chini ya usimamizi na uangalizi wa Waziri wa Katiba na Sheria. Baadhi ya misingi ile iko kwenye Katiba na baadhi ya misingi ile inatakiwa ifanyi kazi katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba pana wasiwasi mwingi, tutashtakiwa, tutafilisiwa, sijui tutapata shida gani kwa sababu ya kutunga sheria hizi, tumezitunga kwa kuzingatia haki yetu iliyo katika Sheria za Kimataifa. Kwa upande mwingine kama nchi hatupaswi sasa kuogopa. Bara la Afrika kwa ujumla limekuwa linatishwa sana, lakini kama nchi tumejipanga, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali sasa iko vizuri kabisa, tuna Ofisi sasa ya Wakili

Mkuu wa Serikali na kama kunajitokeza jambo lolote nchi kama nchi hatupaswi kuwa na wasiwasi wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Waheshimiwa Wabunge kwa wale wanaopenda kusoma wakasome *degree* yake ya tatu ameongelea mambo haya, ndiyo maana nadhani amezungumza kwa kirefu sana lakini ndiyo eneo lake na yeye la kujidai amefanyia utafiti kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja. Pili, nianze kwa kukushukuru sana wewe na pia nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Shukrani zangu zina msingi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata heshima ya kukusimamia *Masters* yako na uliadikia kuhusu *The Rights to Clean and Health Environment* na *case study* yako ilikuwa ni *Geita Gold Mine*. Ingawa nilikusimamia lakini nilijifunza na sikujua hayo ni maandalizi ya baadaye ndani ya utumishi wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye na yeye nilimsimamia *PhD* yake katika somo hili hili alilolizingumza leo na yeye kwake nimejifunza sana. Sikujua kwamba nilikuwa naandaliliwa kuja kufanya kazi ambayo itahusiana na hawa wanafunzi wangu wawili ambao pia ni walimu wangu wakati huo, yaani Naibu Spika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni heshima kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nimshukuru sana na mimi Mwalimu wangu aliyenismamia *PhD* yangu Ujerumani,

chuo ambacho sasa kinafikisha miaka 70 na ye ye amestaafu. Kwa sababu miaka ile ya mwisho wa 80 na mwanzo wa 90 wakati tunayazungumzia haya aliyoyaeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa nchi za Ulaya yalikuwa ni mapinduzi makubwa. Sikujua kwamba baadaye nitapata fursa ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunipa fursa ya kuitumikia nchi hii na kunipa jukumu la kuisaidia nchi hii kutunga sheria hizi za madini na mambo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, falsafa na muktadha wa usimamizi wa madini katika nchi zetu umebadilika. Napozungumza falsafa narudi kwenye Kitabu cha Ibrahim Hussein cha Mashetani, yule shetani mmoja aliyekuwa daima anasema *weltanschauung*, *weltanschauung*. *Weltanschauung* maana yake ni muono mpya wa mambo ambayo yalikuwa dhahiri lakini watu walikuwa hawaoni yakiwa dhahiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unyonyaji wa madini yetu na mataifa ya nje lilikuwa ni jambo dhahiri lakini hatukuliona kuwa ni dhahiri na likapambwa, likarembeshwa likafanya kuonekana ni jambo la kawaida na tukashindwa kutofautisha kati ya uwekezaji (*investment*) na unyonyaji (*exploitation*). Kwa hiyo, kwa muda wote huu sheria zetu za madini zilijikita katika unyonyaji (*exploitation*) na hatukuwa tumeweka mazingira mazuri ya uwekezaji (*investment*) kwa faida ya nchi zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatua tulizozichukua ni hatua za kimapinduzi na ni lazima zipingwe kwa nguvu zote na wale wote waliokuwa wanafaidika na hali hiyo. Kwa hiyo, ni jukumu letu kusimama kidete pamoja na Rais wetu kuhakikisha kwamba hii *weltanschauung* (msimamo) mpya tunausimamia kwa nguvu zetu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana mingoni mwa mambo makubwa ambayo yamefanywa na sheria hii ni kuondoa kabisa *Mining Development Agreements*,

zilioingiwa ndizo za mwisho. Kuanzia sheria hii ilipopitishwa, hakuna tena MDA ni *Special Mining License*, *Mining License* na *Primary Mining License*. Kwa sababu ya matatizo ya utendaji ndani ya Wizara na Kamisheni sasa *Special Mining License* na *Mining License* zitatolewa kwa kibali cha Baraza la Mawaziri. *SML* ni Baraza la Mawaziri ili Serikali nzima ishiriki katika kuhakikisha kwamba leseni za madini za wachimbaji wakubwa zinatolewa kwa manufaa na maslahi ya nchi yetu, hakuna tena MDA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunahangaika na MDA zilizokuwa zimeingiwa lakini hakutakuwa na mpya ili tuondokane na kuwa na matabaka mawili ya wachimbaji wanaochimba kwa leseni na wanaochimba kwa mikataba maalum, wote sasa watachimba kwa masharti ya leseni na asiyetaka hivyo asije. Madini haya babu wa babu zetu, babu zetu, baba zetu na sisi tumeyakuta hayajaoza, asiyetaka kuja kuchimba madini haya kwa masharti haya ayaache na sisi tutakufa, tutazikwa watakuja watoto, wajukuu na vitukuu wetu watavikuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema madini ni utajiri unaokwisha na ni muhali kuyatumia kwa matumizi ya kawaida. Ni lazima yatumike katika uwekezaji wa kukuza ustawi wa watu na maendeleo ya nchi katika miundombinu na viwanda na uwekezaji wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote inayochimba madini *for recurrent expenditure imefilisika*. Madini ni lazima yaende katika *strategic investment; standard gauge railway, Stiegler's Gorge*, viwanda na miundombinu. Maana yake tuvune madini kwa kiasi, tusiyavune madini kwa pupa kama vile mwisho wa dunia ni sisi, tutakufa tutaiacha nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuvune madini kwa kiasi ili vizazi vijavyo navyo viyakute madini na yale tutakayokuwa tumeyachimba wakute faida yake katika sekta nyingine za uchumi; miundombinu, vyuo vikuu, viwanda. Hivyo ndivyo ilivyofanya nchi ya Nigeria na ndiyo

hilo Naibu Spika ulilizungumzia katika Taslifu yako ya *Masters, intergeneration equity*. Sisi kwa lugha ya zamani ni mawakili wa mali za Mungu siyo kwa matumizi yetu sisi tu lakini kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naonya hii shauku/hamu/pupa ya kutaka tuyachimbe madini yote; tuyabakize mengine kwa viazi vijavyo. Bara la Afrika tumekuwa tunasukumwa na nchi za nje kutaka tuchimbe madini yetu kwa namna hiyo. Ndiyo maana baada ya hatua hii iliyochukuliwa, nashukuru sana nchi nyingine za Afrika zimefuata na nchi ya mwisho ambayo nilitegemea ingefuata mfano wa Tanzania ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Zambia wamefanya hivyo na nchi nyingine ili tuyatunze haya madini ya Afrika kwa vizazi vijavyo kama ambavyo Norway wao mafuta wanayoyachimba wanaweka akiba kwa ajili ya vizazi vijavyo na kuna fedha ambayo imewekwa itatumika miaka 50 baada ya tone la mwisho la mafuta na gesi ya mwisho kwisha. Kwa hiyo, unaona wenzetu wanavyofikiria na sisi pia ndiyo malengo ya sheria hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko haya ya kisheria, Mheshimiwa Rais ametusaidia sana, moja ni la makinikia. Makinikia yalisemwa si mali ni mchanga hauna maana lakini sote tumeona mara baaada ya makinikia kuzuiwa kwenda nje ndiyo tumejua kwamba makinikia ni mali, ni rasilimali. Ndiyo maana ndani ya mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 imetamka wazi kuwa sasa makinikia nayo ni mali inayouzwa kama mali inayojitegemea, si kama sehemu ya yale madini yaliyokuwa yamepimwa. Kwa hiyo, limetusaidia na ndiyo maana tangu sheria hii imetungwa hakuna makinikia ambayo yameshatoka nje ya nchi ili uwekwe utaratibu wa kuyaongezea thamani makinikia kama bidhaa inayojitegemea. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo hatukulija ndani ya makinikia kuna aina ya madini ingawa kiasi chake ni kidogo lakini yana thamani kubwa sana yanaitwa *rare-*

earth, ya thamani kubwa sana. Kwa hiyo, utaratibu mpya umekwishafanyika na kanuni zimekwishatungwa na Mheshimiwa Waziri zitakazosimamia suala hilo la makinikia na itakuwa ni marufuku kuyasafirisha makinikia nje ya nchi kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria ya Madini na Kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo ambayo pia yamezungumzwa na kuulizwa sana hapa ni kuhusu kishika uchumba cha majadiliano kati ya Barrick na Tanzania. Kwanza nichukue fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu na pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa sana aliyotupa sisi kusimamia majadiliano hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sakata hilo lilipoanza tulitishwa, tuliambiwa tutafilisiwa, hatutafika popote na hiyo ndiyo illikuwa sababu kwa kiasi kikubwa ya kuwaficha wajumbe wengine kwa sababu bahati mbaya nchi yetu tumeacha kujadili masuala, tunajadili watu. Watu wangejua mmoja wa wajumbe hao ni Chacha, basi huyo Chacha angechambuliwa mpaka angechacha kama chakula kilichokaa siku nyingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mazungumzo yale yaliyokamilika tarehe 19 Oktoba, 2017 yalikuwa ya mafanikio. Mafanikio mimi kama mmoja wa watu walioshiriki, siyo kile kilichopatikana lakini kile ambacho kimetuwezesha sasa kuangalia Tanzania ya kesho katika matumizi yake ya madini. Hii ni kwa sababu tumerithi mikataba ambayo iliyokuwa ina matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yale makubaliano yalikuwa makubaliano ya msingi na baada ya hapo tumeingia katika majadiliano ya kina ambayo napenda kusema kwamba yanaendelea vizuri kati ya timu ya Serikali na Barrick na majadiliano hayo yanakaribia kufikia hatma yake. Kwa mujibu wa ratiba ambayo tulikuwa tumepeana, mwisho wa mwezi Juni au katikati ya Julai tutakuwa tumefikia katika hatua za mwisho na ukamilishaji wake ni pamoja na utaratibu wa ulipwaji wa malipo hayo ya Dola milioni 300. Kwa hiyo,

tunaendelea na *Inshallah*, ndiyo maana ya neno *Inshallah*, maana *Inshallah* ni mapenzi ya Mungu (*Allah*) siyo hiyari yako, *Inshallah*, *Inshallah* mazungumzo hayo yatazaa matunda. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba shughuli hiyo haikuishia tu na Barrick, tunafanya mazungumzo na kampuni nyingine. Tumekwishamaliza mazungumzo na Kampuni ya *Tanzanite One Mining Limited*, mazungumzo ambayo yalifanikiwa na kusainiwa makubaliano tarehe 15 Aprili, 2018. Wao wamekiri makosa waliyoyafanya, watalipa kodi na tozo zote na pamoa na hiyo watatoa fidia kwa Serikali; na tayari *installment* ya kwanza ya fidia hiyo imeshalipwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaishi dunia ambayo tumejifunza, utakapotaja mambo kama hayo wale wasiotutakia mema ambao wanafunga kesi kesho na keshokutwa, watajua mna kiasi gani maana yake nyumba yenye fedha/mali ndiyo wezi huinyemelea. Ndani ya Serikali na kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali atajua fedha hizo zilipoingia na zilipo kwa sababu hazingii kama maduhuli ya Wizara ya Madini, zinaingia kama fidia kwa Taifa na zina utaratibu wake na zinasimamiwa na Katibu Mkuu Kiongozi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nchi tumejifunza hata hiyo fidia hatutaitamka katika kadarnasi lakini ndani ya Serikali na wale wanaoruhusiwa kujua watajua ni kiasi gani *Tanzanite One Mining Limited* wamelipa. Maana yake tumejifunza sasa hivi kesi zimeongezeka kwa sababu wanajua tuna hela, kwa hiyo ni upuuzi pia kusema kila kitu. Unapowaambia watu una pesa unaita watu kuja kukuibia lakini fedha ipo, utaratibu upo, *Paymaster General*/na *Auditor General*/upo na nashukuru sana *Tanzanite One Mining Limited* kwa kutekeleza ya kwao. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza pia mazungumzo na Ashanti Gold na tutaendelea nayo tena Julai, tumekwishakutana nao mara moja. Tutafanya

majadiliano na kampuni nyingine za tanzanite, kampuni kama 10 zinazovuna tanzanite. Tutafanya mazungumzo na kampuni zote, Kampuni ya Williamson Diamond Limited ambayo karibu tutaanza nao mazungumzo lakini pia Al - Hillary.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni mlolongo wa mazungumzo na kila yatakapokwenda Taifa litakuwa linaarifiwa, lakini kwa muktadha na hali ya leo kiasi cha fedha kitaingizwa Hazina na hatutapenda kikitangaza sana na watu watafahamu kwa njia nyingine ili tuepukane na hali ambayo tumejifunza kwamba baada ya watu kujua tuna fedha, tunajenga *standard gauge railway*, tumenunua ndege saba sasa yanakuja madeni mengine ya miaka ya 70. Mtu alikuwa na deni toka mwaka 1978 leo ndiyo analikumbuka, nje huko na ukilisoma unajiuliza tangu mwaka 1978 huyu mtu hizi fedha mbona alikuwa hadai, ni kwa sababu sasa wamejua kuna kitu. Kwa hiyo, nawaomba Watanzania watuelewe, waielewe Serikali yao na waivumilie inapopambana na hali hii ya unyonyaji mkubwa na hatua ambazo imezichukua ili kuyarekebisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimpongeze sana Waziri wa Madini na Naibu Mawaziri wa Madini. Naomba tena kurudia kuunga mkono hoja, niliogopa nisije nikapigwi kengele kabla siaunga mkono hoja mwanzoni, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa maelezo hayo Mheshimiwa Waziri. Mimi naamini kwa sababu tuna taraji kuhitimisha jioni, Waheshimiwa Wabunge ambao hawapo hapa watapata fursa ya kupitia Taarifa Rasmii za Bunge ili wasije wakaendelea kuyauliza tena jioni mambo yaliyoelezwa kwa kirefu kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni ambao hatukupata fursa ya kuwatangaza asubuhi. Tunao wageni wa Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Madini; wa kwanza ni Mwenyekiti wa TAMIDA ambaye ni Sammy Mollel pamoja na wajumbe wake wanne, karibuni sana. (*Makof*)

Tunaye pia Mwenyekiti wa *TAWOMA* Rachel Joseph, karibu sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Katibu wa Chama cha Wachimbaji wa Madini (*MAREMA*) ambaye ni Aboubakar Madiwa pamoja na mjumbe mmoja. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Mwenyekiti wa Bunge Sports Club, anawatangazia kwamba mwishoni mwa wiki, kwa maana ya siku ya Jumamosi na Jumapili kutakuwa na michezo ifuatayo ya kirafigiki. Jumamosi tarehe 2 Juni, 2018, *Ndugai Boys* na Chuo cha St. Johns watacheza mchezo wa mpira wa miguu (*football*) na *netball*. Pia siku ya Jumapili tarehe 3 Juni, 2018, *Ndugai Boys* watacheza na *Ulyankulu Veterans* ambaao hawa wanaitwa *Kadutu Boys*. Michezo yote itafanyika kwenye uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 10.00 jioni. Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wa Dodoma wanakaribishwa kwenda kushangilia timu yao. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nirudie tena tangazo la Katibu wa Bunge kuhusu zoezi la kesho ambalo Mheshimiwa Spika atapokea na kukabidhi Serikalini Taarifa za Kamati Maalum alizozilunda za ushauri kuhusu sekta ya uvuvi wa bahari kuu na gesi asilia. Hafla hiyo itafanyika kesho saa tatu na nusu asubuhi nje ya ukumbi wa Bunge upande wa lango kuu la kuingilia. Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine nimeletewa taarifa hapa mbele kwamba asubuhi baada ya kipindi cha maswali na majibu nilipoombwa miongozo hapa, Mheshimiwa Richard Ndassa hakuwa ameomba mwongozo lakini alisimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47 na 48(2)(a). Kwa sababu hiyo nalazimika kutoa ufanuzi huu ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 47, sina haja ya kurudia maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Ndassa, yalikuwa yanahu matumizi ya mashine za kielektroniki za kukusanya

mapato (*EFDs*) na akasema hazijafanya kazi kwa muda kama wa miezi mitatu hivi na haionekani kama kuna suluhisho ili iweze kusaidia Serikali kupata mapato yake, kwa sababu kwa taarifa alizonazo ye ye mapato yameshuka kutokana na kutokufanya kazi kwa mashine hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ndassa alitumia Kanuni ya 47 akisema hili ni jambo la dharura lakini pia kanuni ya 48(2)(a); Kanuni ya 48 inazungumzia masharti ya matumizi ya Kanuni ya 47. Kanuni ya 48(2)(a) aliyoitumia Mheshimiwa Ndassa ni mojawapo ya masharti yaliyowekwa kwamba hili ni jambo mahsus, ni kweli lakini maamuzi ya kiti juu ya jambo hili, Kanuni ya 48(3)(c) inasema jambo linaloletwa kwa hoja chini ya kanuni hii litahesabiwa kuwa ni jambo la dharura iwapo, (c) hakutatokea fursa ya kulijadili siku za karibuni kwa njia ya kawaida ya kushughulikia mambo ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi Waziri wa Fedha ameshaleta randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake. Kwa hivyo, jambo hili linakuja siku za usoni, Waheshimiwa Wabunge tutapata fursa ya kulijadili kwa kirefu kwa kina na kupata majibu ya Serikali na mwelekeo wake kuhusu jambo hili la *EFD*. Kwa hivyo, Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri katika jambo hili alilokuwa ameomba ufanuzi Mheshimiwa Ndassa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niwakumbushe jambo moja la kikanuni, Kanuni ya 61 Wabunge wengi huwa tunasimama hapa tunatumia neno la Kiingereza tunasema na-*declare interest* halafu hukamilishi kanuni hii inataka kusemajie. Usiseme wewe una maslahi binafsi ikiwa maslahi yako binafsi hayaendani na ile kanuni ya 61. Kanuni ya 61 inataka ukishasema hivyo ueleze maslahi yako binafsi ya kifedha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ukisimama hapa uende na mbele useme una maslahi gani. Maana watu wanasi mama wanasi mama wana-*declare interest* halafu wanasi maha huyu ni rafiki yangu, tusifanye hivyo Waheshimiwa Wabunge. Kanuni ya 61 imetuwekea masharti ya namna ya

kutumia haya maneno ya kusema mimi nina maslahi binafsi, tutajie maslahi gani uliyonayo ya kifedha. Kwa hiyo, tukasome hii Kanuni Waheshimiwa Wabunge tunapoendelea na michango yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

(Saa 6.57 Mchana Bunge Lilisitishwa mpaka saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na sasa ni zamu za wenyе hoja na tutaanza na Mheshimiwa Doto Biteko, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu kwa ajili ya hoja ambayo imewekwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema, naomba nichukue nafasi hii vilevile nimshukuru sana Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametupa uzima na afya mpaka kuifikia siku ya leo na kwa kweli bila yeye tusingekuwa hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa imani kubwa ambayo alinipatia na kunitfea kuwa Naibu Waziri wa Madini. Naomba niseme tu kwamba nafasi hii ambayo ameniteua nitafanya kazi hii kwa nguvu zangu zote, kwa weledi mkubwa na kwa kumtanguliza Mungu mbele ili ndoto ambayo yeye anaiona kwa ajili ya nchi hii niweze kumsaidia kuifikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Madini, mtoa hoja, dada yangu, Mheshimiwa Angella Kairuki, ambaye kwa kweli pamoja na

mambo mengine amekuwa mwalimu mzuri sana kwangu. Mtafahamu mimi nimeteuliwa mwishoni, nimeingia Wizarani nikiwa mgeni. Mheshimiwa Waziri huyu, pamoja na kwamba yeye ni Mbunge mwenzangu, amekuwa mwalimu mzuri sana kwangu. Mimi naweza kuwa shahidi na Wabunge wengine ambao wameshafanya kazi na Mheshimiwa Angella Kairuki watakuwa mashahidi, ni mtu wa pekee ambaye anapenda kuona kila mmoja anatumia kila talanta aliyonayo kutekeleza majukumu yake na yeye anakusaidia kufanya kazi yako kwa urahisi. Kwa kweli ningekuwa na muda wa kusema ningesema sana kwa bahati kubwa ambayo Mungu amenipa ya kufanya kazi na Mheshimiwa Waziri huyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini. Huyu tunaltana pacha; yeye alitangulia kuteuliwa pale Wizarani, amenipokea, ameni-*orient* vitu vingi, nimejifunza mambo mengi sana kutoka kwake kwa namna ya utendaji lakini kuifahamu Wizara kwa sababu nilikuwa mgeni na yeye alinitangulia kufika hapo. Kaka yangu nakushukuru sana, Mungu akubariki sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana familia yangu; mke wangu mpenzi Bernadetha Biteko kwa kuendelea kunivumilia, yeye pamoja na watoto wetu, wakati natekeleza maukumu haya. Naomba niwashukuru sana wananchi wa Bukombe ambao wao ndio walinchagua na kunituma kuwawakilisha kwenye nyumba hii. Naomba niwahakikishie kwamba kazi ambayo walinipa kuifanya kwa niaba yao ntaendelea kuifanya kwa nguvu zangu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba sasa nitangulie kusema naunga mkono hoja. Kwa kweli hoja hii imeletwa muda mwafaka kwa sababu Wizara hii ni mpya na Waziri tuliyenaye ni Waziri mpya na tangu Wizara hii imeundwa ndio Waziri wa kwanza mwanamke, kwa hiyo, ni Wizara ya kipekee sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba mambo mengi sana ambayo yamewasilishwa na Waheshimiwa Wabunge ni ya msingi sana. Mchangiaji wa kwanza hadi wa mwisho, kama atakavyokuja kueleza mtoa hoja, wote ukiwasikiliza utaona mambo mengi wanayozungumza ni ushauri mzuri ambao unatuelekeza namna bora ya kutekeleza majukumu yetu ili sekta hii iweze kukua na iwe na mchango mkubwa kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli *champion* wa kubadilisha sekta hii ya madini hapa Tanzania ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Yeye ndiyo ametoa uongozi na uelekeo wa namna gani tusimamie sekta hii ili madini ambayo Mungu ametupa yaweze kuwanufaisha Watanzania. Rais wetu ametamani kwa muda mrefu na hicho ndicho anachotaka sisi wasaidizi wake tufanye, kuwasaidia Watanzania waweze kunufalika na rasillimali hizi. Naomba niseme juhudhi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya na sisi chini ya Waziri, Mheshimiwa Angella Kairuki, tutaifanya kwa miyo yetu na nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye michango michache ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo limeelezwa hapa ni kuwasaidia wachimbaji wadogo. Nieleze kwamba, historia ya wachimbaji wadogo Tanzania na Afrika kwa ujumla, ni ndefu sana. Sisi Tanzania wachimbaji wadogo ni wengi sana lakini tunazo changamoto ambazo tumezikuta na hizo ndizo tutakazozishughulikia ili tuhakikishe kwamba wachimbaji wadogo hawa wanakua, wanatoka kwenye uchimbaji mdogo wanakwenda kwenye uchimbaji wa kat; wanatoka kwenye uchimbaji wa kat iwanakwenda kwenye uchimbaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo mtoa hoja amesema kwenye hotuba yake, uchimbaji mdogo ni hadhi ya muda mfupi. Sisi kama Wizara tunatoa msukumo mkubwa kuwasaidia wachimbaji wadogo. Ndiyo maana utaona

tunahama kwenye majina ambayo wachimbaji wadogo kwa miaka mingi wamekuwa wakiitwa; mara wanaitwa wavamizi, wasio halali, wachimbaji haramu na majina mengine mabaya. Tunatamani tuwaone wachimbaji wa Tanzania wale wadogo wanakuwa wachimbaji ambao wanarasimishwa, wanachimba kwa kufuata sheria, wanachimba katika mazingira ya kutunza mazingira ili madini wanayochimba yaweze kuwa na manufaa kwao wenyewe na watoto wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tumeuona. Kuna watu wengine wanadhani wachimbaji wadogo ukiwasaidia hawana tija. Tulikwenda Mundarara, Jimbo la Longido kwa Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, tumekuta Wamasai kule ni wachimbaji wadogo wa *rubyna Mbunge* wa Longido naye amesema hapa; wamefanya maendeleo makubwa, wamejenga nyumba za kisasa, wamehama kwenye matende, wanaishi maisha mazuri. Tulipofanya mkutano pale wote wanafurahia kuona kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inawapa fursa ya kunufaika na rasilimali zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii si nguvu ya soda, tutaifanya kwa nguvu zetu zote. Ndiyo maana kila mahali mnapotuona tunakutana na wachimbaji wadogo; kazi kubwa tunayoifanya ni kuwatia moyo na kuwapa miongozo ya Kiserikali namna gani watende kazi zao kwa uadilifu na walipe kodi za Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii, sisi kama Wizara, sisi kama Serikali ya Awamu ya Tano kazi yetu itakuwa hiyo; kuwalea, kuwasaidia na kuwahamisha wachimbaji wadogo kwenye uchimbaji wa kubahatisha na kuwapeleka kwenye uchimbaji wa uhakika ili waweze kujikwamua kimaisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyozungumzwa hapa ni habari ya *STAMICO* na kwa sababu tuko wengi wenzangu watakuja kuzungumza hapa lakini mimi nieleze eneo moja la madeni ya *STAMIGOLD*.

STAMIGOLD ni kampuni iliyoanzishwa na Shirika la Taifa la *STAMICO* na ikarithi mgodi mmoja wa Tulawaka. Shida tuliyopata pale ni suala la *management*. Watu wamekwenda pale bahati mbaya sana baada ya kufika pale wametengeneza utaratibu kana kwamba tayari wamekwisha ku-*break even*. Wamejilipa mishahara mikubwa, wameweka gharama kubwa za uendeshaji, wazabuni wamefanya *tendering* kwa bei kubwa sana, imetokea sasa mgodi ule hauwezi kutengeneza faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu pamoja na mambo mengine tumechukua hatua tisa za kwanza za kufanya. Moja, kuhakikisha kwamba tunabadilisha *management* yote ya *STAMIGOLD* na kuweka *management* ya watu ambao ni waadilifu. Pili, tunatafuta wazabuni ambao bei zao ni bei shindani, bei nafuu, bei za soko. Tunataka tuhame kwenye *exaggerated price* twende kwenye bei ambazo ni halisi za soko na hili jambo tunalifanya kwa nguvu zote. Kwa mfano, kwenye mzabuni anayetupatia mafuta tumempata Puma ambaye bei yake anayotuuzia ina upungufu wa Sh.159, lakini zamani ungeweza kuona kwamba bei ya mafuta tuliyokuwa tunanunua ilikuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge watuamini, Wizara hii ni mpya tunafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba hatuliangushi Bunge hili na zaidi sana hatumuangushi Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote ambao wameiamini Serikali ya CCM iweze kuwaongoza. Naomba niwaombe mtupe muda, kuna kazi kubwa tunaifanya kwa *STAMIGOLD*, baada ya muda mtaona mabadiliko na matokeo makubwa kama ambavyo mmeshauri. Naomba niseme kwamba ushauri wa Waheshimiwa Wabunge juu ya *STAMICO* na *STAMIGOLD* tunauchukua na hatupuuzi ushauri wa aina hata mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine imezungumzwa juu ya kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kufanya utafiti. Hapa nataka nitoe mfano mmoja kwa hoja ya Mheshimiwa Kanyasu, Mbunge wa Geita ambaye

alizungumzia habari ya utafiti wa *GST* kwenye Wilaya ya Bukombe ambako na yeye ana wananchi wake wanachimba kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba utafiti uliofanyika kule Bukombe ni wa awamu ya mwanzo, lakini kuna utafiti unaotakiwa kufuata amba ni *geochemistry*, tulikuwa hatujawahi kuufanya; tumefanya *geophysics*, tukimaliza tunakwenda kwenye *geochemistry* ili tuweze kujuu miamba iliyoko pale ina madini ya namna gani na yenye dhahabu kiasi gani. Namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira baada ya muda tukipata fedha tutapeleka *GST* waende wakakamilishe utaratibu ule walionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nachuma amezungumza mambo mengi juu ya Kamati, kwamba Kamati ya Tanzanite ya Mheshimiwa Spika iliyoundwa hapa ilikuwa na mapendekezo mengi haoni matokeo. Naomba nimhakikishie, kama ambavyo Mheshimiwa mtoa hoja alivyotoa kwenye hotuba yake, dira yetu pamoja na mambo mengine ni pamoja na hizo taarifa za Mheshimiwa Spika. Naomba nimhakikishie na kwa uhakika kabisa, mapendekezo yote ya Kamati zote zilizoundwa, kuanzia zile za Mheshimiwa Rais pamoja na za Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tumezitengenezea *matrix* na *time frame* ya kuweza kuzitekeleza, hata hiyo *One Stop Centre* nayo tunajenga ndani ya ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la tanzanite hatuna mzaha, tunatamani kuona madini haya yanawafurahisha Watanzania. Tutoke kwenye aibu ya kuona madini haya yanapatikana kwenye nchi nyingine na hapa Tanzania sisi tunakuwa wageni. Naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii tunaifanya na tumeshaanza na tuko mbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata haya mabadiliko, mimi nilidhani wakati huu Mheshimiwa Mbunge angetupongeza na angempongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu moja ya

mapendekezo yaliyokuwepo ni kujenga ule ukuta, ameona tumeujenga. Tunakwenda kwenye hatua nyiningine ya udhibiti, tunakwenda kwenye kuhakikisha kwamba tunakuwa na eneo moja la kuuzia madini hayo ili kila mtu anayechimba madini yale aseme nina madini ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kudhibiti madini, moja ambayo ni ya msingi sana ni kuondoa urasimu, hutakimbiza mwekezaji lakini la pili ni kupigana na rushwa, uondoe rushwa kwenye mfumo. Ndiyo kazi ambayo Mheshimiwa Angella Kairuki anahangaika nayo kwenye hii Wizara. Bahati nzuri wafanyakazi wetu tunakubaliana kwamba tuna wajibu wa kujenga *image* ya Wizara yetu kwa kufanya kazi kwa nguvu lakini kuwaondolea urasimu watu wanaohitaji huduma ofisini kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna jambo anahitaji mtu kulipata leo mpe leo kama amekidhi vigezo, hakuna sababu ya kumwambia njoo kesho wakati anastahili kupata ili utengeneze mazingira binafsi. Hili jambo tutapigana nalo kwa nguvu zote na kwa hili hatutaangalia mtu usoni. Tunataka Mtanzania yule mwenye haki apate haki yake, tunataka Mtanzania anayekuja Ofisi yetu ya Madini asiwe na mazingira ya aina yoyote ya kuomba rushwa au kiashiria, hata kukonyezwa tu kwamba mtu anataka rushwa, tunataka kuondoa hali hiyo. Tupeni muda, tumejipanga, Waziri wetu anatupa maelekezo kila siku. Sisi watendaji, Katibu Mkuu na Tume ya Madini tutafanya kazi hii kwa nguvu zetu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Alhaj Bulembo amezungumza habari ya wachimbaji wadogo kuwapatia leseni, hili ndilo jambo tunalolifanya. Kila mahali kunakotokea *rush* tukawakuta wachimbaji wadogo, tukiangalia tukakuta hakuna leseni ya mtu kazi ya kwanza tunayoifanya na tunawashirikisha Waheshimiwa Wabunge, tunawarasimisha wale wachimbaji wadogo waliogundua hayo madini ili wachimbe kihalali, watoke kwenye uchimbaji wa kubahatisha wawe na nyaraka ili mtu ye yeyote akija kuwaona akute ni watu halali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya hayo mambo maeneo mengi na Mheshimiwa Alhaj Bulembo angekuwepo ni shahidi, kule alikokuwa anazungumzia Geita tumerasimisha, ukienda Nyakavangala kule Iringa tumerasimisha, hata Mundarara, kule alikozungumza Mheshimiwa Kalanga na kwenyewe tunawarasimisha. Lengo ni kuhakikisha kwamba wanafanya kazi katika hali ambayo ni rasmi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joel ameeleza habari ya *CSR*kwenye jimbo lake na kwenye ule Mgodi wetu wa Itiso ambako wanachimba *dimension stones*. Nimekwenda mwenyewe Itiso, kampuni ile inafanya kazi kubwa, ina *deposit* kubwa ya mawe, tena yenye gharama kubwa na wao tuliwaambia na wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule Itiso kampuni hii imewachimbia maji wananchi, wanapata maji ya kunywa, lakini imekuwa ikitoa michango mbalimbali kwenye jamii. Lengo ni kurudisha huduma kwa wananchi ili kupata kile kitu kinachoitwa *license on operation*, upate kukubalika kwa wanajamii ili wakati unafanya kazi yako iwe rahisi kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo llingine ambalo limezungumzwa hapa ni jambo ambalo Mheshimiwa Ndassa amelieleza. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Ndassa, ye ye anawatetea wachimbaji wakubwa na wawekezaji. Mimi niseme, Serikali ya Awamu ya Tano nia yake ni kuhakikisha kwamba wawekezaji wote wenye nia njema ya kuja kuwekeza Tanzania kwa hali ya *win-win situation* wanakaribishwa milango iko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, mimi toka nimeteuliwa ukikaa pale ofisini wawekezaji wanaokuja ofisini kuomba *appointment* waweze kuzungumza mambo ya uwekezaji ni wengi huwezi kuwaliliza. Ndiyo maana kuna Mbunge mmoja amesema tunakaa mpaka saa mbili usiku, si kwamba tunakaa tunaangaliana, hapana, tunakutana na wawekezaji wa kila namna. Tunachotamani kukiona kwenye Wizara yetu na

wawekezaji wetu, wawe wawekezaji ambao ni *genuine*, si wawekezaji wajanja wajanja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji ambaye anakuja kwetu hana hata mtaji anataka kuja kutumia rasilimali za Tanzania kutafuta mtaji kisha awekeze hapa, hao hawana nafasi. Mwekezaji ambaye amejipanga kuja kufanya kazi Tanzania tunamkaribisha, tunatamani uwekezaji wa fedha za kigeni ndani ya nchi na hii ndiyo dira ya Mheshimiwa Rais wetu, tunataka tuwaone Watanzania wanafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye Mgodi wa Magambazi nini kilichotokea? Pale kulikuwa na wachimbaji wadogo zaidi ya 5,000, wale wachimbaji wadogo wamechimba wametengeneza marudio lakini ile leseni ilikuwa ya mtu mwingine, tukawaondoa wachimbaji wadogo wampishe mchimbaji mkubwa mwekezaji. Bahati mbaya kumbe yule mchimbaji mkubwa ye ye hakuwa na huo mtaji wa kuwekeza pale, ye ye akaja kuchukua yale marudio ya wananchi anachenjua hayo anapata pesa. Sasa hatuwezi kutumia nguvu ya Watanzania kwa ajili ya mwekezaji wa kigeni kwa kigezo kwamba eti ni mwekezaji. Hawa ni Watanzania wametumia nguvu yao, wamesaga mawe, wametengeneza marudio, kama ni mchimbaji kweli akachimbe naye kama wao walivyochimba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetuma timu ya kwenda kukagua kule, wametuletea mapendeleko, zaidi ya sheria 19 zimevunjwa, sasa tunampa maelekezo namna gani afanye ili aweze kutekeleza sheria yetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ndassa Wizara yetu iko tayari kumsaidia mwekezaji ye yote ambaye yuko tayari kufuata sheria. Kama kuna mwekezaji mwingine ye yote, sio wa Magambazi tu, wa pande kuu nne zote za Tanzania ambaye anadhani anaweza kuja Tanzania na *briefcase* bila mtaji akaupata hapa akarudi kwao akiwa tajiri, zama hizo zimepitwana wakati. Tunataka mtu aje awekeze mtaji, tumsaidie sisi apate leseni na ye ye apate kitu cha kuacha hapa kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie tena kukushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini nirudie kusema namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonipa, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyoendelea kutufundisha kufanya kazi. Ni bahati mbaya tu Mheshimiwa Waziri amekaa nyuma, nilitamani niseme maneno haya ninamuona ilia one sura yangu inachokisema ninakusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Nadhani sasa umeridhika, umemuona. Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO): Mheshimiwa Niabu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na fadhila kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu ikiwa ni mara yangu ya kwanza kabisa kusimama ili kujibu hoja za Wabunge wa Kamati yetu ya Nishati na Madini katika hotuba yetu ya kwanza kabisa ya kuomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha kupitisha bajeti ya Wizara hii mpya ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kuniamini na kunitfea kuwa msaidizi wake kwa kunipa majukumu ya kuwa Naibu wa Waziri wa Madini ambapo Wizara hii ni mpya na yenye majukumu mazito ya kulinda rasilimali hii muhimu kwa nchi yetu. Napenda kumhakikisha Rais wangu na Watanzania wote kuwa nitakuwa mwaminifu na mchapa kazi mkubwa, nitatumia uwezo wangu, nguvu zangu, uaminifu wangu, uadilifu wangu kusimamia na kuongoza sekta hii muhimu na bila kumuangusha Rais wangu na Watanzania wote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipayende kumshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki kwa ushirikiano na maelekezo anayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii mpya. Kipekee, namshukuru sana Mheshimiwa Kairuki maana yeye amekuwa ni mtu muhimu sana kwangu kwa jinsi anavyonipatia mbinu na maarifa ya kuongoza na kujiamini katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii muhimu na yenye changamoto nyingi. Mheshimiwa Kairuki siyo mtu wa kujivuna kama mnavyomuona hapa ni mchapakazi na asiye mchoyo wa kukupa ujuzi na uelewa wa mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kunisaidia maarifa ya kutatua changamoto zinazotukabili katika Wizara yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko pacha wangu, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu mwenzangu wa Wizara ya Madini. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuongezea nguvu katika Wizara yetu kwa kutambua uwezo usiokuwa na mashaka wa Mheshimiwa Doto Biteko. Basi ni uhakika kuwa changamoto na majukumu ya Wizara hii yenye changamoto nyingi sasa kwa umoja wetu, kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Simon Samwel Msanjila ni hakika kuwa tutaendelea kusimamia vizuri sekta hii na bila shaka yoyote tutaendelea kuhakikisha tunatekeleza llani ya chama chetu Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niwashukuru sana familia yangu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutimiza majukumu yangu. Kwa kweli wanani umilia sana kipindi napokuwa sipo nao katika kutimiza majukumu yangu ya kulitumikia jimbo langu na Taifa langu kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa kipekee kabisa napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo Maswa Mashariki, kwanza kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. Nina imani kuwa hawakukosea kunichagua na ninawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa kila hali na mali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendelee kuwashukuru sana kwa kunivumilia kuwa mbali nao pindi napokuwa katika kutekeleza majukumu yangu ya Unaibu Waziri wa Madini. Napenda kuwaahidi kuwa nitaendelea kuwa nao katika kuhakikisha Maswa yetu inaendelea kupata maendeleo kadri tunavyotarajia na mambo mazuri zaidi wategemee yanakuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na hotuba hii, napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wangu aliyoleta katika Bunge lako Tukufu. Baada ya kusema hayo, naomba sasa niendelee kwa kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza pindi Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakichangia bajeti hii ya Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamechangia na wamechangia vizuri sana. Kamati ya Nishati na Madini nayo imetoa mapendelekezo yake, Wabunge waliochangia, wamechangia wengi kwa mdomo na wengine wamechangia kwa maandishi, napenda kuwaambia kwamba tunesoma maandishi yote na tumeona mawazo yao mazuri. Tunapenda kusema kwamba tutaendelea kuchukua ushauri wao na kuweza kuutendea kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru AG kwa maneno mazuri aliyojatoa leo, kwa *lecture* nzuri aliyatupatia, katueleza historia nzuri ya sheria za madini. Kwa kweli kila mmoja aliyesikia ameweza kuona tunatoka wapi na sasa tunakwenda wapi katika kusimamia hii sekta yetu muhimu kabisa ya madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye naye ameellezea vizuri kuhusu mikataba na leseni ambazo kwa kweli toka siku za nyuma jinsi zilivyokuwa zikitukandamiza na mikataba mbalimbali ambayo ilikuwa inakandamiza maslahi ya nchi yetu. Ameelleza vizuri, ametusaidia kutupa somo zuri ambalo kwa kweli kila mmoja aliyesikia ameweza kuelewa

na kuona ni jinsi gani tunavyoenda sasa kusimamia rasilimali yetu hii ya madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamechangia, tumepata pongezi nyingi sana, mimi Naibu mwenzangu pamoja na Waziri wetu. Napenda kusema kwamba kwa pongezi mlizotupa mmezidi kutupa chaji/betri ya kuweza kufanya kazi kwa moyo kwa sababu tunaona ni jinsi gani mmeridhika na kazi tunazozifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingine iliyokuja ni jinsi gani Wizara yetu imeongeza kukusanya maduhuli. Tumeweza kukusanya maduhuli kupita kiasi ambacho kilikuwa kimepangwa, mpaka sasa hivi tuna zaidi ya 130% ya makusanyo ya maduhuli tuliyoyakusanya. Tumeweza kufanikisha kwa sababu kwanza kabisa tumeweza kurekebisha Sheria yetu ya Madini ya mwaka 2017 ambapo tumeongeza kiasi cha mrabaha kwenye madini ya metali pamoja na madini ya vito ambapo sasa tunakusanya 6%. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo yameongeza na kwa kweli hii inatia moyo tutaendelea kufanya kazi hii ya kukusanya maduhuli kwa sababu Wizara yetu *typically* kazi yake ni kukusanya maduhuli. Tukishakusanya maduhuli haya tunapeleka katika Mfuko Mkuu na wenyewe utapeleka fedha kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo na kuweza kuleta maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wameongea mambo mengi naweza nikachambua moja baada ya lingine na siwezi kumtaja kila mmoja. Wengi wameongelea kuhusu tafiti mbalimbali ambazo kwa kweli ziko chini ya Taasisi yetu ambayo tunaiongoza katika Wizara yetu ya Madini yaani GST - *Geological Survey of Tanzania*, wameongea kwa kirefu. Kwa ujumla inaonekana kabisa GST wanahitajika kufanya kazi kubwa ya kufanya tafiti mbalimbali ili tuweze kuwasaidia wachimbaji wetu kuwapa taarifa mbalimbali za kijiolojia waweze kuchimba maeneo ambayo yana tija, yenye *deposit* nyingi ya madini, waweze kutumia fedha au mitaji yao kwa

kuchimba maeneo ambayo wanaweza wakachimba kwa kupata faida ili waweze kupata fedha ambazo kwa kweli zitawasaidia katika kuinua uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika *GST* mambo mengi yameongelewa kwamba tafiti wanazofanya ni zile za awali. Wabunge wengi wamependekeza kwamba tuende mbele, *GST* iwezeshwe fedha waweze kufanya tafiti ambazo zinaweza kuona kiasi gani cha madini tuliyonayo ili iwe rahisi sasa tunapokwenda kumpatia mtu leseni, aidha, tuuze leseni kwa njia ya mnada hapo baadaye kwa kuona kabisa kwamba tuna *deposit* ya uhakika, mwekezaji anapokuja ikiwezekana tumuuzie leseni ambazo tuna uhakika kuna madini kiasi gani. Hiyo itatuwezesha kupata wawekezaji ambao kwanza watanunua pengine kwa mnada na watakapoweza kununua itakuwa na tija na sisi tutakuwa tuna uhakika kwamba anaponunua kwenda kuchimba tuna uhakika atachimba kwa kiasi gani na sisi Serikali tutapata kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yameongelewa kuhusu *STAMICO*. Mheshimiwa Waziri wangu atakuja na ataeleza msimamo uliopo kuhusiana na *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni kwamba kuna madeni mengi katika Migodi ya Buhemba na Kiwira. Madeni hayo mengine yalikuwa makubwa, Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu ameeleza kuhusu madeni ya *STAMIGOLD*. Kuna madeni ambayo yalikuwa ni makubwa mno ambayo kwa kweli tulikuwa tunaona yana *forgery* lakini sasa tutatuma timu kwenda kuhakiki madeni hayo na tukishakupata uhakika wa madeni hayo basi Serikali itakapopata fedha itahakikisha kwamba inawalipa wale ambao wanadai wakiwemo wafanyakazi na wale watu ambao walikuwa wamechukuliwa maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge wameongea kuhusu vifaa duni kwa wachimbaji. Napenda kusema kwamba bado Wizara yetu ina kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunawasaidia wachimbaji wetu kwa

kuwapa elimu lakini kuangalia namna ya kuwawezesha kupata mitaji na kuweza kupata vifaa vyta kisasa ili wachimbe kwa gharama ndogo waweze kupata *return* kubwa na wao itakuwa imewasaidia katika kuijendeleza katika miradi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusu mikopo, ni kweli kabisa wachimbaji wengi hawana sifa ya kukopeshwa na mabenki yetu. Wanapokwenda kukopa benki, benki haziko tayari kuwapa fedha kwa ajili ya ku-*rise* mitaji yao ni kwa sababu hakuna taarifa za uhakika, hakuna taarifa zinazoonyesha kuna *deposit* kiasi gani. Hivyo basi, sisi kama Wizara kwa kushirikiana na *GST* tunaangalia namna bora ya kufanya tafiti vizuri kuweza kuona *deposit* zenye uhakika. *Deposit* hizi pamoja na ripoti za *GST* ziweze basi kutumika kupeleka benki na kuweza kuwa-*identify* kwamba huyu mtu anaweza akakopeshwa kiasi fulani na atakachokopeshwa basi benki inakuwa na uhakika kwamba huyu mtu atarudisha na huyu mtu atabaki na fedha kwa maana ya kupata faida zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya madini pia yameongelewa. Kwa kweli tunakwenda kuijandaa kutafuta masoko ya madini mbalimbali yakiwemo madini ya vito, dhahabu na madini mengineyo. Tunaangalia namna bora ya kuweka masoko, ikiwezekana katika madini ya dhahabu basi tuanze walau na masoko ya kila mkoa watu waweze kuchenjua madini yao, wapeleke sehemu, wanunuzi wafike pale, waweze kununua madini na Serikali tutakuwa pale na tutawapa *support* ya kutosha. Pia Serikali tutakuwa imara kusimamia kuweza kupata kodi yetu na sisi kuwapa *export permit*, kuwapa urahisi na kupunguza ile *bureaucracy* ya kupata *export permit*. Kwa hiyo, tuko tayari, tumejipanga na tutahakikisha kwamba kila mkoa tutaweza kuwawekea mazingira ya kuanzisha soko la madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yameongelewa na Waheshimiwa Wabunge ikiwemo kodi. Ni kweli kabisa kuna kodi zingine ni nyingi, kwa mfano, kwenye dhahabu kuna kodi nyingi ambazo pengine baadhi ya

wachimbaji wanashindwa ku-comply na kodi hizo. Tutaendelea kutoa elimu ya kodi, tutaendelea kutoa elimu ya kulipa mrabaha (*royalty*) ili wachimbaji waweze kuzifahamu kodi hizo, waweze kutunza nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kodi ili kuweza kuwapa unafuu na kuweza kujikinga na kutozwa kodi mara mbili mbili yaani *double taxation. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano *withholding tax* mtu anapolipa anashindwa kuweka risiti, anapokwenda kutoa madini yake ku-export *TRA* wanamchaji tena, wanapomchaji tena analalamika kwamba anachajija mara mbili. Hii ni kwa sababu watu hawa wengine wanakosa ile elimu ya kutunza nyaraka. Tunaangalia namna bora ya kuondoa kodi kero lakini wakati huohuo tutaendelea kutoa elimu ya mlipa kodi kwa wachimbaji ili kodi hizo zisiwe mzigo kwao, waweze kufanya biashara vizuri na waweze kupata faida katika biashara hiyo ya uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yameongelea kuhusu mikataba, Mheshimiwa Waziri wa Katiba hapa ameелеza kuhusu mikataba mibovu. Suala hili limeelezewa kwa namna mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge wameongea vizuri sana. Kwa somo la leo, nina hakika kabisa kwamba wameweza kupata somo la uhakika kwa maana ya kwamba uwelewa utakuwa umeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema sisi pamoja na Wizara yetu tutaendelea kujipanga kama walivyopendekeza Waheshimiwa Wabunge tuwe na semina za mara kwa mara ili kuweza kuwaelimisha Waheshimiwa Wabunge kuhusu kodi mbalimbali, mikataba mbalimbali pamoja na shughuli za uchenjuaji wa madini kama vile tulivyofanya katika maonyesho ya madini tuliyoyaleta. Kwa maonyesho haya, watu wamejifunza, wengine walikuwa hawajawahi kuona tanzanite, kwa mara ya kwanza Waheshimiwa Wabunge wameona tanzanite na dhahabu na jinsi ya ku-process madini hayo. Mungu akitujalia tutaendelea kutoa elimu zaidi kwa Wabunge waweze kupata ufahamu na tunapoingia katika Bunge lako watu wawe

wanachangia kitu wanachokifahamu na iwe rahisi kuweka michango mizuri na kupata ushauri mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya mwaka 2017 imezuia ku-*export raw minerals* yaani madini ghafi. Watu wa Mundarara, Mheshimiwa hapa Kalanga amezungumzia, tulikwenda kule Mundarara tukaenda kutoa ahadi kemkem. Ahadi mojawapo ilikuwa ni kwenda kuwaeleza kwamba sheria hii na mabadiliko yake siyo mzigo kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli *raw minerals* zimezuliwa kutoka lakini tunaangalia namna ya kuja na mwongozo bora na wa kitaalam ambao utaweza kuonyesha tutaweza ku-*process* madini yetu katika kiwango gani na kile kiwango ambacho kinakubalika ku-*export*. Tutakapoleta mwongozo huo basi kila mchimbaji ataweba ku-*comply* na sheria hiyo na itakuwa siyo mzigo tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi watu wa Mundarara niwaeleze kwamba wasiwe na wasiwas, ahadi tulizowapatia ziko pale pale, tutawaleta mwongozo wataendelea kuchimba kwa faida kubwa. Kama alivyosema Naibu mwenzangu pale Mundarara wamejenga nyumba nzuri na majengo mazuri, kwa kweli hali ya pale ukifika unaona kabisa fedha inayotokana na machimbo inakuwa na tija katika jamii inayowazunguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumziwa suala la *CATA Mining*. *CATA Mining* ni mgodi wa mchimbaji wa katil ulio katika Mkoa wa Mara. Huyu mchimbaji alikuwa na leseni sita yaani *Primary Mining Licences* ndani ya eneo la jeshi. Watu wamesema kwamba kuna mgogoro, Waheshimiwa Wabunge niwahakikishie hakuna mgogoro katika mgodi ule. Sasa hivi tumewashauri kwamba wakae na Jeshi la Wananchi Tanzania waelewane, Jeshi la Wananchi Tanzania lina ile *surface right* yaani anamiliki ardhi ya juu, yule mchimbaji amepewa leseni ya kuchimba pale kwa maana kwamba yeye ana *mining right*, kwa maana ana haki ya kuchimba pale, sasa wao wakae kwa pamoja na wamekwisha

kuelewana, sasa hivi ule upande wa pili ni kwamba zile *Primary Mining Lisences* zao sita zitakwenda kuunganishwa na kupata kitu kimoja ambacho tunaita *Mining Lisences*. Hiyo *Mining Lisences* itakuwa chini ya kampuni inaitwa CATA *Mining* yaani kampuni ya Mtanzania mmoja anayemiliki 50% na Mkanada anayemiliki 50%. Kwa umoja wao wataingia mkataba na Jeshi la Wananchi ili waweze kuchimba haraka na iwezekanavyo. Kwa kweli tunaona mgodi huu una *potential/kubwa* kwa wananchi wa maeneo hayo, wananchi zaidi ya 400 ajira zao ziko pembedi, wameshindwa kufanya kazi kwa sababu mgodi huo umesimama wakisubiri mikataba hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawahakikishia kwamba mgodi huo baada ya kupata *Mining Lisence* wataanza operesheni, wananchi wa maeneo hayo wataweza kupata ajira. Vilevile sisi kama Serikali tutaendelea kupata kodi kutoka katika mgodi huo ili nayo iweze kupeleka kwa wananchi kwa ajili ya kuwaletea maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengine Waheshimiwa Wabunge wameyaongea, wameongea maneno mazuri, Mheshimiwa Kanyasu ameongea, kuna Wabunge wengi hapa wameongea na mzee wangu hapa Mheshimiwa Mwambalaswa katupa hongera nydingi. Kwa kifupi, kuna malalamiko ya kuchanganya leseni, unakuta kuna leseni ya utafiti na watu wengine wameomba leseni za kuchimba madini ujenzi. Wizara yetu tutaendelea kuahakisha kwamba tunawapa leseni hizo watu waweze kuchimba madini ujenzi na tuna hakika kwamba yatawasaidia wananchi kupata *material/ya kuweza* kufanya ujenzi katika maeneo yao, vilevile sisi Serikali tutapata marahaba kutoka kwenye madini ujenzi na kuongeza maduhuli katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niendelee kukushukuru wewe na Bunge lako Tukufu, niwashukuru Wabunge kwa mawazo na maneno ambayo wametupa toka jana yametupa afya njema kwa sababu tumeona kwamba kweli Bunge letu lina upendo. Bila kujali

upande wowote, wametoa mawazo mazuri na wametupa hongera nzuri. Mawazo yao waliyoyatoa tunayachukua, tutaendelea kufanya kazi kwa uhakika na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunafuata ushauri wanaotupatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda tena kusema kwamba naunga mkono hoja hotuba ya Waziri wangu wa Madini, Mheshimiwa Angellaah Jasmine Kairuki. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Madini, mwenye hoja yake. (*Makofi*)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kipekee kabisa kukushukuru kwa kunipa fursa hii kuweza kuhitimisha hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote takribani 65 ambaa waliweza kuchangia, kwa kuongea walikuwa 26 na kati yao 39 waliweza kuchangia kwa maandishi. Kwa hakika kwa niaba ya Wizara ya Madini tunawashukuru sana kwa michango hiyo mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kipekee kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Rais wetu mpwendwa, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kwa kunipa nafasi hii ambayo kwa hakika ni heshima kwetu. Niendelee tu kumhakikishia mimi pamoja na Naibu Waziri wangu; Mheshimiwa Nyongo pamoja na Mheshimiwa Biteko kwamba hatutamwangusha na tutahakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi na ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Biteko. Kwa hakika kama nilivyosema wakati nawasilisha hoja hii wamekuwa ni watu wa msaada sana kwangu. Nilieleza kwa

takribani miezi mitatu sikuwepo, wamefanya kazi kubwa lakini pia wanaendelea kufanya kazi kubwa, kwa kweli ninajivunia kuwa nao kama Naibu Mawaziri wangu. Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na niwahakikishie kwamba nitakuwa wazi kwao, tutaendelea kushirikiana wakati wowote watakapohitaji mwongozo wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Prof. Kabudi, tumekuwa tukishirikiana sana katika suala hili la usimamizi wa sekta hii ya madini hususani katika suala zima la majadiliano ya mikataba. Napenda kumshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Kilangi kwa namna ambavyo anaendelea kutushauri kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutupatia Miongozo mbalimbali na tafsiri na fafanuzi katika masuala ya kisheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wahenga walisema tunahitaji mikono, jicho na mdomo wa kila mwanakijji kuweza kumlea mtoto mmoja kwa mafanikio. Kwa hakika hivi ndivyo ilivyo kwa Wizara hii mpya ya Madini. Katika upya wetu tunahitaji sana mchango wa maoni, mapendelekezo, ushauri wenu kukosolewa na kila Mheshimiwa Mbunge pale ambapo mtakapoona kuna haja ya kufanya hivyo. Sisi tunaamini kwa kufanya hivyo, hiyo hiyo ndiyo njia pekee ya kuweza kuimarisha Wizara yetu hii mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mwaka jana upande wa sekta ya madini wachangiaji hawakuwa wengi sana lakini nilikuwa nafurahi sana kila ambavyo nilikuwa naona Mbunge anasema mpaka tumefikisha Waheshimiwa 65 kwa maandishi na mdomo, tunawashukuru sana sana. Napenda kipekee kuwashukuru wote walioweza kuchangia hoja hizi, mmetuimarisha sana na napenda kutoa shukrani za dhati kwa michango mizuri ambayo mmetupatia. Niwahakikishie kwamba tumeipokea, tumefaidika sana na niwaahidi tu kwamba tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajibu hoja chache lakini kwa zile ambazo nitaweza kuzijibu niwahakikishie kabla ya Bunge letu hili halijaweza kuhitimishwa tarehe 30 Juni

tutaweza kuwasilisha majibu yote kwa maandishi kwa kila Mheshimiwa Mbunge kwa namna alivyochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ambacho kinanipa faraja mimi na wenzangu ni kwamba sisi na Waheshimiwa Wabunge wote tunazungumza lugha moja na sote tunavuta katika upande mmoja wa kutetea maslahi ya Watanzania wenzetu. Sote tunaamini kwamba sekta ya madini itakaposimamiwa vizuri, tutaweza kuvuna zaidi ya kiasi cha madini tunachokivuna hivisasa. Zaidi kwa ujumla wetu tunao, muafaka sote kwamba wananchi wetu ndiyo wenyewe kustahili kufaidika zaidi na rasilimali ya madini waliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu. Pia tunakubaliana kimsingi kwamba wakati ndioyo sasa na sisi ndiyo wale historia imetukabidhi jukumu na wajibu wa kuliwezesha hili. Naamini, madamu tunakubaliana katika haya ya msingi basi hakuna kwa hakika lilitakaloharibika. Kwa lugha ya leo tunaweza kusema yajayo yanafurahisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano iko bega kwa bega na Bunge lako Tukufu katika kusimamia rasilimali ya madini ya nchi yetu. Ni kwa msingi huo Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Madini ambayo Waheshimiwa Wabunge mliweza kuipitisha pamoja na Kanuni mpya nilizozitunga mwaka huu wa 2018. Niwahakikishie tena Waheshimiwa Wabunge tangu mabadiliko ya Sheria yalipofanyika, kampuni mbalimbali za madini za ndani na nje ya nchi zimeonyesha nia ya kuwekeza katika sekta ya madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kufuatia kuundwa kwa Tume mpya ya Madini tunatarajia kwamba maombi ya leseni kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya madini yatashughulikiwa mapema ipasavyo. Vilevile kama Serikali tumeanza kutekeleza mpango wa kujenga uwezo wetu wa kuhakiki mitaji inayowekezwa na shughuli zinazofanywa na kampuni za madini. Nia yetu kubwa ni kuwa na uwezo wa kuhakiki taarifa za kampuni kuhusu uwekezaji wao na shughuli zao. Napenda kuwahakikishia kwamba sisi kwa upande wetu kama Wizara hatatalala, tutakuwa macho na tutaendelea

kuchukua hatua kila mara itakapobidi. Nachoomba Waheshimiwa Wabunge kutoka kwenu ni mambo mawili. La kwanza, ni imani na ushirikiao wenu katika kutekeleza wajibu wetu huu mkubwa. Pili, niendelee kuwaomba kwa heshima na unyenyekevu mkubwa mtupitishie bajeti hii ambayo kwa hakika ndiyo itakayokuwa nyenzo muhimu kwetu ya kutuwezesha kutekeleza azma yetu hii. Haya yote mawili kwa hakika yamo ndani ya uwezo wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, niruhusuni sasa nianze kujibu baadhi ya hoja kama zilivyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwepo hoja ya Mheshimiwa Kanyasu kuhusiana na Mzee wangu Felix Ngowi na wenzake amba wana mgogoro na mgodi wa *GGM*. Kwa kweli ameeleza kwa hisia kubwa na mimi nimesikitika. Hukumu takribani sita zimeweza kutolewa kuhusiana na suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kumhakikisha Mheshimiwa Kanyasu pamoja na Mheshimiwa Musukuma na Wabunge wote wa Geita na wengine wote wenye mapenzi na wanyonge wetu katika Taifa hili kwamba suala hili nitalichukua kwa uzito wa pekee. Kwa kuwa na mimi mwenyewe ni mwanasheria, nitakaa na Mheshimiwa Jaji Mkuu kuweza kuliangalia suala hili limekaaje ili kuweza kulipatia ufumbuzi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja pia kuhusiana na *GGM*, wanapokuwa wanatoa mipango mbalimbali ya uwajibikaji katika jamii au *CSR* kwamba bei kubwa za vifaa zinakuwa *inflated*. Tulielezwa hapa, lori moja la mchanga mpaka takribani Sh.350,000. Napenda kusema tu kwamba hili halikubaliki, niendelee tu kuwaomba Waheshimiwa Madiwani wetu, kupitia kifungu cha 105(1)(2) na (4) cha Sheria yetu ya Madini ya 2010 kama ilivorekebishwa mwaka 2017, kabla hawajaridhia mpango wa mwaka wa uwajibikaji kwa jamii wahakikishe kwamba wamejiridhisha kile kinachoahidiwa katika mpango huo wa

mwaka basi kweli kinaendana na thamani halisi ya fedha. Napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote, tutafanya ukaguzi maalum kupitia Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kuiangalia migodi yote mikubwa katika *CSR* zao ambazo wamekuwa wakizitoa katika jamii zao na kuona kwamba kweli zinaendana na kiasi halisi cha fedha inayoelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuhusiana na ruzuku, wapo wachimbaji wadogo ambao waliweza kunufaika lakini kwa bahati mbaya wapo takribani wanufaika tisa ambao hawakuweza kuwa waaminifu na walizitumia fedha zile vibaya kwa kukiuka mkataba. Napenda tu kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge suala hili tumelipaleka TAKUKURU na tayari uchunguzi wake umefanyika na tunaamini wataweza kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusiana na suala zima la madini ya bati kwa upande wa Kyerwa. Wote tunafahamu tunao Mkataba wa */CGLR* ambapo kupitia mkataba huo, hatuwezi kuuza madini yetu nje ya mipaka yetu bila kusaini Itifaki ile ya *Illegal Exploitation* pamoja na mkataba ule wa */CGLR* kuhusiana na usalama na ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Bilakwate ameeleza suala hili kwa uchungu mkubwa, tunaona hoja hii kwa msingi wake. Kama Serikali tumeshaanza kulifanyiakazi na tuko katika hatua ya mwisho ili kuhakikisha kwamba tunaleta mkataba huu Bungeni ili uweze kuridhiwa na kuruhusu biashara ya bati kuuzwa katika soko la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuhusiana na mgodi wetu wa Buckreef, kwa muda mrefu wabia wetu au wabia wenza wa *STAMICO* wamekuwa wakishikilia mgodi ule lakini wamekuwa hawatimizi kama ambavyo mikataba imewataka. Napenda kuwahakikishia tayari tumeshafikisha suala hili katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na

tunaamini tutaweza kupata tafsiri na miongozo ya namna gani ya kuweza kuachana na mikataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusiana na kukamilisha ujenzi wa *smelter*; Mheshimiwa Mama Nagu, Mheshimiwa mama Mbene, Mheshimiwa Kapufi na wengine wengi wameweza kulizungumzia hili kwa uzito mkubwa. Kama nilivyowaeleza awali, niwahakikishie kwamba tayari tumeshapata waombaji takribani 27 na tunachokifanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunayachambua na kuweza kufanya uchunguzi au *due diligence* ili kuhakikisha kwamba tunampata mwekezaji ambaye kweli anavyo vigezo na ni mahiri katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja za Mheshimiwa Catherine Magige kuhusiana na utoroshwaji wa madini ya tanzanite lakini zaidi alitupa ushauri tuweze kuimarisha mipaka yetu ya Namanga, Horohoro pamoja na mipaka mingine. Nimpahakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufuatilia mnyororo mzima wa uchimbaji, uendeshaji wa biashara hii ya tanzanite pamoja na mauzo nje ili kudhibiti utoroshaji. Pia napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kama Wizara hivi sasa tunaandaa utaratibu imara wa kuweza kuwapatia motisha wananchi watakaoweza kutoa taarifa au *whistleblowers* juu ya watoroshaji wa madini ya tanzanite pamoja na madini mengine. Pia tunaandaa simu maalum au *hotline* maalum ambayo tutaitumia katika kupokelea taarifa kuhusiana na masuala ya utoroshaji na biashara nzima hii ya madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja za Mheshimiwa Ndassa ambaye kimsingi aliweza kutushauri tuweze kuonyesha ni namna gani tunaweza kuwasomesha wathamini wetu wa madini ambao hivi sasa tunao wathamini wachache. Napenda kumshukuru kaka yangu Mheshimiwa Ndassa na nimhakikishie tu kwamba tunalipa suala hili la uthamini wa madini uzito wa kipekee. Tayari tumeshaa inisha au tumeshawatambua watumishi 10 ambao tutawapeleka

kwenye mafunzo katika nchi ya Thailand pamoja na India ili waweze kupata mafunzo maalum ya *gemology* kwa ajili ya kuweza kutambua madini ili waweze kutambua na kufanya uthamini ili tusiweze kuibwa na kuweza kupata fedha stahiki au mirabaha stahiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusiana na kufunga *security system* katika ukuta wetu wa Mererani. Nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Bulembo kwa kuweza kuona umuhimu wa suala hili. Nimpakikishie kwamba ni suala ambalo kwa kweli tunalipa upekee mzito. Ameeleza hapa masuala ya mitobozano na masuala mengine. Nisingependa kueleza masuala mengi ya kiusalama lakini nimhakikishie kwamba hoja na ushauri wake utazingatiwa na tutahakikisha kwamba tutakuwa na mfumo wa ulinzi ambao kwa kweli hapatakuwa na utoroshaji hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Bobali kuhusiana na tozo nydingi katika chumvi pamoja na masuala mengine lakini pia Mheshimiwa Hamida, Mheshimiwa Ngombale na Waheshimiwa wengine, niwashukuru kwa hoja hii. Kipekee kabisa napenda kuwaeleza kwamba nilipata hoja hii kutoka kwa Taasisi yetu ya TASPA ya wazalishaji wa chumvi. Nasi kama Wizara kwa kweli tulilliona kwa uzito mkubwa. Ukiangalia gharama inayotumika katika uzalishaji wa chumvi wanapata faida kidogo sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni takribani Sh.150 peke yake katika kilo 50, Sh.3 kwa kila kilo ni fedha ndogo sana. Hii inatokana na tozo zilizopo katika biashara nzima, wana tozo zaidi ya 16. Tayari kama Serikali, tumeanza mashauriano, tumewasilisha Wizara ya Fedha, kwa upande wetu kama Wizara ya Madini na Wizara ya Viwanda kuona ni namna gani suala hili linaweza likaangaliwa kwa mapana yake ili kuweza kuhamasisha uzalishaji wa chumvi ya Tanzania. Maana yake hivi sasa Tanzania tunayo chumvi nydingi na ukiangalia sekta hii ya chumvi imekuwa ikiajiri akina mama wengi sana lakini tumegeuzwa kuwa soko la nchi nydingine,

tunanunua chumvi ya nchi zingine kwa sababu tu ghamara za uzalishaji zimekuwa kubwa. Napenda tu kusema kwamba tunaomba muweze kutuvumilia katika suala hili, Serikali yetu sikivu, tunaamini suala hili litawenza kupatiwa ufumbuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na pendekerezo la Mheshimiwa Bilakwate kuhusiana na suala zima la uongozi wa *STAMICO*. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumeanza kufanya mageuzi kwa ajili ya uongozi wa Shirika hili la *STAMICO*. Tayari tumeshambadilisha Mkurugenzi Mtendaji, tumeshaanza kubadilisha baadhi ya Wakurugenzi na tutafanya hivyo kila mara itakapoonekana inahitajika. Hoja hiyo pia ilielezwa na kaka yangu Mheshimiwa Bobali pamoja na Waheshimiwa wa Bunge wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa n aibu Spika, illijitokeza pia hoja ya Mheshimiwa Rashid Shangazi kuhusiana na madini ya bauxite kule Lushoto lakini pia alinialika niweze kutembelea eneo hilo. Nimueleze kwamba mimi natoka Same na anajua Same ni jirani na Lushoto, kwa hiyo, kwa hakika kila nikitembelea Same nitahakikisha pia nakwenda Lushoto ili kuweza kujiona maeneo yale ya Makanya, Magamba, Soni pamoja na Malindi lakini zaidi kuwaunganisha wananchi wa Lushoto wale ambao wanayo *reserve* ya bauxite na wawekezaji ambao watakuwa tayari kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ya Ndugu yangu Mheshimiwa Issaay ambaye naye aliweza kutualika. Pia alitoa ushauri wa kuendelea kutoa ruzuku kwa wachimbaji wetu wadogo. Nimpahakikishie tu kwamba suala hili tunaliangalia ili kuweza kupata utaratibu mzuri ambao utaweza kuwanufaisha wachimbaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja nyiningine ambapo Waheshimiwa Wabunge walishauri *STAMICO* iachie maeneo ambayo haiendelezi. Napenda tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tayari kwa upande ule wa mgodi wa Buckreef tumeshaainisha mgodi ule au eneo la Lwamgasa *South II* pamoja na Nyamalimbe *II* na Lwamgasa *West* na

hayo tutaendelea kuyatambua na kuweza kuwatengea wachimbaji wetu wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja pia ya Mheshimiwa Ngalawa ambaye alipendekeza *GST* wajengewe uwezo iliwaweze kufanya utafiti zaidi katika suala hili la uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia kuna hoja ya Mheshimiwa Mussa Mbarouk kuhusiana na Chuo cha Madini kuongeza idadi ya wanafunzi ili kuweza kupata wataalam zaidi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mussa Mbarouk kwa mwaka huu wa fedha tumepata wanafunzi 542 lakini kuanzia Julai tutakuwa na wanafunzi 850 na lengo letu ni kuhakikisha kwamba ifikapo 2019/2020 tunakuwa na wanafunzi 1,350.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi tumeanza mashauriano na Bodi yetu ya Mikopo ili kuona ni namna gani sasa wanafunzi wale wanaosomea cheti na diploma katika sekta ya madini katika Chuo chetu cha Madini na wenyewe waweze kunufaika na mkopo huu wa elimu hiyo. Naenda kuwaalika Waheshimiwa Wabunge, ndugu zenu lakini zaidi wapiga kura wenu waweze kukaribia katika Chuo chetu cha Madini ili kuweza kujifunza katika sekta hii ya madini ikiwemo jiolojia na masuala mengine ya uhandisi na uchenjuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusiana na usimamizi wa ufuatiliaji wa walipa kodi katika sekta ya madini. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutafanya hivyo na tutashirikiana na taasisi zingine ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata kodi zake stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Alhaj Bulembo pia aliweza kutupa ushauri kwa Tume yetu mpya ya Madini ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na zaidi itahitaji ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Seif Gulamali kuhusiana na usafirishaji wa *carbon* kutoka Geita ambapo yeche alitolea mfano *carbon* ambayo

ilikuwa ikienda Mwanza. Nitaomba Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo hili mnisikilize kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya uchenjuaji katika miaka ya 2000, wachimbaji na wachenjuaji wadogo wengi nchini wamekuwa wakitumia kemikali ya *cyanate* kwa ajili ya kuchenjua madini ya dhahabu. Ni kwa kutumia teknolojia hii ya kemikali hii ya *cyanate* waliweza kuchenjua madini ya dhahabu ambayo imekuwa ikihusisha utumiaji wa *vat leaching* pamoja na *activated carbon*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi nisingependa kwenda kwenye utaratibu mzima wa namna ambavyo *vat leaching* hii na *carbon* inafyonza dhahabu lakini napenda tu kusema kwamba, katika suala zima la usafirishaji wa *carbon* kutoka katika maeneo mbalimbali hususani Geita, Singida pamoja na maeneo mengine wamekuwa wakienda katika mkoa jirani au katika mkoa mwingine wa pili kwa ajili ya kufanya uchenjuaji. Napenda tu kusema, kuanzia leo tarehe 1 Juni, 2018 itakuwa ni kosa kwa mtu ye yeyote kusafirisha *carbon* kutoka katika mkoa ambapo mchanga au *carbon* inazalishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika televisheni wale wenye viwanda vya uchenjuaji Mwanza na sehemu zingine wakieleza na mpaka humu ndani wameandika barua yao kwamba suala hili litawakosesha ajira. Kama Serikali napenda kusema kwamba Sheria ya Madini iko wazi na kuanzia leo niombe vyombo vya ulinzi na usalama yeyote atakayekutwa anasafirisha *carbon* kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine achukuliwe hatua kazi za kisheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa suala la ajira, nitolee mfano wa eneo la Geita, miundombinu ipo, barabara zipo, umeme upo na kila kitu kipo, haingii akilini nini kishindikane wachenjuaji wale wenye viwanda vya uchenjuaji kuweka viwanda vyao vya uchenjuaji Geita, Singida, Tanga na maeneo mengine? Ni marufuku kuanzia leo tarehe 1 Juni, 2018, yeyote atakayekamatwa anasafirisha

carbon hiyo kutoka katika eneo moja kwenda lingine hasa mkoja mmoja kwenda mwingine itakuwa ni kosa la jinai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nisisitize hili, lengo hapa ni kuhakikisha tunalinda ajira katika mkoa husika unaozalisha *carbon* ile pamoja na mchanga ule wa madini hususani madini ya dhahabu na mengineyo. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaongeza mzunguko wa fedha na tunadhibiti utoroshwaji wa madini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamekuwa wakitoa dhahabu Geita, Singida kwenda Mwanza na maeneo mengine lakini unashangaa katika *record* zetu Wizara ya Madini huoni *record* za mauzo yale ya madini, huoni *record* za vibali tunavyovitoa vya mauzo ya madini yale nje, huoni *record* ya malipo ya mirabaha na kwa kweli tumekuwa tukipoteza fedha nyngi katika eneo hili. Niombe sana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vihakikishe vinalisimamia suala hili ili kupiga marufuku na kuhakikisha suala hili linafika mwisho na ni imani yangu tutapeana ushirikiano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi niwaombe *TRA* pamoja na Ofisi zetu za Madini kufanya ukaguzi wa kina na *forensic audit* kwa wote ambao walikuwa wakifanya uchenjuaji au walikuwa wana viwanda hivyo vya uchenjuaji na kufuatilia minyororo mizima ya biashara yao hiyo katika viwanda vya uchenjuaji ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata fedha na malipo yake stahiki. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunachochea ukuaji wa uchumi katika maeneo husika ambako michanga hiyo na *carbon* zinazalishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tuone mabenki katika maeneo hayo, huduma zingine zipo, malazi yapo, bidhaa zipo sasa unajiliza, iweje mtu atoe *carbon* Geita aipeleke Mwanza, iweje mtu atoe *carbon* Tanga aipeleke Mwanza? Kwa nini asiichenjue pale au kwa nini asiwezekeze pale? Endapo atashindwa kuwekeza wako wengine ambao wako tayari kuwekeza na wameonyesha nia hiyo. Kwa hiyo,

napenda sana kusitiza eneo hili na ni imani yangu Ofisi zetu za Madini pamoja na vyombo vyetu nya ulinzi na usalama vitalisimamia agizo hili kikamilifu ili kuhakikisha kwamba tunaweza kuona tija na ufanisi katika susla zima la uchenjuaji na sekta hii ya madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwahamasisha wachimbaji wote na wawekezaji watakaoguswa na agizo hili, waweze kujenga mitambo na miundombinu ya uchenjuaji katika mikoa ambayo wanazalisha hiyo *carbon* pamoja na michanga ili kuweza kutekeleza agizo hili ipasavyo. Pia nizitake Ofisi za Madini zishirikishe kikamilifu vyombo vyetu nya ulinzi na usalama ili kuweza kusimamia shughuli za uzalishaji wa madini kwenye maeneo husika. Nipige marufuku kuanzia leo kwa Ofisi zetu za Madini kutoa kibali cha usafirishaji wa *carbon* pamoja na michanga hiyo kutoka katika mkoa mmoja kwenda katika mkoa mwingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja hapa kuhusiana na ruzuku katika awamu yetu ya I na ya II ya SMMRP. Wapo ambao walitaka kujua ni Mikoa mingapi imeweza kunufaika na mikopo hiyo. Napenda tu kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge, ni mikoa takribani 24 yenye wanufaika takribani 115 ndiyo walioweza kunufaika na mkopo wetu wa SMMRP.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mwambalaswa kwa ushauri wake mzuri ambao ameendelea kutupatia kuhusiana na namna ya kusimamia sekta yetu ya madini katika Wilaya yake ya Chunya na katika eneo lake la Itumbi. Kipekee tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mapendekezo yao mazuri pamoja na ushauri. Niwahakikishie mimi pamoja na wenzangu tutayafanyia kazi na wakati wote tutaweza kutii maelekezo yenu na ushauri na tutakapoona tuna changamoto tutaweza kurudi kwenu na tutaomba basi muweze kutuwezesha ili kufanikisha yale tunayoyahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilliona kwa leo nieweze kuyasema hayo. Kwa wale ambao tutakuwa hatujaweza kuwajibu vizuri, tutaomba tuweze kuwajibu kwa maandishi kwa siku za usoni. Kwa kipekee kabisa tuwaombe waweweze kutupitishia bajeti yetu hii ili tuweze kuwa na nguvu kuweza kutekeleza na kusimamia sekta hii nzito ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, kipekee kabisa, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:

Fungu 100 – Wizara ya Madini

Kif. 1001 – *Administration and HRM*.....Sh.4,238,723,888/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Waziri, nimeletewa majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge wanaohitaji ufanuzi wa ziada. Tutaanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia nilizungumzia kuhusu kishika uchumba kile ambacho tumeambibiwa kwamba wale wenzetu wa Acacia walikuwa wameahidi kukitoa cha Dola milioni 300. Leo wakati wa kuhitimisha hoja Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na maelezo mengi aliyyoatoa lakini hakwenda moja kwa moja kwenye hoja ya kwamba, je, pesa hizi tayari zimeshatolewa au bado? Yeye amejikita kuelezea mambo mengine ya madeni kwamba wasingependa yawe wazi sana kwenye jumuiya hasa jumuiya za kimataifa. Nilitaka ufanuzi kutoka Serikalini kwamba pesa hizi ziko katika kitabu gani maana kwenye bajeti hii ambayo tunakwenda kuipitisha sijaona mahali popote inapoonyesha pesa hiyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ufanuzi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufanuzi wa swali lilitolizwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza tarehe 19 Oktoba, 2017 tulisaini na siyo Acacia bali Barrick ambaye ndiye mwenye hisa mkuu katika migodi ya madini ya Bulyankulu, Buzwagi ambao sasa wamesimamisha kuzalisha lakini wanapitia yale mawe waliyoyachimba mpaka mwaka 2020 na North Mara na *Agreement of Undertaking* ulisainiwa na Serikali na Prof. Thornton. Baada ya hapo tulikubaliana nao kwamba kulingana na taratibu za kampuni ambazo ziko katika masoko ya mitaji Toronto na London kuna utaratibu wa ndani ambao watautumia ili hatimaye kutekeleza yale ambayo tumekubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu ilikuwa ni *Agreement of Undertaking* imekuwa inafuatiliwa na uandaaji wa mikataba mingine. Kwa sababu hiyo, tulikubaliana *timeline* kati ya wao na sisi na majadiliano hayo yanaendelea. Tulikubaliana kwamba ifikapo mwisho wa mwezi Juni, tutakuwa tumekamilisha hatua nydingi za kuandaa nyaraka mbalimbali ambazo ni muhimu kwa jambo hili ili

litekelezwe na wao waziwasilishe katika Bodi zao na sisi tuziwasilishe kwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali ili ipate idhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba tayari nyaraka zaidi ya 14 zinazohusika na jambo hili zimekamilika na mbili za mwisho zipo katika hatua ya kukamilika. Baada ya ukamilikaji wote huo, taratibu za malipo hayo zitafanyika. Kama nilivyoeleza malipo hayo yatafanywa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkoo wa Serikali kwa sababu haya siyo maduhuli ya kawaida. Katika majadiliano haya tunayoyafanya na makampuni mbalimbali ya madini tumemaliza na Tanzanite, tutafanya na Geita *Gold, Williamson Diamond* na hata Shanta, tunakuwa na aina mbili ya malipo, yapo yale halali ya Serikali hayo hayana msamaha kwa sababu ni ya kisheria lakini wanapolipa fidia, kwenye fidia ipo ya *goodwill* na ipo fidia ya *compensate and settlement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilieleza kwamba fedha hizi hazionekani kwenye kitabu chochote kwa sababu zina utaratibu wake wa kutumiwa lakini mara zitakapoingia kwenye Mfuko wa Serikali ni mapato ya Serikali na matumizi yake yatapitishwa katika bajeti za Serikali ambazo ndiyo sasa tunazipitisha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba azma iko palepale na tuko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha utekelezaji wa yale tuliyokubaliana ili na wao waweze ku-comply na *regulations* za *London Stock of Exchange* na *Toronto Stock Exchange* ili iweze kutoka kwa sababu kampuni zao ni *public listed*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeridhika kwa sababu nilidhani zimeshalipwa kumbe bado ziko katika mchakato. Nashukuru sana kwa ufanuzi huo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wachangiaji nadhani na mimi tulikuwa tunazungumzia kuhusu kunufaika zaidi kwa nchi na rasilimali hasa kwenye kuongeza thamani ya madini. Nataka nitoe picha moja kwamba madini haya ambayo tunasema kuongeza thamani kila aina inatofautiana na mteja unayempeleke. Kama Serikali pengine ilikuwa ni muhimu kutoa maelekezo kwamba madini ya aina gani wanataka yaongezwe thamani kwa *level*/fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano, niliwahi kuhudhuria *Hong Kong Trade Fair* ukikuta tanzanite hii ya Tanzania namna ambavyo imetengenezwa kwenye *Trade Fair* ile unaweza ukakuta aina 15 za utengenezaji ambazo zimetengenezwa pale ikiwemo matumizi ya chengachenga zilizotumika kuchonga. Watu wetu wengi wanao-*deal* na madini hapa kwanza *skill* hizo hawana, lakini pili nadhani lazima tu-*define* tunataka tuongeze thamani kutoka *level* gani kwenda *level* gani kwa sababu mawe haya yanatofautiana ili waweze kutumia pia chengachenga hizo ambazo tunazungumza. Hata dhahabu hii ambayo tunaiiza sasa hivi *level/yake ya purification* haijafikia asilimia 100 ipo labda asilimia 70 inapouzwa nje bado kuna *technic* zingine zinazotumika ku-*purify*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nipate *commitment* ya Wizara watatenganisha vipi hili ili kuondoa kikwazo, hatuwezi kuwa na jibu moja kwenye maswali yanayotofautiana. Kwa sababu watumiaji wa vito hawafanani *design* ya uongezaji wa thamani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Madini.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa fursa hii. Namshukuru Mheshimiwa Kanyasu kwa kuweza kuwasemea wazalishaji wa madini haya ya nakshi au aina ya *dimension stone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kimsingi kwa upande wetu kama Wizara tumefanya vikao kadhaa

na wazalishaji hawa wa madini ya nakshi takribani viwanda tisa na walieleza hoja zao lakini na sisi pia kama Wizara na wataalam wetu ni suala ambalo tumeendelea kulifanyia kazi ili kuweza kuitafisiri sheria kwa upande wa suala la *value addition* au uongezaji wa thamani. Tumeanza kulifanyia kazi na hata hao wenye viwanda tisa wanafahamu tumeanza kuchukua hatua, *internally* tunataka tuone ni namna gani tunaweza kutoa tafsiri kwenye kila aina ya madini ni hatua ipi ya msingi ili ikifikiwa hiyo utasema basi kweli uongezaji thamani umeweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda tu kumwambia Mheshimiwa Kanyasu tumeanza kulifanyia kazi na nimshukuru kwa hoja hiyo. Nimuombe tu atupe nafasi tuweze kulikamilisha sisi pamoja na Tume ya Madini ili tuweze kuona endapo kutakuwa na haja ya kuweza kutoa mwongozo huo na utakuwa wa aina gani, kwa kiwango kipi basi Mheshimiwa Mbunge atawea kujulishwa ni hatua gani tumeweza kufikia. Kaka yangu nikuombe tu uweze kuridhika na haya usije ukafikia katika hatua ya kutoa shilingi nikajikuta na mtoto wangu huyu mdogo akakosa hata na maziwa halafu ikawa tabu sana. Kaka yangu hebu majibu haya yakutoshe. Nakushukuru. (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kanyasu, naona ameridhika.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika. (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi, nilimsikiliza Naibu Waziri Mheshimiwa Doto Biteko alivyokuwa anajibu alisema kwamba, kama Wizara wana mkakati wa kuwahamisha wachimbaji wadogo kutoka kwenye uchimbaji wa kubahatisha kwenda kwenye uchimbaji wa uhakika. Hakuwa *very specific* na jambo hili ni muhimu na la msingi sana kwa ajili ya uchumi wa nchi, kama

tukiwawezesha wachimbaji wetu wadogo wadogo hawa wakawa wachimbaji wakubwa, wakamiliki uchumi wa nchi maana yake Taifa tutakuwa tunakwenda sehemu nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea anatoka nje anayeitwa mwekezaji ilimradi anaonekana ni ngozi nyeupe, anakuja huku anafanya utafiti anapewa leseni na anajua kabisa kwenye eneo hili kuna kiwango hiki cha dhahabu au cha madini. Hiyo leseni anaipeleka kwenye mabenki ya nje anapewa mkopo anakuja kuchimba lakini ukiangalia yeye hana hata shilingi, ametumia mtaji wetu kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ufanuzi kwamba sisi kama nchi na niseme kabla sijagongewa kengele kwamba nitatoa shilingi kama sikupata maelezo ya kutosha, kwamba sisi kama nchi sasa hawa wachimbaji wadogo wadogo tulionao Tanzania ambao ndiyo wanaweza kuisababisha nchi ikatoka hapa ilipo kiuchumi tumejandaa vipi kuwasaidia kiuchumi ili kuwa wachimbaji wakubwa? Nataka *specific measures* ambazo kama Wizara mtazichukua, kama haikukaa vizuri nitatoa shilingi ili tuweze kujadili namna ya kuwasaidia wachimbaji wadogo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Doto Biteko ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na niseme tu kwamba namshukuru Mheshimiwa Ryoba kwa hoja yake. Ukweli ni kwamba mchakato wa kuwasaidia wachimbaji wadogo kuwatoa walipo kuapeleka hatua ya mbele kama tulivyosema kwenye hotuba yetu kwamba uchimbaji mdogo ni hadhi ya muda tu ndivyo tunavyoona sisi. Tunatamani tuwaone wanatoka kwenye uchimbaji wa kubahatisha kwenda kwenye uchimbaji wa uhakika, kwa kufanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunawarasimisha. Utakumbuka juzi tu hapa tumejibu swalii hapa Bungeni tunayo maombi mengi sana ya wachimbaji wadogo ambao

hawakuwa rasmi ya kuwapatia leseni, zaidi ya leseni 5,000 tumezigawa kwa wachimbaji wadogo ambao ni Watanzania. Nia ni kuwapa uwezo wa kumiliki maeneo hayo ili waweze kuchimba kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatua nyingine, kwa kutumia Taasisi yetu ya *GST* pamoja na *STAMICO* tutawafanya utafiti wa kujua viashiria vya madini viko wapi ili wahame huko kwenye kubahatisha bahatisha. Baadaye tuwape mafunzo waweze kuchimba kisasa kwa kuzingatia usalama mahali pa kazi lakini kwa kuzingatia usalama wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumzia na ni la kweli, tusipokuwa makini wapo wageni wanatumia nafasi ya uchimbaji mdogo wanakuja kuchukua leseni ya hapa Tanzania wanakwenda kukopa nje kwa kutumia *collateral* ya ndani hapa na uwekezaji hawafanyi ndani wanawekeza huko nje. Ndiyo maana mmeona wako wengine hata *retention lisence* tumefuta lengo ni kurudisha manufaa ya uchumi huu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe sana ndugu yangu, mwalimu mwenzangu, Mwalimu Ryoba, atupe shilingi tukafanye kazi ili mwakani apate cha kutuuliza. Sasa hata leo ukikatalia shilingi tutaenda kufanyaje kazi? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ryoba Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, kuwapa leseni na kuwarasimisha ni jambo moja, kuwafanya utafiti kwa kutumia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ryoba kwenye hii ngazi ya pili unasema kama umeridhika na maelezo ama unatoa shilingi ili wenzio wakuunge mkono. Ngazi hii hauchangii tena mpaka baadaye utakapofunga hoja.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakuja hapo kwamba...

MWENYEKITI: Huwezi kutoa maelezo, sema kama unatoa shilingi wenzio wakuunge mkono au umeridhika na maelezo.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na naomba kutoa shilingi tujadili lakini nilitaka unisikize hapo...

MWENYEKITI: Siwezi kwa sababu yeye sitompa nafasi ya kuchangia Mheshimiwa Ryoba, wewe sema unatoa hoja ya kutoa shilingi ili wenzio wakuunge mkono, ndiyo utaratibu ulivyo.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ili tuweze kujadili.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa, kwa hiyo, wabaki wamesimama wale wanaotaka kuchangia kwenye hoja hii. Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Dkt. Kafumu, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Naibu Waziri Mazingira Kangi Lugola, Mheshimiwa Mitolea, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Waziri utapewa fursa. Tuanze na Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Suala ambalo analiongelea Ryoba, ni pana sana. Mimi nimekuwa kwenye fani ya madini na Waheshimiwa Mawaziri wanafahamu, anachokiongelea Mheshimiwa Ryoba ni kwamba wanapokuja wawekezaji wanapata leseni kubwa ama leseni za katiki, ni nyaraka hizo hizo wanaondoka nazo wanakwenda kwenye mabenki aidha ya kwao ama ya ndani wanachukulia mikopo kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu benki haiwezi kukopesha mgodi na haiwezi kukopesha mgodi sio tu kwa sababu mtu hana leseni lakini *confusion* ambayo inakuwa

created kwa wachimbaji wadogo wadogo katika Taifa hili ni kubwa sana. *Attitude* ya Wizara kwa wachimbaji wadogo wadogo wa madini iko so negative kuliko *attitude* ya Wizara kwa wawekezaji wa nje. Wawekezaji wote wa nje wanatumia leseni na vitalu vya nchi hii kupata mikopo aidha mabenki ya nje ama ndani. Sasa *commitment* tunayotaka, Serikali ina mkakati gani, moja ya kutoku-create hiyo *negative attitude*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mererani na naomba Bunge hili liweke kumbukumbu, kama itaendelea hivyo ilivyo baada ya mwaka mmoja Mererani itafungwa, migodi karibia asilimia 60 imefungwa kwa sababu ya *negative attitude* dhidi ya wafanyabiashara wa madini. Hapa *commitment* siyo tu uwezo wa kupata mikopo lakini *commitment* pia ya Wizara kuelewa *industry* hii vizuri ili iweze kujua thamani halisi ya hivi vitu na namna ya kuwasaidia wawekezaji wa ndani katika uchimbaji wa madini.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ryoba. Wachimbaji wadogo ndiyo hasa Watanzania wenzetu, ndiyo hasa wanaoweza kubadilisha uchumi wa Taifa hili kwa kutumia haya madini tuliojaliwa kuwa nayo ili Tanzania ikang'ara na ikaonekana kuwa na uchumi mzuri badala ya kuwategemea wageni ambao kimsingi wametuibia sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutosheke na kuibiwa ambako kumefanywa na wageni, kumefanywa na hao wanaojiita wachimbaji wakubwa na sasa tuongeze nguvu kuhakikisha tunawasaidia wachimbaji wadogo wadogo wawze kuchimba na kuvuna madini ya nchi hii ambayo ni rasilimali ya nchi hii, ni rasilimali ya kwao kwa ajili ya kulinufaisha Taifa hili. Tukiendendelea kuwa kwenye michakato tu kila wakati madini haya yanayazidi kuondoka, wageni wanazidi kunufaika. Wenzetu wakipata hizo leseni wanaenda kukopea sisi hapa wa kwetu hawawezi kukopa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *speedya* Serikali katika kuhakikisha rasilimali hizi za madini zinawanufaisha Watanzania ni ndogo. Kila siku majibu yatakuwa ni haya haya, tunawarasimisha, tunatambua, siku zinakwenda na madini yetu yanazidi kuondoka. Sasa tunataka tuone *commitment* ya Serikali kwamba kweli sasa imebadilika inataka kuhakikisha kwamba Watanzania ndio wananufaika na madini yao. Tunataka Serikali ijielekeze katika hili ikiwezekana hata mseme kwamba sasa hivi hebu wachimbaji wageni kwanza wapumzike kwani tuna haraka ya nini, haya madini si yetu, hebu tujipange kwanza ili yaweze kuwanufaisha wazawa jamani. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nimemuelewa vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri na sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa hasa kwenye machimbo tunafahamu ili uweze kumkopesha mtu lazima ujue thamani ya madini yaliyoko pale chini. Moja ya kasoro inayofanya wachimbaji wadogo wasikopesheke ni kwa sababu wengi wanachimba machimbo ya *rushing* au ya kubahatisha. Benki haiwezi kutumia kama *collateral/machimbo* ambayo hakuna uhakika kuna thamani gani pale chini. Kwa kweli hoja ya kuwafanya wawe wengi na hoja ya kuwafanya wafanye utafiti na kugundua thamani ya madini yao ni ya muhimu kabla ya kuwakopesha. Kwa hiyo, nilimuelewa Mheshimiwa Naibu Waziri kuna hatua za kuchukua kabla ya kufikia *stage* ya kuwapa pesa waweze kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ryoba kwamba sasa hivi naishukuru Serikali mwelekeo huu wa kuhakikisha haya madini yanashughulikiwa

na yanachimbwa na yanazalishwa na Watanzania. Ni vizuri kabisa tukafikiria kuwasaidia wachimbaji wadogo ili wawe wachimbaji wakubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wako wachimbaji ambao wameshafikia labda kuwa wachimbaji wa kati kwa mfano Bwana Baraka kule Busolwa au Bwana Mwita ana mgodi wake kule Nyamongo na Bwana Kadeo yuko Geita kule, hawa Serikali inatakiwa iwape msaada maalum kwa sababu tunataka hii shughuli ya uchimbaji mdogo iwe kubwa lakini iwe ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Ryoba ni kwamba hebu tuwasaidie hawa Watanzania, hili suala la *indignation* ya hii *program* lazima ifanyike kweli. Nchi kama Australia kwa mfano wanawapa watafutaji wa madini na wachimbaji hela kutoka Serikalini ili kuwaimarisha. Naomba *commitment* ya Serikali hawa ambao wameonyesha tuwasaidie, tuwape hata fedha kwa sababu zitarudi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa sehemu kubwa tayari tumeshaelekeea kwenye mwelekeo ambao Mheshimiwa Ryoba ametaja, tayari mafunzo yameanza, leseni zote leo hazipo tena mikononi mwa watu ziko mikononi mwa Serikali, zimefutwa na wanaangalia upya utaratibu mzima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa tunafuatilia kwa karibu katika Ofisi zetu za Kanda tungepata utaratibu huo. Nilivyochangia nilisema kwamba kuna maeneo muhimu ambapo Serikali lazima iangalie kulinda Watanzania na wamekubali kwamba jambo hilo litafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kubwa na tutaendelea kuishauri Serikali ni kwamba kwenye *expertise*

yaani namna ya kufundisha wachimbaji wadogo na namna ya kuwezesha waendelee kusajiliwa vizuri kwa makundi ambapo watapata elimu ya kutosha ili suala hili sasa lifanyike kitaalamu. Muhimu kuliko yote, kama wenzangu walivyochangia na Mheshimiwa Kanyasu alivyochangia ni kwenye masoko na kufungua ile *Trade Fairya Arusha* ili Serikali iweze kupata mapato yake na wachimbaji wadogo waweze kuuza madini yao hapa hapa nchini kuliko kwenda nje ya nchi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Serikali kwa maana kwamba toka jana na leo na hata tunavyoona hii timu ambayo iko kwenye Wizara ya Madini inafanya kazi kama Wabunge wanavyotaka. Kwa sababu hii Wizara imegawanywa na hawa waliongia wanamtazamo mpya ule ule ambao ni mtazamo huo huo ambao Wabunge wanauzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri hoja ya msingi hapa ni kurudisha shilingi yao ili waweze kufanya kazi kwa sababu wote hapa tunaamini wanafanya kazi na maelezo yao yamejitosheleza kabisa na wako wazi. Mheshimiwa Doto tunamuona anavyohangaika, Mheshimiwa Nyongo mniamwona, Mheshimiwa Angella ametoka kwenye kujifungua na mnamuona anavyohangaika, mimi sioni shida. Tukubaliane kwamba tuwape kazi wafanye bajeti ijayo tutawauliza, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kangi Alphaxed Lugola.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naunga mkono maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Nashindwa kuelewa Mheshimiwa Ryoba anahitaji *commitmentya* namna gani kutoka Serikalini.

Nimhakikishie Mheshimiwa Ryoba kitu ambacho Serikali ya Awamu ya Tano inakifanya kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuchukua umakini mkubwa kwenye sekta ya madini, tumechukua uzoefu kwenye Serikali ya Awamu ya Nne ambapo wachimbaji wadogo walipewa ruzuku, fedha za bure wengine kwenda kununua mashine hawakununua wakaenda kuolea na kuongeza wake wengine, wengine ndiyo hao wakanunua magari ya kifahari hawakuingiza kwenye uchimbaji mdogo. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali sasa tumekuambieni kwamba wachimbaji wadogo tunawarasimisha hata wale ambao hawakuwa na leseni wapatiwe leseni. Mfano mzuri uko pale Isizo tumeenda juzi na Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna Mtanzania pale ambaye anachonga mawe unadhani yametoka China, yule sasa hivi kuna Wazungu ambao wanataka kuingia naye ubia, ni kwa sababu ana leseni, ni kwa sababu Serikali imewasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ryoba shilingi yake hiyo itakuwa ni muhimu sana iwapo atamrudishia Mheshimiwa Waziri ili hao wachimbaji wadogo ambao anawatetea ambao Serikali ya Awamu ya Tano inatatea wanyonge na tumeshaonyesha mfano na tuko bega kwa bega kuwasaidia hao wanyonge anaowatetea, hatuko mbali sana Mheshimiwa Ryoba. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Madini.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nimuombe tu ndugu yangu Mheshimiwa Ryoba aweze kuelewa na kukubali maelezo ya Serikali. Bahati nzuri Mheshimiwa Getere na wengine wameeleza, hata katika maonyesho yetu tuliwaleta hawa kaka Mwita pamoja na

Kadio. Ukimchukulia Mwita wa *Mara Mining*, tuliweza kumpatia ruzuku ya takribani milioni 100 na alikuwa ni mchimbaji wa chini kabisa amefikia mtaji wa milioni 700 na anaelekea kuwa mchimbaji wa kati. Ukija kwa Kadio hivyo hivyo, ukija kwa Baraka wa Busolwa ndiyo kabisa alianza kama mchimbaji mdogo tumeenda naye, tumemlea, tumemwezesha sasa hivi ana mtaji wa takribani dola milioni 25. Ana mgodi wa kisasa kabisa kwa kweli huwezi kuamini kama ni Mtanzania ambaye alianza katika uchimbaji mdogo ameweza kufikia hapo. Mheshimiwa Doto alieleza lakini pia katika hotuba yangu nilieleza lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawalea ili waweze kuelekea katika uchimbaji wa kati na hatimaye waweze kufikia katika uchimbaji mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi tuliweze kujenga migodi ya mfano, ukiangalia mfano kama Lwamgasa tumeweka mitambo ya uchenjuliaji, tumeweka *mine shaft* pale waweze kuja waweze kuona mbinu bora za uchimbaji, za kiusalama, za afya na mazingira lakini pia ni namna gani wafanye waweze kuzalisha uzalishaji mkubwa zaidi. Tumeweza kujenga vituo vya umahiri takribani vituo saba na Musoma ipo na kwa kuwa anatoka Serengeti pia ye ye na wenzake wote wa Serengeti na Musoma wataweza na wenyewe kunufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia kwenye maeneo ya *rush*, ukichukulia ile ya Bingwa ya Geita ukiweza pia kuichukulia Mwakitalyo walikuja pale, eneo lilikuwa na leseni za watu lakini tumewaachia wanaendelea kuchimba. Yote hiyo ni kuhakikisha kwamba na wenyewe wanajipatia riziki lakini hatimaye waweze kukua na kuwa wachimbaji wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hiyo tu, ukiangalia katika suala zima hata la *local content* pamoja na huu uchimbaji utaona azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunawawezesha wazawa. Pia lengo letu kubwa huko baadaye ni kuweza kuifanyia mapitio Sera yetu ya Madini ya mwaka 2009 ili kuona kunakuwa na vivutio vya aina gani

kwa wachimbaji wetu wadogo ambao tunajua kabisa leseni hizi za *PML* hazitolewi kwa raia wa kigeni ni kwa wachimbaji wadogo ambao ni Watanzania. Lengo letu kubwa ni kuona namna gani tunawalea ili na wenyewe waweze kuzalisha kwa faida na waweze kuchangia katika pato letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata katika llani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 tunaendelea kuwatafutia masoko, tunawapatia taarifa mbalimbali za teknolojia na masoko. Kama tulivyoeleza hapa, tumeanza mchakato wa kuanzisha masoko haya ya dhahabu na madini mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe tu kaka yangu Mheshimiwa Ryoba aweze kutuelewa, atuachie hiyo shilingi twende kuzalisha ili aweze kuja kutupima mwaka ujao haya tunayoyaeleza kama kweli tumeweza kutekeleza au laah! Kila mwaka tunatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kwa mwaka ujao wa fedha tumeahidi takribani maeneo mapya manne na tunaamini yataweza kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo. Naamini maelezo haya kwa niaba ya Wizara ya Madini yataweza kuwa yamemtosheleza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoha hoja Ryoba Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikilza sana Mheshimiwa Waziri na Wabunge wengine walivyochangia. Nimefurahia sana nilivyomsikiliza Waziri wengine kuliko Mheshimiwa Kangi, maana Waziri kasema vizuri kabisa kwamba kuna wachimbaji wadogo walipewa fedha, walilelewa na sasa hivi mitaji yao imekua, Mheshimiwa Kangi kasema walienda kuolea sidhani kama ni nzuri. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme sina haja sana na shilingi ya Waziri. Nia yangu ama nia yetu sote ni kuona hawa wachimbaji wadogo wanapata namna ya kupata fedha ili wapate ile teknolojia wachimbe wenyewe

itusaidie Watanzania wote. Vinginevyo sina shida na shilingi yake, ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini nizungumzie hoja ya tozo za chumvi ambazo Mheshimiwa Waziri amezitolea maelezo kuna tozo karibia 16 ambazo zinawafanya wazalishaji wa chumvi washindwe kuingia katika ushindani wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona namna ambavyo wazalishaji wa chumvi wameleta malalamiko kwa Serikali na kuomba wasaidiwe kupunguziwa hizi tozo mbalimbali. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inafikiria kukaa na kuona namna gani ya kupunguza tozo hiz. Inanipa mashaka, unaposema unafikiria maana yake inaonekana kwamba hauko tayari kusaidia. Ningombwa Mheshimiwa Waziri anipe majibu ya uhakika ni kwa namna gani Serikali itaweza kusaidia kupunguza hizi tozo ili wazalishaji wa chumvi waweze kuingia katika ushindani wa soko hilo. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Madini.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida kuhusiana na hatua gani labda tutazichukua katika kuhakikisha kwamba tozo hizi ambazo zimekuwa ni nyingi na nyingine zimeonekana labda ni kero katika uzalishaji wa chumvi. Napenda tu kumhakiishia dada yangu nilitoa maelekezo kwa upande wa Wizara yangu Katibu Mkuu aliongoza vikao akishirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Katibu Mkuu Viwanda na wengine na tumeanza kuchua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ya tozo na kodi yana michakato. Tunajua wote kuna Muswada ule wa Fedha huwezi tu ukafuta ghafla, kuna hatua zake. Nimuombe

tu dada yangu aweze kutukubalia tuendelee katika hatua zetu Serikalini ili tuweze kujenga hoja katika suala hili na hatimaye siku za mbele liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini litaweza kuonekana kwa sababu katika kikao waliazimia tayari takribani tozo tisa ziweze kuondolewa lakini bado ni hatua. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba ule upungufu wa au ile *gap* ya uzalishaji wa takribani asilimia 46 ambayo inatoka nje basi iweze kuzalishwa humu ndani. Nimwombe tu dada yangu Mheshimiwa Hamida aweze kutuelewa ili tuweze kulifanya kazi kuwanufaisha wazalishaji hawa wa chumvi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamida Abdallah, naona umeridhika?

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimeridhika na majibu hayo lakini Serikali ione umuhimu sasa wa kukaa kwa haraka na kuona namna ya kuwasaidia wazalishaji wa chumvi ili waweze kuingia katika soko. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni sera ya Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha wachimbaji wadogo ili waweze kujiongezea kipato na kuboresha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya madini inakua siku hadi siku kwa sababu ya kuongezeka kwa teknolojia na uelewa wa wananchi kwa ujumla wake. Naomba nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali ina mpango gani wa kusogeza huduma karibu na wananchi na wachimbaji wadogo ambao sasa inaonekana wameachwa mbali? Nina maana ina mpango gani wa kuanzisha Ofisi za Madini katika kila Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufanuzi wa kina na kama maelezo hayatatosha basi nakusudia kushika shilingi. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Madini, ufanuzi.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe tu kaka yangu Mheshimiwa Ngombale mwaka jana tuliweze kupitisha marekebisho ya Sheria ya Madini mwezi Julai. Katika vifungu nya sheria ile, pamoja na kwamba kwa hivi sasa katika mfumo wetu tulikuwa na Ofisi za Kanda takribani 10 katika mikoa 16, tuna ofisi 26 lakini baada ya sheria ile kupitishwa maelekezo au masharti ya sheria ile ni kwamba kila mkoa uweze kuwa na Ofisi ya Madini ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria imeenda mbali zaidi kila mgodi utakuwa na Afisa Mgodi Mkazi ambaye ni *resident pale* wa kuweza kusimamia masuala mazima ya ukaguzi, uzalishaji pamoja na mambo mengine. Kwa hiyo, badala ya kwenda katika Halmashauri sheria imeenda mbali zaidi ni katika kila mgodi *especially* mkubwa na wa kati itakuwa na Afisa wake Madini Mkazi. Kwa hiyo, naamini hawa wataweza kutoa huduma hizo vizuri zaidi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngombale.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Waziri sijaridhika nayo, naomba nitoe hoja ili basi Washeshimiwa Wabunge waweze kupata nafasi ya kujadili.

MWENYEKITI: Hoja haijaungwa mkono. (*Makof*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuzisome vizuri hizi Kanuni zetu. Sehemu inayozungumzia hoja za humu ndani ni moja tu, isome vizuri. Mheshimiwa Rashid hapo aliwahi

kuomba mwongozo, muoneshe kanuni jirani yako hapo. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyochangia kwenye mchango wangu nilizungumzia madini ya batii ambayo naamini yanapatikana maeneo mengi ikiwemo na Kyerwa. Madini haya hayajaletewa utaratibu hasa wa soko wachimbaji wadogo hao wanapochimba wanapata hela ndogo sana. Mbaya zaidi madini haya kwa sababu bado hayajawekewa utaratibu mzuri nchi jirani ndio wanaofaidi kwa sababu yanatoroshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine wawekezaji ambaao wamekuja kuwekeza viwanda vyta uchenjuaji kwa kweli wamekuwa wakizungushwa sana na inaonesha kama madini haya hayana umuhimu. Niombe *commitment* ya Serikali ni lini Muswada huu ambaao Mheshimiwa Waziri amesema utaletwa haraka tuweze kuokoa madini haya ambayo ni muhimu. Madini haya ni ya miaka mingi nimezaliwa nakuta madini haya yapo na yalianza kuchimbwa hata kabla Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe *commitment* ya Serikali ni lini Muswada huu utaletwa ili uweke utaratibu mzuri wa kuweza kuuza madini haya. Vinginevyo kama sitaridhika nitashika shilingi. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Madini.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Bilakwate kwa namna ambavyo anawatetea wananchi wake wa Kyerwa hususani katika kuhakikisha kwamba kunakua na soko katika madini haya ya Batii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Bilakwate kama nilivyoeleza katika majibu ya hoja zangu, tunao Mkataba ule wa *ICGLR* wa mwaka 2006 pamoja na Mkabata wa *ICGLR* kuhusiana na matumizi au *illegal exploitation* katika madini haya ya batii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali, bahati nzuri na Mheshimiwa Kabudi yupo hapa, ukiangalia katika ule mkataba wa kwanza ni wa Wizara ya Mambo ya Nje na tayari wao kwa upande wao ndani wameanza kuchukua hatua na naamini utakapokamilika basi kwa hakika utaweza kuletwa katika Bunge lako. Katika mkataba ule wa pili hauwezi kuridhiwa mpaka wa kwanza uanze na tumeshanza mashauriano na Mheshimiwa Prof. Kabudi na kimsingi naamini yeye ndiyo atakayekuwa mtu sahihi kabisa kwa sababu Mkataba ule wa *Illegal Exploitation* unahusiana na maliasili, madini lakini pia ni masuala ya *natural wealth*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyokumbuka katika Sheria yetu ile ya Madini iliambatana na Sheria ile *Permanent Sovereignty* pamoja na *Natural Wealth* na yeye ndiye alikuwa ni mtu sahihi kwa sababu ulikuwa ukigusa sekta nyingi na kwa kweli aliweza kuupitisha na tunaamini pia katika huu, tayari ameshaanza kuchukua hatua. Kwa hiyo, tumuombe tu Mheshimiwa Mbunge aweze kutupa nafasi, kupitia vikao vya Bunge pamoja na vikao vyetu vingine ndani Serikalini ili tuweze kuwasillisha Muswada au Mkataba huu haraka iwezekanavyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bilakwate.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya maeleo ya Mheshimiwa Waziri na ameyasema haya Bungeni basi mimi naachia shilingi yake ili utaratibu mwingine uendelee. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* Sh.794,568,140/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*Sh.794,089,383/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD A. SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda tu kutaka kuelewa kwenye item 22014 ambayo kuna Sh.22,400,000, *Hospitality Supplies and Services*. Hii ni Wizara mpya na kwa mujibu wa randama inasema kifungu kinatumika kwa ajili ya kulipia gharama za chakula, maji, vinywaji wakati wa mikutano muhimu ya kikazi inayoratibiwa na Idara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata kwenye *subvote* nyingine, Wizara ya Madini mmejjipangia fedha nyingi za vinywaji, viburudisho, chakula na kadhalika, shilingi milioni 22, shilingi milioni 18, shilingi milioni 90, sasa tunapata mashaka makubwa. Kuna baadhi ya vifungu mmeweka fedha za mfanyakazi bora au kuna sherehe za Mei Mosi na sherehe nyingine lakini kuna mahali mmeweka ni vinywaji tu, viburudisho, chakula na fedha mmeweka nyingi sana huku mmesema mnabana matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watuambie, Madini na kula inakuwaje mwaka huu? Tatizo nini zaidi? Mbona mmejjipangia fedha nyingi za chakula ukiachia mambo ya mfanyakazi bora na mambo mengine, tena kwenye *subvote* nyingi tu. Ukiangalia kwenye *Hospitality Supplies and Services* mmeweka mambo hayo, tatizo nini? Nawashangaa sana. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud, hutaki tupewe hata maji tukienda huko? Mheshimiwa Naibu Waziri Stanslaus Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Napenda tu kumtaarifu Mheshimiwa Masoud kwamba, kipengele hiki kipo upande wa utawala na Wizara yetu ya Madini sasa hivi ina taasisi nyingi. Kwanza tuna Tume mpya ya Madini ambayo inatumia fedha na ni Ofisi yenye watu wengi, tuna Taasisi ya MRI, GST, Ofisi Kuu ya Wizara, TEITI ambayo yenye ni taasisi, STAMICO, kwa hiyo, watu ni wengi sana. Mheshimiwa Masoud hata kiasi hiki tulichowekewa ni kidogo sana, sasa ukituonea gere kwamba tuna fedha nyingi hapo utakuwa umetuonea. Tuachie tu Mheshimiwa ili tuweze kutenda kazi, tumejinyima vya kutosha, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud kwa kuona afya zilizoko hapa, ameridhika kabisa. (*Kicheko*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.454,200,594/=
Kif. 1005 – <i>Legal Service Unit</i>	Sh.482,056,585/=
Kif. 1006 – <i>Government Comm. Unit</i>	Sh.405,895,755/=
Kif. 1007 – <i>Procurement Mgt</i>	Sh.419,708,390/=
Kif. 1009 – <i>Mgt Information System Unit</i>	Sh.790,437,099/=
Kif. 2001 – <i>Minerals Division</i>	Sh.30,907,838,158/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 100 – Wizara ya Madini

Kif. 2001- <i>Minerals Division</i>	Sh.19,620,964,000/=
---	---------------------

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA MADINI: Mheshimwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kanuni ya 104(3)(a) na (b), kwamba Bunge lako liliaka kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji . *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kufikia hapa Bunge limepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Madini. Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuwapongeza

sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri na Watendaji wote kwa kazi nzuri mlionfanya ya kuleta haya makadirio na naamini mwakani tutapata maswali ya kuuliza hapo. Kwa niaba ya Bunge zima tunashukuru sana Kamati kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kulishauri Bunge hili namna ambavyo Wizara imeleta hayo makadirio yao mbele ya Kamati. Tunawashukuru pia Wabunge wote mlionfanikiwa kuchangia kwa sababu mmefanya kazi nzuri ya kuishauri Wizara na wao wamekiri hapa Naibu Mawaziri lakini pia Waziri namna ambavyo ushauri wenu utawasidia katika kutekeleza bajeti hii ambayo tumepitisha leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla wetu wote mmefanya kazi nzuri. Tuwatakie kila la kheri katika utekelezaji sasa wa haya mlionyaleta na kuahidi na wakati Wabunge wakitaka ufanuzi mmesema kwamba wawape nafasi mkafanye kazi. Kwa hiyo, tunaamini mwakani yale yote Wabunge waliyoyazungumza yatakuwa yamepatiwa ufumbuzi na zile ambazo ni changamoto mtakuwa mmezifanya kazi.

Waheshimwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninayo matangazo machache, tangazo la kwanza ni la mgeni, kuna mgeni ambaye hakuwepo asubuhi na huyu ni Ndugu Mabeyo Ngowelo, ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Kangi Lugola, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ni mdogo wake kutoka Mwibara. Karibu sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine tulitangaza asubuhi lakini tunapenda kuwakumbusha kwamba kesho kutakuwa na hafla ya uwasilishaji wa Taarifa za Kamati Maalum alizoziunda Mheshimiwa Spika kuhusu sekta ya uvuvi wa bahari kuu na gesi asilia. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kesho saa tatu na nusu asubuhi, wakati ambapo Mheshimiwa Spika atapokea taarifa hizi na kuiqidhi Serikali ili iweze kuyafanya kazi kama ambavyo ni wazi katika michango yenu mmepongeza hatua zake alizozichukua hapo awali kwenye suala la hii Wizara ya

Madini. Kwa hiyo, kesho mnakumbushwa Waheshimiwa Wabunge kuhuduria.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine la kuwakumbusha ni la Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, kwamba kesho saa kumi kutakuwa na mechi kati ya *Ndugai Boys* na Chuo cha *St.Johns* kwa upande wa *football* na *netball*. Pia siku ya Jumapili *Ndugai Boys* tena watashindana na *Kadutu Boys* na michezo hii itafanyika Uwanja wa Jamhuri. Waheshimiwa Wabunge na umma wote uliopo Dodoma mnakaribishwa sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu tarehe 4 Juni, 2018, saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.50 Jioni Bunge Lillahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 4 Juni, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*